

SIKU
40
za maombi
IBADA YA KUTUANDAA KWA UJIO WA YESU
Enendeni mtandaoni kote ministry, maarifamtandaoni.com na RohoyaUnabii.Africa
Cover By:
JAKABOSO
0656 724 294

# UWE TAYARI—YESU ANAKUJA

# YALIYOMO


UTANGULIZI.....1

SEHEMU YA I—UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU.....2

SIKU YA 1

KAZI MBILI ZA ROHO MTAKATIFU.....3

SIKU YA 2

KUPOKEA UBATIZO WA ROHO BAADA YA PENTEKOSTE.....5

SIKU YA 3

FAIDA ZA KUPOKEA UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU.....7

SIKU YA 4

KRISTO NDANI YAKO.....10

SIKU YA 5

UBATIZO WA ROHO NA UTII.....13

SIKU YA 6

KUMHUZUNISHA ROHO.....16

SIKU YA 7

ROHO NA MVUA YA MASIKA.....19

SIKU YA 8

UBATIZO WA ROHO NA MAREJEO YA KRISTO.....22

SEHEMU YA II—UBATIZO WA ROHO NA MAOMBI.....25

SIKU YA 9

MSUKUMO WA SALA UNAOTOLEWA NA ROHO.....26

SIKU YA 10

KIELELEZO CHA SALA CHA YESU NA WANAFUNZI.....29

SIKU YA 11

KWA NINI MAOMBI NI MUHIMU?.....32

SIKU YA 1

KUOMBA KATIKA ROHO.....35

SIKU YA 13

KUUNGANA KWA AJILI YA MAOMBI KATIKA ROHO.....37

SIKU YA 14

MAOMBI STAHIMILIVU KATIKA ROHO ........ 40
SIKU YA 15
MAOMBI YA MAOMBEZI KATIKA ROHO KWA AJILI YA WENGINE ........ 42
SIKU YA 16
KUOMBA AHADI ZA MUNGU KATIKA ROHO ........ 45
SEHEMU YA III—UBATIZO WA ROHO NA UINJILISTI ........ 49
SIKU YA 17
KAZI YA INJILI YAKAMILIKA CHINI YA UWEZA WA ROHO MTAKATIFU ........ 50
SIKU YA 18
UBATIZO WA ROHO NA USHUHUDA ........ 53
SIKU YA 19
UMUHIMU WA UBATIZO WA ROHO KATIKA KUSHUHUDIA ........ 56
SIKU YA 20
UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU NA KUANDAA NJIA KWA AJILI YA UJIO WA KRISTO ...... 61
SIKU YA 21
TATIZO LA KANISA LA LAODIKIA ........ 64
SIKU YA 22
SULUHISHO LA HALI YA LAODIKIA YA KANISA ........ 67
SIKU YA 23
MAOMBI NA UINJILISTI ........ 70
SIKU YA 24
MBINU YA KRISTO YA UINJILISTI ........ 74
SEHEMU YA IV—UBATIZO WA ROHO NA KUKAA KATIKA KRISTO ........ 77
SIKU YA 25
NJIA YA KUGUNDUA ........ 78
SIKU YA 26
MAPAMBANO YA MKRISTO ........ 81
SIKU YA 27
UWEZO WA DHAMBI KUVUNJWA ........ 85
SIKU YA 28
KRISTO ANATOA USHINDI ........ 88
SIKU YA 29
HAKI KWA IMANI ........ 92
SIKU YA 30

AMRI ZA MUNGU NA KUKAA KATIKA KRISTO ........ 95
SIKU YA 31
KUISHI NDANI YA KRISTO NA UTUMISHI ........ 99
SIKU YA 32
MAPUMZIKO YA SABATO ........ 102
SEHEMU YA V—UBATIZO WA ROHO NA USHIRIKA ........ 105
SIKU YA 33
KITU FULANI KINAKOSEKANA ........ 106
SIKU YA 34
KANISA LA AWALI NA USHIRIKA ........ 109
SIKU YA 35
UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU NA VIKUNDI VYA USHIRIKA ........ 113
SIKU YA 36
KANISA ........ 116
SIKU YA 37
FAMILIA YA MUNGU ........ 118
SIKU YA 38
MATUNDA YA ROHO NA USHIRIKA ........ 121
SIKU YA 39
KARAMA ZA ROHO NA USHIRIKA ........ 124
SIKU YA 40
VIKUNDI VYA USHIRIKA NA UKUAJI WA KANISA ........ 128
Kiambatanisho A: Orodha ya Maombi ya Kila Siku ........ 131
Kiambatanisho B: Vitendo vya Kuonyesha Upendo Wako ........ 132
Kiambatanisho C: Mapendekezo ya Salamu kwa Mawasiliano ya Maombi ........ 133
Kiambatanisho D: Baada ya Siku 40 za Maombi na Masomo ya Kiroho ........ 134

**SHUKRANI ZOTE KWA MUNGU WA MBINGUNI**

TABARUKU

Watafsiri, Waombezi, Wahariri, Washauri, Wahakiki, Wataalamu wa Teknolojia, na watia moyo wote, Marafiki na Ndugu

1. Grace Momadi-Masaka- Jersey, Marekani
2. Elias Luwela-Sumbawanga, Tanzania
3. David Masaka -Pennslyvania, Marekani
4. Kwandu Kasiri-Mpagalushu- Bariadi, Tanzania
5. Daniel Nyangaresi Masaka- Kisii, Kenya
6. Musa Budodi-Shinyanga, Tanzania
7. Walter Nehemia-Rorya, Tanzania
8. Sandra Barron-North Carolina, Marekani
9. Baraka Ndege Aruya – Morogoro, Tanzania
10. Mbusi Mpagalushu-Arusha, Tanzania

# UTANGULIZI

Hii ni tafakari ya siku 40 za maombi na masomo iliyokusudiwa kuandaa kanisa la MUNGU kwa ajili ya kuja kwa mara ya pili kwa Kristo, na pia kuwafikia wengine kwa maandalizi ya tukio hilo kuu. Maandalizi haya huanza na washiriki wa kanisa walio tayari kujitolea kwa siku 40 za maombi na tafakuri ili kukuza uhusiano binafsi wa karibu na Yesu Kristo, na pia kuwafikia watu watano ambao BWANA amewaweka moyoni mwao kuwaombea kila siku.

Yesu alisema, 'Ikiwa wawili kati yenu watakubaliana duniani kuomba kitu chochote, watapewa na Baba yangu aliye mbinguni' (Mathayo 18:19). Kuna nguvu kuu katika maombi ya pamoja, na kuna faraja na nguvu ya kiroho katika ushirika wa Kikristo. Inashauriwa upate mwenza wa maombi ili kushirikiana naye, kwa simu au ana kwa ana, kila siku katika kipindi hiki cha siku 40.

Kwa faida kubwa zaidi, inapendekezwa pia kuunda kikundi cha watu kadhaa mtakaotumia kitabu hiki cha mafundisho ya kiroho. Inafaa kukutana mara moja kwa wiki ili kushiriki na kuomba pamoja. Kila mshiriki achague mwenza wa maombi wa kila siku. Kwa njia hii, kila mmoja atabarikiwa zaidi wakati wa siku hizi 40.

Kila somo limefuatiwa na maswali ya kutafakari na kujadili binafsi, pamoja na lengo la maombi kwa siku hiyo, likijumuisha 'aya ya maombi.'

Ikiwa unataka kukuza uhusiano wa karibu na Yesu na kuwafikia wale ambao MUNGU amekuonyesha, iwe ni wanafamilia, marafiki au wafanyakazi wenzako, basi kitabu hiki ni kwa ajili yako.

# SEHEMU YA I—UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU

## SIKU YA 1

## KAZI MBILI ZA ROHO MTAKATIFU

Wazo la ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kwamba kuna kazi mbili za Roho: ya kwanza ni kutuongoza kumkubali Kristo na kubatizwa kwa maji. Hii ni kazi ya Roho kwa kila mtu. Kazi ya pili ya Roho ni kumjaza Mkristo uwepo wake ili aishi maisha ya Kikristo kwa uhalisi na kufanya kazi za MUNGU. Hii ndiyo inaitwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kazi hii si kwa wasioamini bali ni kwa wale waliompokea Yesu Kristo. Yesu alisema ulimwengu hauwezi kumpokea kwa namna hii (Yohana 14:16-17).

Yesu ni mfano wetu katika mambo yote. Alizaliwa kwa nguvu ya Roho, akaongozwa na Roho kutoka utotoni hadi utu uzima, na akabatizwa kwa maji. Baada ya ubatizo wake wa maji, aliomba, ndipo akapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu (Luka 3:21-22).

Baada ya kujazwa na Roho aliweza kuanza huduma yake kwa nguvu, kushinda majaribu ya Shetani, kuhubiri, kufundisha, kuponya wagonjwa, na kufukuza pepo (Luka4:1-19).

Yesu alisema wote wamwaminio watafanya kazi alizozifanya, na hata kubwa zaidi, kwa sababu ataenda kwa Baba na kumimina Roho Mtakatifu (Yohana 14:12).

Hii ina maana kwamba tunapopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, tunapewa nguvu ile ile iliyokuwa ndani ya Kristo. Kabla ya kujazwa kwa Roho, MUNGU yu pamoja na mwamini kwa sababu alimwita amkubali Kristo na kubatizwa kwa maji. Lakini nguvu kamili ya Roho inakuja baada ya ubatizo wa Roho Mtakatifu (Matendo 1:4-8).

Ubatizo wa Roho Mtakatifu unapatikana kwa kila Mkristo leo. MUNGU ameahidi kumpa kila aombaye kwa imani (Luka 11:13; Wagalatia 3:14).

Masharti mawili ya kupokea ni: kwanza, kumpokea Kristo kama Mwokozi wako; pili, kufanya uamuzi wa kujitolea maisha yako kikamilifu kwake. Ukishafanya hivyo, unaweza kuomba kwa imani ili ujazwe na Roho Mtakatifu.

**Sala Kielelezo:**

Baba, nakushukuru kwa kuniongoza nimkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu. Naomba unisamehe dhambi zangu zote. Ninatamani kujitoa kwako asilimia mia moja. Nakushukuru kwa ahadi yako ya kunijaza kwa Roho wako Mtakatifu. Sasa

ninadai ahadi ya ubatizo wa Roho Mtakatifu maishani mwangu. Baba, nijaze kwa Roho wako na udhihirishe kwangu matunda yake yote. Naomba uwepo wa Yesu ukae nami ili tabia yake ionekane kwangu kikamilifu. Ninadai ahadi yako ya kuniwezesha kwa Roho wako kukutumikia. Kwa jina la Yesu, Amina.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Ni kazi zipi mbili za Roho Mtakatifu?
- Nani anastahili kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu?
- Taja faida mbili za kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.
- Je, unatamani kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu leo?

**Kujishughulisha Kuomba**

Fikiria kwa maombi kile unachoweza kufanya kuonyesha unawajali wale walio katika orodha yako ya kuwaombea. Wasiliana na kila mmoja, ukiwaambia kwamba unawaombea, na waulize kile wanachotaka uwaombee kwa niaba yao. Amua ni nani awe mwenza wako katika maombi unapoomba katika siku hizi 40 za maombi.

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU awabatize kila mmoja kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU afungue uelewa wenu unapojifunza kesha hili kila siku
- Ili MUNGU awabariki na ushirika wenu pamoja na mwenza wako wa maombi
- Kwa ajili ya kila mmoja wa wote mliowaorodhesha kuwaombea.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

“Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea; Nitakushauri, jicho langu likikutazama.” (Zaburi 32:8).

*Tuongoze na tufundishe, BWANA, ili daima tuwe chini ya maongozi Yako maishani na kanisani kwetu.*

## SIKU YA 2

## KUPOKEA UBATIZO WA ROHO BAADA YA PENTEKOSTE

Yesu aliwaahidi wafuasi wake kuwabatiza kwa Roho Mtakatifu ili wawe na nguvu ya kuchukua injili kwa ulimwengu wote (Matendo 1:4-8). Ahadi hii ilitimia siku ya Pentekoste wakati Roho Mtakatifu alipojaza wanafunzi na wakaanza kunena kwa lugha mbalimbali (Matendo 2:1-4).

Lakini ubatizo wa Roho Mtakatifu haukuwa tu kwa wanafunzi wa Pentekoste. Hili ni tukio linalopatikana kwa kila Mkristo tangu wakati huo. Katika Matendo 10:44-47 na Matendo 11:15-17, tunajifunza kuwa Roho aliwajilia hata wale waliokuwa wasio Wayahudi walipokuwa wakisikiliza neno la MUNGU, na wakajazwa kama vile mitume walivyopokea.

Pia tunaona mfano wa Samaria katika Matendo 8:12-17. Waliamini, wakabatizwa kwa maji, lakini bado hawakuwa wamepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mitume Petro na Yohana walienda huko, waliwawekea mikono na kuwaombea, ndipo Roho akawashukia.

Mfano mwingine ni Sauli (baadaye Paulo) aliyepokea ubatizo wa Roho kupitia sala na kuwekewa mikono na Anania kabla ya ubatizo wake wa maji (Matendo 9:17-18). Hali kadhalika, wanafunzi wa Efeso walipokea kwa njia hiyo hiyo walipoombewa na Paulo (Matendo 19:1-6).

Tunajifunza kwamba ubatizo wa Roho na ubatizo wa maji ni mambo mawili tofauti. Ubatizo wa maji huonyesha kuokoka, lakini ubatizo wa Roho huleta nguvu ya kuishi na kushuhudia. Roho ya Unabii inasema: “Tunachohitaji ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Bila hili, hatuko tayari kwenda ulimwenguni, kama vile wanafunzi walivyokuwa baada ya kusulubiwa kwa BWANA wao” (Review and Herald, 1890).

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Kwa nini Yesu aliwaambia wanafunzi wake wasubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu?
- Ni lini wanafunzi walipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu?
- Je, kila Mkristo alipompokea Kristo au kubatizwa kwa maji, alipewa pia ubatizo wa Roho?
- Waumini wa Samaria walipokeaje ubatizo wa Roho Mtakatifu?
- Sauli (Paulo) alipokeaje ubatizo wa Roho?

- Roho ya Unabii inasema nini kuhusu umuhimu wa kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu?
- Je, kuwekewa mikono ni lazima ili kumpokea Roho Mtakatifu?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kwa Roho wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU atumie nguvu za Roho kupitia maisha yenu.
- Kwa ajili ya Wale walio katika orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Ee BWANA, kumbuka rehema zako na fadhili zako, Maana zimekuwako tokea zamani." (Zaburi 25:6).

*Ee MUNGU, utuhurumie na utusamehe dhambi zetu. Turejeshee upendo wako na utukuze jina lako kupitia maisha yetu.*

## SIKU YA 3

## FAIDA ZA KUPOKEA UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU

Ni nini hutokea tunapomwomba MUNGU ubatizo wa Roho Mtakatifu?

Baadhi ya mabadiliko ambayo ujazo wa Roho huleta katika maisha ya mpokeaji ni:

- Shauku kubwa zaidi ya kujifunza Neno la MUNGU.
- Maisha ya maombi yenye bidii zaidi.
- Toba ya kina kwa dhambi zetu.
- Mabadiliko katika mitindo ya maisha na shughuli zetu.

Ujazo wa Roho ni muhimu kwa muumini kutembea kwa ushindi ndani ya Kristo. Kulingana na Biblia, mtu hamjui Kristo kwa ukamilifu wa maana yake ya kiroho bila ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Hii imeonyeshwa katika mfano wa wanawali kumi (Mathayo 25:1-13). Yesu aliwaambia wanawali wajinga, waliokuwa bila mafuta (Roho Mtakatifu): "Siwajui ninyi" (aya ya 12).

Kwa hiyo, kuujua ukweli au hata kushiriki katika huduma mbalimbali si mbadala wa kumjua Kristo kwa karibu kupitia ujazo wa Roho Mtakatifu.

Ubatizo wa maji unaweza kulinganishwa na sherehe ya ndoa, ilhali ubatizo wa Roho unalinganishwa na hatua ya "bibi arusi kumjua bwana arusi wake." Ni jambo ambalo Shetani hulipinga sana, kwa sababu anajua ujazo wa Roho huvunja nguvu zake katika maisha ya muumini.

Kuelewa na kupitia ujazo wa Roho Mtakatifu ni jambo la muhimu sana — linakuja mara baada ya kumkubali Kristo kama Mwokozi. Hakuna kazi nyingine muhimu zaidi kwa muumini kuliko kutafuta ujazo wa Roho na kujifunza kutembea kwa ushindi katika Roho.

Sehemu nyingine muhimu ni kwamba tunapaswa kuomba ujazo huu kila siku. Sio uzoefu wa "mara moja na basi." Paulo alisema: "Lakini mtu wa ndani anafanywa upya siku kwa siku" (2 Wakorintho 4:16). Tunahitaji kufanywa upya na Roho kila siku ya maisha yetu.

Paulo pia alisema: "Msiwivie mvinyo… bali mjazwe Roho" (Waefeso 5:18). Hili ni agizo la kuendelea kila siku.

Yesu ni mfano wetu katika hili. Roho ya Unabii inasema:

“Kila siku alipokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu. Katika saa za asubuhi mapema BWANA alimwamsha kutoka usingizini, na roho yake na midomo yake ikapakwa neema, ili apate kuwapatia wengine” (Christ’s Object Lessons, uk. 139).

Kama Kristo alihitaji ujazo wa kila siku wa Roho, basi Wakristo pia wanapaswa kuomba uzoefu huu kila siku.

Ukomavu wa kiroho ni mchakato wa kila siku:

“Lakini sisi sote, kwa uso usiofunikwa, tukitazama kama katika kioo utukufu wa BWANA, tunabadilika tufanane na mfano huohuo, kutoka utukufu hata utukufu, kama vile kwa Roho wa BWANA” (2 Wakorintho 3:18).

Roho ya Unabii inasema tena kuhusu mabadiliko haya:

“Roho wa MUNGU akimiliki moyo, hubadilisha maisha. Mawazo ya dhambi huondolewa, matendo maovu yanaachwa; upendo, unyenyekevu na amani huchukua nafasi ya hasira, wivu na ugomvi. Furaha huchukua nafasi ya huzuni, na uso huangaza nuru ya mbinguni” (The Desire of Ages, uk. 173).

Hii ndiyo baraka ya ajabu MUNGU aliyoandaa kwa kila mmoja wetu kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Taja faida nne za kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.
- Je, ubatizo wa Roho ni tukio la mara moja tu katika maisha ya Mkristo?
- Mkristo anapaswa kupokea mara ngapi ubatizo wa Roho Mtakatifu?
- Yesu mwenyewe alipokea mara ngapi ubatizo wa Roho Mtakatifu?
- Ubatizo wa Roho Mtakatifu hufanya nini kwa uhusiano wetu na Kristo?
- Kwa nini Shetani anaogopa tukipokea ujazo wa Roho?

Roho ya Unabii inasema nini kitakachotokea katika maisha yetu tukipokea ujazo wa Roho Mtakatifu?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- MUNGU aendelee kuwabatiza ninyi kwa Roho Wake Mtakatifu.

- Kristo alete mabadiliko yanayohitajika katika maisha yenu ili mweze kumwakilisha kikamilifu.
- Kwa ajili ya watu wote walio katika orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Tazama, jicho la BWANA li kwao wamchao, kwao wamngojeao fadhili zake; ili kuokoa nafsi zao na mauti, na kuwahisha wakati wa njaa. Nafsi zetu zimengojea BWANA; yeye ndiye msaada wetu na ngao yetu. Maana mioyo yetu itamfurahia, kwa kuwa tumelitumainia jina lake takatifu. Ee BWANA, fadhili zako na ziwe juu yetu, kwa kadiri tumekutumainia" (Zaburi 33:18-22).

*Geuza tumaini letu kwako, BWANA, na si kwenye mambo ya dunia. Tukomboe toka katika hali yetu ya ufu kiroho. Rejeza maisha yetu ya kiroho, toka kwenye hali yetu ya ukame kiroho. Uwe msaada na ngao yetu—tufanye kufurahi katika Wewe.*

## SIKU YA 4

## KRISTO NDANI YAKO

Muumini anapopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa kweli anampokea Kristo zaidi ndani ya maisha yake. Yesu alitabiri jambo hili alipowaahidi wanafunzi Wake Msaidizi mwingine ambaye Baba angepeleka akae nao na "kuwa ndani yao":

"Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi milele; ndiye Roho wa kweli, ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa sababu haumwoni wala haumjui; bali ninyi mnamjua, kwa maana anakaa nanyi, naye atakuwa ndani yenu" (Yohana 14:16-17).

Kisha Yesu akasema:

"Sitawaacha yatima; naja kwenu" (Yohana 14:18).

Kwa hiyo, kupitia Roho Mtakatifu, Yesu hukaa na pia ndani ya watu Wake. Ni kupitia ujazo wa Roho ambapo Yesu huishi kikamilifu ndani ya wanafunzi Wake.

"Naye ashikaye maagizo yake hukaa ndani yake, naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa Roho yule aliyetupa" (1 Yohana 3:24).

Yohana anatufundisha kwamba Wakristo watakaokuwa hai wakati Yesu atakapokuja watakuwa "kama Yeye":

"Wapenzi, sasa tu wana wa MUNGU, wala bado haijadhihirika yatakavyokuwa. Lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo" (1 Yohana 3:2).

Kwa jinsi gani tutafanana naye? Neno la Kiyunani lililotafsiriwa "kama" lina maana ya "sawasawa kabisa na Yeye." Hii itawezekana tu kupitia ubatizo wa kila siku wa Roho Mtakatifu, ambapo Yesu ataishi maisha Yake ndani yetu.

Paulo aliandika:

"Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo anaishi ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, naishi katika imani ya Mwana wa MUNGU, aliyenipenda akajitoa kwa ajili yangu" (Wagalatia 2:20).

Kwa njia hii, muumini aliyejazwa na Roho ataweza kuwa na akili ya Kristo (1 Wakorintho 2:16; Wafilipi 2:5), akipenda kile anachopenda Kristo — haki na

utakatifu, na kuchukia dhambi. Atakuwa na shauku ya kutii mapenzi ya Baba, na moyo wa kutafuta waliopotea (Luka 19:10).

Zaidi ya hayo, Roho huleta tunda la Roho ndani ya muumini:

"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, ustahimilivu, wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria" (Wagalatia 5:22-23).

Kwa hivyo, ubatizo wa Roho Mtakatifu humfanya muumini afanane zaidi na Kristo kila siku, hadi tabia ya Kristo ikidhihirishwa kikamilifu.

Yesu pia aliahidi kwamba waumini waliojazwa Roho watafanya kazi alizozifanya Yeye — kuhubiri, kufundisha, kuponya, na kufukuza pepo — hata "kubwa zaidi" (Yohana 14:12). Kwa njia hii, kila muumini anakuwa mikono, miguu, na kinywa cha Kristo duniani.

Paulo alisema:

"Kwa maana viumbe vyote vinatazamia kwa shauku kubwa kufunuliwa kwa wana wa MUNGU" (Warumi 8:19).

Na Yohana akaona wakati huo katika maono:

"Baada ya hayo nikamwona malaika mwingine akishuka kutoka mbinguni, mwenye uwezo mkuu; na nchi ikaangaza kwa utukufu wake" (Ufunuo 18:1).

Ndiyo maana Paulo alifundisha kwamba:

"Kristo yumo ndani yenu, tumaini la utukufu" (Wakolosai 1:27).

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Muumini anapopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, anamkaribisha nani zaidi ndani ya maisha yake?
- Ni faida zipi Mkristo hupata Yesu anapokaa ndani yake kwa njia ya Roho Mtakatifu?
- Viumbe vyote kwa shauku kubwa vinangojea nini?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza ninyi kwa Roho Wake Mtakatifu.

- Ili Kristo akae ndani yenu kikamilifu na adhihirishe tabia na kazi Zake kupitia kwenu.
- Kwa ajili ya watu wote walio katika orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Wenye haki walilia, na BWANA akasikia, akawaponya na dhiki zao zote" (Zaburi 34:17).

*Tusikie na tuokoe toka kwenye mambo yatuzuiayo kukua kikamilifu katika Kristo, mmoja mmoja na kama kutano.*

## SIKU YA 5

## UBATIZO WA ROHO NA UTII

Kuna makusudi mawili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Moja ni kumwakisi Yesu kikamilifu maishani mwetu:

“Mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tuliyoikatibu, iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa MUNGU aliye hai; si katika vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama.” (2 Wakorintho 3:3).

Lengo la MUNGU ni kwamba Kristo aonekane ndani yetu; ili tudhihirishe tabia ya Kristo. Kusudi la pili la ujazo wa Roho ni kupokea nguvu kwa ajili ya kushuhudia.

“Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.” (Matendo 1:8)

Katika tafakari ya leo tutajikita katika kusudi la kwanza—kuakisi tabia ya Yesu. Roho Mtakatifu alihusika zaidi pale MUNGU alipotoa Amri Kumi kwa Musa. Kwa kweli, alikuwa ni Roho aliyeandika zile Amri kwenye mbao za mawe. Jambo hili linakuwa wazi pale tunapolinganisha kauli za Yesu ambapo anafananisha “kidole cha MUNGU” na “Roho wa MUNGU.”

“Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa MUNGU, basi ufalme wa MUNGU umekwisha kuwajilia.” (Mathayo 12:28).

“Lakini, ikiwa mimi natoa pepo kwa kidole cha MUNGU, basi ufalme wa MUNGU umekwisha kuwajilia.” (Luka 11:20).

Hivyo, Roho Mtakatifu yule yule aliyeandika Amri Kumi kwenye mbao za mawe leo ataiandika sheria ya MUNGU kwenye moyo wa watoto waliojazwa na Roho wa MUNGU:

“Mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tuliyoikatibu, iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa MUNGU aliye hai; si katika vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama.” (2 Wakorintho 3:3).

Mkristo aweza kushiriki katika aina mbili za utii. Kwanza ni ule ninaouita utii wa nje. Utii huu hutokea pale muumini anapotii sheria ya MUNGU kwa sababu MUNGU asema kuitii. Aina hii ya utii kwa kweli ni ushupavu, hautoki moyoni. Aina ya pili ya utii ni wa ndani, na hutokea kutokana na msukumo wa ndani na

wa kina ndani ya muumini kumtii MUNGU. Utii wa nje usio moyoni haukubaliki kwa MUNGU:

“Maana hupendezwi na dhabihu, au ningeitoa, Wewe huridhii sadaka ya kuteketezwa. Dhabihu za MUNGU ni roho iliyovunjika; Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee MUNGU, hutaudharau.” (Zaburi 51:16, 17).

“Watu hawa huniheshimu kwa midomo; Ila mioyo yao iko mbali nami.” (Mathayo 15:8).

Nilikutana na kielelezo kimoja miaka mingi iliyopita kinachofafanua tofauti kati ya utii wa nje na wa ndani. Tuchukulie mfano, baba yangu alikufa, na sina hakika kama ninapaswa kuomboleza kifo chake, au la, basi ninakwenda kwa rafiki na kumwomba ushauri wake. Tunajadili kwamba niomboleze ama sivyo. Rafiki yangu mwishowe anasema, ‘Ingawaje alikuwa baba yako na ulikuwa mwanaye, basi nafikiri unapaswa kuomboleza kifo chake.’ Kutokana na ushauri wake ninaanza kuomboleza. Ninadhani inakuwa dhahiri kwamba kuomboleza kwangu katika hili si kutoka moyoni. Bali ni kuomboleza kwa nje kwa kuwa ilikuwa ni wajibu wangu kama mwana wa baba yangu, kuomboleza kifo chake. Kuomboleza halisi kungetokana na hiari toka moyoni. Nisingeliweza kujizuia kuomboleza ikiwa ilikuwa maombolezo ya kweli. Ndivyo ilivyo kuhusu utii kwa MUNGU. Mtu anapokuwa na uhusiano mzuri na MUNGU kupitia ujazo wa Roho, utii hububujika wenyewe kwa hiari toka moyoni pasipo hata kufikiria. Majaribu ya kutokutii yatakuja; hata hivyo, yatadhoofishwa na shauku kuu ambayo MUNGU ameiweka moyoni kutii.

Kwa njia ya ubatizo, au ujazo wa Roho Mtakatifu, sheria ya MUNGU huandikwa mioyoni mwetu. Hili halitokei kikamilifu pale tunapomkubali Kristo na kubatizwa kwa maji. Paulo anasema kwamba sharti tudumu ‘kujazwa na Roho,’ ambalo ni muhimu ili sheria ya MUNGU idumu kuandikwa moyoni mwetu: “” (Eph. 5:18).

Roho ya Unabii inaufafanua utii huu wa ndani, ububujikao toka katika uzoefu wa daima wa ubatizo wa Roho Mtakatifu, alipoandika “Utii wowote wa kweli huja toka moyoni. Ni moyo ulioguswa na Kristo. Na ikiwa tunakubaliana, Yeye atajitambulisha hivyo katika mawazo yetu na makusudi yetu, akichanganya mioyo na mawazo yetu katika hali ya kupatana na mapenzi yake, kiasi kwamba wakati wa kumtii tutakuwa tunatenda kulingana na misukumo yetu wenyewe maana inapatana na mapenzi yake. Nia, iliyosafishwa na kutakaswa, itakuta hitaji lake la juu ni kufanya kazi yake. Tunapomjua MUNGU kama tunavyojaliwa kumjua, maisha yetu yanakuwa maisha ya utii endelevu. Kupitia katika kuikubali tabia ya Kristo, kupitia ushirika pamoja na MUNGU, dhambi itakuwa kitu cha kuchukiwa kwetu.” (The Desire of Ages, p. 668).

## Tafakari na Majadiliano Binafsi

- Ni makusudi gani mawili ya kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu?
- Ni Mhusika yupi katika Uungu aliyeandika Amri Kumi kwenye mbao za mawe?
- Ni aina gani mbili za utii ambazo Wakristo wanaweza kuwa na uzoefu nazo?
- Ni aina ipi ya utii ambayo MUNGU huikubali?
- Ni kwa namna gani Roho ya Unabii inafafanua utii kutoka moyoni?

## Kujishughulisha Kuomba

Endelea na juhudi zako kuwasiliana na wote walio kwenye orodha yako ya maombi wiki hii ili kuwaambia unawaombea, na waulize kile wanachotaka uwaombee kwa niaba yao.

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU adumu kumbatiza kila mmoja wenu na Roho Wake Mtakatifu
- Ili MUNGU aandike sheria Yake moyoni mwenu.
- Kwa ajili ya wale mliowaorodhesha kuwaombea.

## Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako

"Ee MUNGU, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu Usinitenge na uso wako, Wala roho yako mtakatifu usiniondolee. Unirudishie furaha ya wokovu wako; Unitegemeze kwa roho ya wepesi." (Zaburi 51:10-12).

*BWANA, niondolee moyo utendao dhambi na roho yenye majivuno. Kwa rehema zako nilete karibu nawe, na rejeza ukamilifu wa Roho Wako kwangu. Niongoze kufurahia furaha kamili ya wokovu Wako, na nipatie nguvu Zako.*

## SIKU YA 6

## KUMHUZUNISHA ROHO

Kuna mambo ambayo twaweza kufanya ambayo yatamhuzunisha Roho:

"Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa MUNGU; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi." (Waefeso 4:30).

Tusipomtafuta Yeye kila siku na kushirikiana katika kumfuata anapotuongoza, uweza Wake utapungua na uzoefu wetu wa Kikristo utadhoofika. MUNGU halazimishi. Tunapopokea ubatizo wa Roho, Yeye atafanya makubwa kwenye maisha yetu. Tutahisi msukumo Wake kwa nguvu zaidi. Kila siku atakuwa akiweka tamanio moyoni mwetu kumtii MUNGU. Atatuita tujifunze Neno la MUNGU na kuomba zaidi. Roho atatuongoza kuanza kupenda kuhesabiwa haki na kuchukia dhambi. Hata hivyo, daima tu huru kupuuza msukumo Wake. Tunapofanya hivi twaanza "kumhuzunisha," au "kumzimisha," Roho. Paulo anatoa ushauri unaofaa katika sehemu nyingi za Maandiko jinsi ya kuepuka kutenda hivi. Mashauri haya yafaayo kwa muumini katika kuishi maisha ya Ukristo yamekusudiwa kutusaidia kudumisha ukamilifu wa Roho maishani mwetu. Mifano miwili ya ushauri kama huo yapatikana katika mafungu ya Biblia yafuatayo:

"Mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya MUNGU katika haki na utakatifu wa kweli. Basi uvueni uongo, mkaseme kweli kila mtu na jirani yake; kwa maana tu viungo, kila mmoja kiungo cha wenzake. Mwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka; wala msimpe Ibilisi nafasi. Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji. Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia. Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa MUNGU; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi. Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na MUNGU katika Kristo alivyowasamehe ninyi." Waefeso 4:24-32

"Ndugu, twawasihi, waonyeni wale wasiokaa kwa utaratibu; watieni moyo walio dhaifu; watieni nguvu wanyonge; vumilieni na watu wote. Angalieni mtu awaye yote asimlipe mwenziwe mabaya kwa mabaya; bali siku zote lifuateni lililo

jema, ninyi kwa ninyi na kwa watu wote. Furahini siku zote; ombeni bila kukoma; shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya MUNGU kwenu katika Kristo Yesu. Msimzimishe Roho" 1 Wathesalonike 5:14-19

Paulo alitambua kuwa Roho wa MUNGU akiishi ndani ya muumini atasukumwa kutenda mambo yaliyoorodheshwa katika mafungu haya. Tukikataa kukubali maongozi Yake, hata hivyo, tutakuwa kwenye hatari ya kumhuzunisha na kumzimisha Roho.

Ukiona kwamba unamhuzunisha Roho, usivunjike moyo! Mwombe MUNGU akusamehe, Naye atafanya hivyo:

"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." (1 Yohana 1:9).

"Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?" (Luka 11:13).

Daudi alijua rehema za MUNGU. Alikuwa ametenda dhambi za uzinzi na uuaji. Alikuwa ametanga mbali na msukumo wa Roho wa MUNGU katika maisha yake alipotenda vitendo hivi vya kutisha. Hata hivyo aliposadikishwa na Roho kwamba ametenda dhambi, alimgeukia MUNGU kwa sala. Zingatia hasa maneno haya:

"Usitiri uso wako usitazame dhambi zangu; Uzifute hatia zangu zote. Ee MUNGU, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu Usinitenge na uso wako, Wala roho yako mtakatifu usiniondolee. Unirudishie furaha ya wokovu wako; Unitegemeze kwa roho ya wepesi." (Zaburi 51:9-12).

Tunapogundua kwamba tumekuwa tukitanga mbali na MUNGU sharti tusiruhusu nafasi nyingine ipite bila kuungama dhambi yetu, na kukubali msamaha wa MUNGU, na kudai ahadi za kuhuishwa na Roho maishani mwetu kama tu alivyofanya Daudi. Ndipo tutaimarishwa kwa mara nyingine tena katika utu wa ndani kumshinda shetani:

"Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani. Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa MUNGU." Waefeso 3:16-19

Twamtumikia MUNGU wa ajabu. Tunapomkosea, tukumbuke:

"BWANA amejaa huruma na neema, Haoni hasira upesi, ni mwingi wa fadhili. Yeye hatateta sikuzote, Wala hatashika hasira yake milele. Hakututenda sawasawa na hatia zetu, Wala hakutulipa kwa kadiri ya maovu yetu. Maana mbingu zilivyoinuka juu ya nchi, Kadiri ile ile rehema zake ni kuu kwa wamchao. Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi. Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake, Ndivyo BWANA anavyowahurumia wamchao. Kwa maana Yeye anatujua umbo letu, Na kukumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi." (Zaburi 103:8-14

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Orodhesha baadhi ya mienendo na mielekeo ambayo Roho Mtakatifu atafanya kukurejesha katika maisha ya Ukristo.
- Ni kwa namna gani Mkristo humhuzunisha Roho Mtakatifu?
- Tunapomhuzunisha Roho Mtakatifu, tufanye nini?
- Ni upi mwelekeo wa MUNGU juu ya watoto Wake?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU adumu kuwabatiza kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU awasamehe ikiwa mmemhuzunisha Roho Mtakatifu kwa namna yo yote?
- Ili MUNGU awape shauku ya kukubali maongozi ya Roho katika maisha yako.
- Omba kwa ajili ya wote walio kwenye orodha yako.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Kwa maana macho ya BWANA hukimbia-kimbia duniani mwote, ili ajionyeshe mwenye nguvu kwa ajili ya hao, waliokamilika moyo kuelekea kwake. Kwa hayo umetenda upumbavu; kwani tangu sasa utakuwa na vita." (2 Mambo ya Nyakati 16:9).

*Fanya mioyo yetu ijitoe kikamilifu Kwako. Jionyeshe Mwenye nguvu kwa niaba yetu ili kuleta mabadiliko yanayoitajika ndani yetu ili hatimaye tuishi uamsho na matengenezo tunayohitaji.*

## SIKU YA 7

## ROHO NA MVUA YA MASIKA

Ni muhimu mno kwamba kila siku tupate ubatizo wa mvua ya vuli/awali wa Roho Mtakatifu ili tuweze kukua kiroho hadi kufikia kiwango ambacho tutafaidika toka katika mvua ya masika ya Roho, inayomwandaa mkristo kwa ajili ya pambano la mwisho na marejeo ya Kristo. Hata hivyo, wengi hawalitambui hili na wanadhani kwamba lazima wasubiri mvua ya masika ya Roho ili hatimaye wawe washindi juu ya dhambi zinazowazonga na kutokua kiroho. Mtazamo kama huo utaishia katika maafa kwa yule anayeushikilia. Roho ya Unabii inaonya:

"Niliona kwamba wengi walikuwa wakipuuza maandalizi ambayo yanahitajika sana, na walikuwa wakitazamia wakati wa 'kuburudishwa' na 'mvua ya masika' ili kwamba wafae kusimama katika siku ya BWANA, na kuishi chini ya uangalizi Wake. Lo, ni wangapi niliwaona katika wakati wa taabu wakiwa hawana pa kukimbilia! Walikuwa wamepuuza maandalizi yanayohitajika, hivyo hawakuweza kupokea kuburudhishwa ambako wote sharti wafae kuishi mbele za MUNGU Mtakatifu"

Ni lazima tuwe washindi juu ya majaribu yote na dhambi maishani mwetu ikiwa tunataka kufaidika na mvua ya masika ya umwagwaji wa Roho. Ni udanganyifu wa Shetani ikiwa tutaamini kwamba hatupaswi kuchukua hatua juu ya tatizo la dhambi maishani mwetu:

"Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake BWANA" (Matendo 3:19).

"Mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena…Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa MUNGU katika Kristo Yesu. Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake; wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa MUNGU kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa MUNGU kuwa silaha za haki. Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema." (Warumi 6:6, 11-14).

Roho ya Unabii inathibitisha hili inaposema maneno haya:

"Niliona kwamba hakuna awezaye kugawana na mwingine 'uburudisho' [mvua ya masika], mpaka pale watakapopata ushindi juu ya kila tatizo, juu ya

majivuno, ubinafsi, kuupenda ulimwengu, na juu ya kila neno na tendo baya" (Ibid. uk. 113).

Hili laweza kuonekana kama haliwezekani kwako kwa sasa hivi. Hata hivyo, njia ya kuelekea kwenye ushindi juu ya majaribu ni katika kujifunza jinsi ya kumruhusu Yesu aishi ndani yetu na kupitia sisi maisha ya ushindi wa dhambi. Kweli hiyo ya kushangaza ya kibiblia itafafanuliwa katika kurasa za mbele za kesha hili.

Mvua ya vuli, au ya awali ya Roho, ambayo ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, ilianza pale katika siku ya Pentekoste. Petro alilisema hili pale aliposema kwa mkutano siku hiyo:

"Lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli, Itakuwa siku za mwisho, asema MUNGU, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto. Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake Roho yangu, nao watatabiri." (Matendo 2:16-18).

Ubatizo wa Roho, au mvua ya awali ya Roho, hutuleta kwenye ukomavu wa kiroho unaohitajika ili tuweze kufaidika na mvua ya masika:

"Mvua ya masika, kuiva kwa mavuno ya nchi, huwakilisha neema za kiroho zinazoliandaa kanisa kwa ajili ya marejeo ya Mwana wa Adamu. Lakini mvua ya awali isiponyesha, hakutakuwa na uhai; jani lenye kijani kibichi halitachipuka. Matone ya awali yasipofanya kazi yake, mvua ya masika haiwezi kukomaza mbegu." (The Faith I Live By, p. 333).

Ukuaji kamili wa kiroho chini ya mvua ya vuli ya ubatizo wa Roho ni muhimu kwetu kuweza hata kutambua mvua ya masika ya Roho pale inaponyesha. Roho ya Unabii inasema:

"Pasipo kuzidi daima katika kuonyesha kielelezo cha uwezo tendaji wa Ukristo, hatutaweza kutambua udhihirisho wa Roho Mtakatifu katika mvua ya masika. Inaweza kuwa inanyesha mioyoni karibu nasi, lakini hatutaitambua au kuipokea" (Testimony to Ministers and Gospel Workers, p. 507).

Ikiwa haujapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu usikawie siku nyingine. Kumpokea Kwake inapaswa kuwe mara moja na kwa kipaumbele maishani mwetu, kwani Kipawa hiki kitaleta vipawa vingine vyote kwetu. Kujazwa kwa roho kutamfanya Kristo aishi ndani yetu na kubadili udhaifu wetu kutoka ulegevu hadi uchangamfu, kutoka udhaifu hadi kuwa na nguvu, na ushuhuda wetu utakuwa na nguvu ambayo haijawahi kuonekana tangu siku ya Pentekoste:

"Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa MUNGU, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." (Wagalatia 2:20).

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." (Matendo 1:8).

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Umwagwaji wa namna mbili wa Roho Mtakatifu unaitwaje katika Biblia?
- Ni lini mvua ya vuli/awali ya Roho ilianza?
- Inahitajika kiasi gani kwa Mkristo kupokea ubatizo wa Roho ili kufaidika toka kwenye mvua ya masika?
- Ni mabadiliko gani sharti yatokee katika maisha ya Mkristo chini ya mvua ya awali/vuli ya Roho Mtakatifu ili kuwa tayari kwa ajili ya mvua ya masika ya Roho?
- Je ni busara kusubiri kwa ajili ya mvua ya masika kabla ya kulichukulia hatua tatizo la dhambi maishani mwetu?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwenza wako wa maombi na jadili kesha hili naye. Omba na mwenza wako wa maombi:

- Ili MUNGU adumu kuwabatiza kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU awatayarishe kupokea mvua ya masika ya Roho.
- Kwa ajili ya wale wote uliowaorodhesha kuwaombea.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Malaika wa BWANA hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa." (Zaburi 34:7).

*Tuokoe kwenye hali yetu ya ulegevu wa kiroho na tulinde dhidi ya mashambulizi ya Shetani.*

## SIKU YA 8

## UBATIZO WA ROHO NA MAREJEO YA KRISTO

Habari njema siku ya leo ni kwamba Yesu anakuja upesi! Sisemi hili kwa sababu tu ya mashambulizi ya kigaidi, migogoro ya ulimwengu, maafa ya mlipuko, au majanga ya asili—yote haya kwa hakika yanaashiria marejeo ya Kristo yapo karibu mno. Hata hivyo, kuna kingine zaidi kinachonisadikisha zaidi kwamba ujio wa Kristo u karibu mno. Ni utendaji Wake miongoni mwetu kuelewa na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Mafungu ya mwisho ya Ufunuo 6 yanafafanua ujio wa Yesu na yanauliza swali Nani ataweza kusimama? Kumaanisha, nani ataweza kustahimili tukio hili? Jibu linapatikana katika Ufunuo 7:1-3

Ni wale tu wenye muhuri wa MUNGU watakaoweza kustahimili marejeo ya pili ya Kristo. Kwa kweli, MUNGU anashikilia na kuzuia nguvu nyingi zenye kuharibu duniani mpaka watu wa MUNGU wametiwa muhuri. Swali muhimu, ni jinsi gani tunatiwa muhuri? Biblia yasema twatiwa muhuri na Roho Mtakatifu:

"Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa MUNGU; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi." (Waefeso 4:30).

Hivyo ndivyo ubatizo wa Roho Mtakatifu ulivyo. Ni kwa kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu kila siku ndipo twatiwa muhuri na kujitayarisha kwa ujio wa pili wa Kristo.

MUNGU hasubiri mashambulizi zaidi ya kigaidi, milipuko ya magonjwa, au majanga ya asili. Roho ya Unabii inasema kile ambacho Kristo amekisubiri:

"Hakuna kingine isipokuwa ubatizo wa Roho Mtakatifu unaoweza kulileta kanisa mahali pake sahihi, na kuwaandaa watu wa MUNGU kwa pambano linalokaribia haraka" (Manuscript Releases p. 30).

Kama Waadventista Wasabato tuna hatari. Twafikiri tuko salama na tutakuwa tayari kwa ajili ya marejeo ya Kristo kwa sababu twaijua Sabato, fundisho la hali ya wafu, alama ya mnyama, na namna ya marejeo ya Kristo mara ya pili. Hili ni kosa la kufisha. Mafundisho haya ni ya muhimu; hata hivyo, maarifa haya peke yake hayatatuokoa. Kumbuka, walikuwa ni watoa zaka, watunza Sabato, wanamatengenezo ya afya waliomsulubisha Yesu. Hapana; si kile tunachokijua bali ni nani tunayemjua ndivyo kutatuwezesha sisi kuokolewa (Yohana 17:3). Sharti tuwe na uhusiano wa karibu mno na Yesu Kristo ikiwa tunataka kujitayarisha kwa marejeo Yake.

Leo MUNGU anaita watu kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu katika kujitayarisha kuwa kama Yesu, ili kupokea mvua ya masika ya Roho, na kuwa tayari kwa marejeo ya Kristo:

"Wapenzi, sasa tu wana wa MUNGU, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo." (1 Yohana 3:2).

Walakini leo kanisa lina tatizo. MUNGU atwambia kwamba tu katika hali ya Laodikia na, kama hatutabadilika, hatutakuwa tayari kwa marejeo ya Kristo. MUNGU pia anatupatia suluhisho: kumruhusu Yesu aingie maishani mwetu kikamilifu zaidi:

"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami." (Ufunuo 3:20).

Ni kwa namna gani twamruhusu Yesu kuingia mioyoni mwetu na kuwa na uhusiano wa karibu mno na Yeye ili tuwe naye? Roho ya Unabii inasema:

"Sharti tuwe na uhusiano hai na MUNGU. Ni lazima tuvikwe na nguvu na uweza utokao juu kwa kubatizwa na Roho Mtakatifu ndipo tunaweza kufikia viwango vya juu; kwani hakuna msaada kwa ajili yetu kwa njia nyingine yo yote" (Review and Herald, April 5, 1892).

### Tafakari na Majadiliano Binafsi

- Kwa nini malaika wanazuia pepo za uharibifu katika dunia hii?
- Je, kujua mafundisho ya Biblia ndivyo tu tunavyopaswa ili kuokolewa? Kwa nini, au kwa nini sivyo?
- Kulingana na Biblia, twatiwa muhuri kwa namna gani?
- Ubatizo wa Roho Mtakatifu una kazi gani juu ya uhusiano wetu na Kristo?
- Ni kipi pekee kitakachotutayarisha kwa ajili ya pambano la mwisho?

### Kujishughulisha Kuomba

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU adumu kuwabatiza kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU awatayarishe kwa ajili ya pambano la mwisho la dunia na marejeo ya Kristo.
- Kwa ajili ya wale wote uliowaorodhesha kuwaombea.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"BWANA yu karibu nao waliovunjika moyo, Na waliopondeka roho huwaokoa." (Zaburi 34:18).

*Vunjavunja mioyo yetu yenye kiburi na weka roho iliyopondeka ndani yetu. Tuokoe na njia za dhambi na tuponye kurudi kwetu nyuma kiroho.*

# SEHEMU YA II—UBATIZO WA ROHO NA MAOMBI

## SIKU YA 9

## MSUKUMO WA SALA UNAOTOLEWA NA ROHO

Tunapopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, msukumo na shauku yenye kina itaanza kuinuka ndani yetu ili kuwa mtu was ala kwa Baba yetu wa mbinguni:

“Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba; nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee; nao wataona uchungu kwa ajili yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza.” (Zekaria 12:10)

Twaweza kujielekeza kwenye msukumo na shauku hii itolewayo na MUNGU, au kupuuza na kuendelea kuwa mkristo mwenye itikadi kali kuliko kuwa mkristo wa sala. Walakini, ikiwa tunataka kuwa na uzoefu wa kina wa mambo ya MUNGU na ukamilifu wa Kristo maishani mwetu, sharti tujielekeze kwenye msukumo huu kuwa na maombi. Ikiwa tunataka kuona uweza Wake uokoao ukijidhihirisha katika maisha yetu juu ya kila ambacho Shetani hujaribu kuleta juu yetu na kuona uweza wa MUNGU ukijidhihirisha kupitia sisi katika kuwabariki wengine na ukombozi Wake, sharti tutumie muda mwingi na MUNGU katika sala.

Kwa miaka sasa Wakristo wametambua umuhimu wa maombi. Mara nyingi tumekuwa na juhudi kupata muda katika maombi, lakini nyakati zile mahususi za maombi zilitiwa nguvu na migogoro fulani na hazikuendelea zaidi. Tatizo letu ni kwamba tumekuwa watu wenye kujiona tumetosheka katika kukutana na mahitaji yetu wenyewe na mahitaji ya kanisa. Tumejifunza kutegemea juhudi zetu wenyewe kufanya kazi ya MUNGU. Tumehusika katika mipango mingi na program nyingi. Tumejifunza kutegemea juhudi za mwilini kufanya kazi ya MUNGU. Kwa huruma, amebariki juhudi zetu dhaifu. Hata hivyo, Baraka zipitazo matarajio yetu makuu zatusubiri pale tunapopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu na kuingia katika uhusiano wa sala anaotamani kwetu. Ni kwa njia hiyo ndipo mipango yetu itakuwa mipango ya MUNGU, na kushughulika kwetu kunakuwa ni kushughulika kwa MUNGU.

Yesu alikuwa na uhusiano wa namna hii ufaayo, wa kina, na wenue nguvu na Baba Yake. Kwa kweli, uhusiano ulikuwa wa karibu mno kiasi kwamba Yesu alisema:

“Mimi na Baba tu umoja.” (Yohana 10:30)

Kila alichofanya Yesu kilikuwa chini ya mwongozo wa Baba Yake. Maneno Yake, kutenda Kwake vilifanyika chini ya mwongozo na uweza wa Baba. Yesu alisisitiza hili pale aliposema:

"Husadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu? Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake." (Yohana 14:10)

Ni kwa jinsi gani Yesu alipata umoja wa karibu kiasi hicho na Baba Yake? Ilikuwa kwa sababu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu na kwa njia ya Sala. Yesu alipobatizwa kwa maji, aliomba:

"Ikawa, watu wote walipokwisha kubatizwa, na Yesu naye amebatizwa, naye anaomba, mbingu zilifunuka; Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili, kama hua; sauti ikatoka mbinguni, Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe." (Luka 3:21, 22)

Katika kujibu sala ya Kristo Roho Mtakatifu alimjia na kushuka juu Yake na akapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Muda mchache baada tu ya tukio hili, aliongozwa na Roho kutumia siku 40 usiku na mchana, akifunga na kuomba nyikani:

"Na Yesu, hali amejaa Roho Mtakatifu, alirudi kutoka Yordani, akaongozwa na Roho muda wa siku arobaini nyikani, akijaribiwa na Ibilisi. Na siku hizo alikuwa hali kitu; hata zilipotimia, aliona njaa." (Luka 4:1, 2).

Kutoka katika muungano huu mahususi na Baba Yake, Kristo alitoka nyikani akiwa amejitayarisha kuifanya kazi aliyokujia duniani kuifanya. Aliwezeshwa kuwa mshindi juu ya Shetani na kumshinda:

"Yesu akarudi kwa nguvu za Roho, akenda Galilaya; habari zake zikaenea katika nchi zote za kandokando." (Fungu la 14).

Siku 40 za maombi ambazo umezichagua kushiriki zimekusudiwa kufanya vivyo hivyo kwa ajili yako. Wakati wa siku hizi 40 utapitia uzoefu wa kuwezeshwa kuwa mshindi juu ya Shetani ma kuwa mfereji kwa ajili ya Kristo kuwatumikia wengine kupitia wewe.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Ni kwa jinsi gani Roho Mtakatifu ataathiri maisha yetu ya sala?
- Kwa ujumla, ni kipi ambacho Wakristo wana kawaida ya kukitegemea kuliko sala?
- Ni maisha gani ya sala ambayo Yesu alikuwa nayo?

- Kwa sababu ya uzoefu na maisha ya Yesu kwa kubatizwa na Roho, ni kwa namna gani Yesu aliweza kufafanua uhusiano Wake na Baba Yake?
- Maisha ya sala na uzoefu wa Yesu kwa kubatizwa na Roho kulimwezeshaje Yeye kufanya?
- Unadhani ni maisha gani ya sala ambayo Yesu anakutaka uwe nayo?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU adumu kuwabatiza kila mmoja kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU awapatie msukumo mkuu wa kuomba.
- Kwa ajili ya wale wote uliowaorodhesha kuwaombea.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao." (2 Mambo ya Nyakati 7:14).

*Tuongoze katika kujidhili. Tuwekee msukumo mioyoni mwetu wa kuwa watu was ala na tugeuze toka katika njia za uovu. Usikie sala zetu, utusamehe, na utuponye na kurudi kwetu nyuma kiroho.*

## SIKU YA 10

## KIELELEZO CHA SALA CHA YESU NA WANAFUNZI

Kila mara, twamwona Kristo katika maombi wakati wa huduma Yake akiwa duniani. Baada ya juwafundisha makutano makubwa na kuwaponya magonjwa yao, tunaambiwa:

“Lakini yeye alikuwa akijiepua, akaenda mahali pasipokuwa na watu, akaomba.” (Luka 5:16)

Luka anaripoti kwamba kabla ya kuitwa kwa wanafunzi 12:

“Ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba MUNGU. Hata kulipokuwa mchana aliwaita wanafunzi wake; akachagua kumi na wawili miongoni mwao, ambao aliwaita Mitume” (Luka 6:12, 13)

Katika mlima pale ambapo Yesu alibadilika sura, Yesu aliomba (Luka 9:29). Aliongozwa na Roho kuwa pamoja zaidi na Baba Yake wa mbinguni katika sala. Akaitikia kusonga mbele kwa hitaji alilohisi lenye kina na la ndani kwa ajili ya sala. Alijua kwamba ilikuwa ni kupitia nyakati hizo za sala peke yake kwamba angeweza kuwa pamoja na Baba na kuwezeshwa kuitenda kazi aliyokujia kuitenda.

Yesu alijipatia ushindi Wake dhidi ya kazi za Shetani kupitia nyakati za kuwa na maombi pamoja na Baba. Tunaposoma juu ya Yesu kukabiliana na Shetani katika maisha ya wanaume na wanawake na katika ulimwengu wa asili katika sura za watu waliokuwa wamepagawa na mapepo, wagonjwa, vifo, dhoruba, n.k, hatumwoni Kristo katika saa hiyo akiwa kwenye maombi ya kina pamoja na Baba Yake, akiomba kwa ajili ya nguvu za kuokoa. Tayari alikuwa amekwisha pokea nguvu hiyo toka kwa Baba katika nyakati za sala. Akiwa anakabiliana na Shetani na kazi zake, Yesu alinena Neno tu katika uweza na mamlaka ya Baba, na nguvu za Shetani zilivunjwa. Neno la Kristo lilitoa mapepo, liliponya wagonjwa, lilifufua wafu, na lilituliza dhoruba.

Somo la kujifunza li wazi. Kristo alidumisha muungano Wake na Baba na akapokea uweza Wake dhidi ya adui wakati wa majira Yake ya sala pamoja na Baba Yake. Kisha alitoka kwenye majira ya sala akiwa pamoja na Baba Yake. Alitambua uwepo wa Baba nyakati hadi nyakati na siku hadi siku. Kristo alidumisha utambuzi huu na muungano halisi pamoja na Baba Yake katika maisha Yake yote. Kila mara alipokabiliana na Shetani, alikuwa amekwishajitayarisha

kukutana na changamoto na kujipatia ushibdi kwa sababu ya maisha Yake ya sala.

Kielelezo cha maisha ya Kristo ya sala hayakupotea kwa wanafunzi. Maombi ilikuwa sehemu kuu na muhimu ya huduma yao. Ukuaji wa Kanisa ulipoanza kuhitaji zaidi muda wa wanafunzi, kuliasisiwa mashemasi "kuhudumu mezani." Wanafunzi walisema juu ya vipaumbele vyao:

"Na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno." (Matendo 6:4).

Waumini wa Kanisa la awali walikuwa wanaume na wanawake wa maombi. Imeandikwa kuwa kumbukumbu juu yao:

"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali." (Matendo 2:42).

Waumini hawa wa awali walifanya sala hekaluni, majumbani kwao, na nje kwenye mazingira ya asili.

"Hata siku ya sabato tukatoka nje ya lango, tukaenda kando ya mto, ambapo tukadhani ya kuwa pana mahali pa kusali; tukaketi, tukasema na wanawake waliokutana pale." (Matendo 16:13)

Mitume wote walikuwa wanaume wa sala. Paulo alisema aliomba mchana na usiku kwa ajili ya waumini:

"Usiku na mchana tunapoomba kwa juhudi tupate kuwaona nyuso zenu, na kuyatengeneza mapungufu ya imani yenu?" (1 Wathesalonike 3:10)

Kwa sababu mitume walikuwa wanaume wa maombi, walikuwa wanaume wa uweza katika BWANA. Wakristo wa awali vilevile walikuwa wanaume na wanawake wa sala, na MUNGU aliweza kutenda maajabu makuu na miujiza kupitia wao. Kwa sababu ya maombi injili ilienea ulimwenguni.

"Mkidumu tu katika ile imani, hali mmewekwa juu ya msingi, mkawa imara; msipogeuzwa na kuliacha tumaini la Injili mliyosikia habari zake, iliyohubiriwa katika viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu; ambayo mimi Paulo nalikuwa mhudumu wake." (Wakolosai 1:23)

MUNGU anamwita kila Mkristo kuwa shujaa wa maombi mwenye uwezo mkuu.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Kwa nini Yesu alitumia muda mwingi zaidi katika maombi?
- Ni kwa namna gani kielelezo cha Yesu katika sala kiliwaathiri wanafunzi?

- Ni maisha ya sala ya namna gani ambayo waumini wa kanisa la awali walikuwa nayo?
- Ni kwa jinsi gani unataka maisha yako ya maombi yabadilike?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU adumu kuwabatiza kila mmoja kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU akuongoze kuwa shujaa wa maombi kama alivyokuwa Yesu na wanafunzi.
- Kwa ajili ya wale wote uliowaorodhesha kuwaombea.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

“Unifahamishe njia ya mausia yako, Nami nitayatafakari maajabu yako.” (Zaburi 119:27).

*Fungua ufahamu wngu kwa ajili ya mafundisho Yako. Nifanye nikutafakari daima.*

# SIKU YA 11

## KWA NINI MAOMBI NI MUHIMU?

Ingawa Wakristo wengi wanaamini kuwa maombi ni muhimu, wengi hawaelewi kwa nini maombi ni muhimu hasa. Wengi huhoji ikiwa MUNGU ni Mtawala na anaweza kutekeleza mapenzi Yake, kwa nini tena tuhitaji kumwomba ili afanye kile ambacho tayari anakihitaji na anapanga kukitenda? Wengine huuliza kwamba maombi ni msingi kwa faida yetu, lakini MUNGU bado anatenda kile akitakacho Yeye hata tukimwomba ama tusimwombe. Wazo limeenea kwamba kuomba ni 'upendeleo' lakini kwa kweli ni muhimu sana kuomba ili MUNGU atende mapenzi Yake hapa duniani. Ukweli wa jambo ni kwamba ni muhimu kwa watoto wa MUNGU kuomba. Kwa nini tena Yesu atuambie kusali ili mapenzi ya MUNGU yatimizwe?

"Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni." (Mathayo 6:9, 10)

Ikiwa waumini hawaombi, mapenzi ya MUNGU hayatatimizwa hapa duniani.

Kitabu cha Mwanzo kinahifadhi kumbukumbu ya Uumbaji wa ulimwengu huu na jamii ya mwanadamu:

"MUNGU akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. 27 MUNGU akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa MUNGU alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba." (Mwanzo 1:26, 27)

Maneno ya Kiebrani yaliyotafsiriwa 'mfano,' 'sura,' huonyesha kwamba MUNGU aliumba wanadamu katika namna nyingi kama Yeye Mwenyewe.

MUNGU alifanya kitu fulani zaidi pale alipomwumba mtu. Tunaambiwa katika fungu hapo juu kwamba MUNGU alimpatia mwanadamu 'utawala; juu ya ulimwengu huu. Neno la Kiebrania lililotafsiriwa 'kutawala' humaanisha, 'kuongoza, 'kutawala kifalme' juu ya. Kama mwakilishi wa MUNGU, Adamu alipaswa kuwa mtawala wa ulimwengu huu:

"BWANA MUNGU akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza." (Mwanzo 2:15).

Wajibu wa Adamu 'kuitunza' dunia ilimaanisha alipaswa kuilinda dhidi ya cho chote ambacho kingeweza kuidhuru. Adamu alipaswa kuwa mwakilishi mwenye mamlaka wa MUNGU katika dunia hii. Alipaswa kuwa mwangalizi na mlinzi wa dunia.

Mtunga Zaburi anafafanua zaidi nafasi ambayo MUNGU alimpatia mwanadamu katika Uumbaji

"Umemfanya mdogo punde kuliko MUNGU; Umemvika taji ya utukufu na heshima" (Zaburi 8:5).

Tukiangalia tena katika maneno asili ya Kiebrania yaliyotafsiriwa 'utukufu,' na 'heshima,' tunapata kuona kwamba mwanadamu alipewa mamlaka sawasawa na yale ya mfalme atawalaye. Hivyo, twaona kwamba katika Uumbaji dunia iliwekwa kuwa chini ya mamlaka ya Adamu. Kile kilichopaswa kutokea duniani kilitegemea Adamu.

Maombi ni muhimu, kwa sababu tangu mwanzo MUNGU alikusudia kutenda kupitia wanadamu, si kwamba Yeye tu peke Yake, katika kutekeleza mapenzi Yake duniani. MUNGU hutenda kupitia maombi ya watu Wake. MUNGU anaponuia kutenda kitu fulani duniani, ni muhimu kwa jamii ya wanadamu kuomba kwamba Mingu atende hivyo. Mifano mingi ya hili inapatikana katika Agano la Kale na Jipya. Hatuna budi kuomba ili 'Mapenzi ya MUNGU yatimizwe duniani' (Mathayo 6:10). Hatuna budi kumwomba MUNGU a-'tupe mkate wetu wa kila siku' (Fungu la 11).

Yesu alipoona hitaji kuu la makutano, aliwaomba wanafunzi Wake kufanya lifuatalo kwa Baba:

"Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji. Ndipo alipowaambia wanafunzi wake, Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni BWANA wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake." (Mathayo 9:36-38)

MUNGU anataka kutuma watendakazi kwenye mashamba yanayohitaji mavuno ya dunia hii. Hata hivyo, ni muhimu kwa Mkristo kumwomba Yeye ili atende hili.

Paulo aliwaomba waumini kuomba kwa ajili ya kusonga mbele kwa injili:

"Hatimaye, ndugu, tuombeeni, neno la BWANA liendelee, na kutukuzwa vile vile kama ilivyo kwenu" (2 Wathesalonike 3:1)

Mambo yote yaliyoorodheshwa hapo juu ni mapenzi ya MUNGU; lakini ni muhimu kwa mwanadamu kuomba kwa ajili ya hayo kwa sababu maombi hukaribisha uweza wa MUNGU kutekeleza mapenzi Yake duniani. Kumbuka, ni mpango wa MUNGU kutenda kazi 'kupitia' jamii ya mwanadamu, si kutenda Yeye peke Yake. Maombi yako ni muhimu ili mapenzi ya MUNGU kutimizwa maishani mwako na katika maisha ya wengine unaowaombea.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Kwa kuwa MUNGU ni MUNGU, na ana uweza kutenda lo lote atakalo, je, hatatekeleza mapenzi Yake hata kama tukiomba ama tusipoomba? Kwa nini ndivyo, au kwa nini sivyo?
- Ni wajibu gani Adamu alikuwa nao pale mapenzi ya MUNGU yalipotimizwa duniani?
- MUNGU anapotaka kutenda kitu fulani duniani, ni kipi cha muhimu kwa Mkristo kufanya?
- Je, maombi ni muhimu, au ni upendeleo tu? (Kwamba nipende au nisipende)
- Unadhani kwa jinsi gani Shetani hujisikia kuhusiana na muda wako wa kuomba na MUNGU?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU adumu kuwabatiza kila mmoja kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU akupatie uelewa Dhahiri wa umuhimu wa kuomba.
- Kwa ajili ya wale wote uliowaorodhesha kuwaombea.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Uniondolee njia ya uongo, Unineemeshe kwa sheria yako." (Zaburi 119:29).

*Nigeuze toka katika njia za dhambi. Nipe neema ili Jina Lako litukuzwe.*

## SIKU YA 12

## KUOMBA KATIKA ROHO

Kila Mkristo anahusika katika vita dhidi ya adui na matokeo ya umilele hatarini. Pambano hili ni halisi kama mapambano mengine yo yote yaliyowahi kupiganwa duniani kati ya mataifa. Pambano ni kati ya ufalme wa MUNGU na ufalme wa giza. Paulo anafafanua pambano hili kama kabiliano la kimweleka, ambalo li karibu na ni la mtu binafsi:

“Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.” (Waefeso 6:12)

Baada ya hapo Paulo anafafanua silaha ya MUNGU kwamba Mkristo sharti avae kwa ajili ya ushindi. Paulo anahitimisha maelezo yake juu ya vita hii na ulinzi wetu dhidi ya adui kwa maneno haya:

“Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote” (Fungu la 18)

Zingatia kwamba Paulo anatuamuru kuomba ‘daima.’ Ni lazima tuwe wapatanishi tunaokesha katika sala, tukiomba kwa ujasiri na ustahimilivu. Kisha anaongeza, “katika Roho.” Hapa twaona kwamba ikiwa tunataka ushindi dhidi ya adui, kuomba katika Roho ni muhimu kwani ni kuvaa silaha zote za MUNGU.

Swali la muhimu ni, ‘inamaanisha nini kuomba katika Roho? Maana iliyo fupi ingekuwa kwamba twaomba katika Roho pale maombi yetu yanapokuwa yamewezeshwa na Roho Mtakatifu. Hatuna budi kuongozwa na Roho juu ya nini cha kuomba na ni muda gani wa kuomba. Tunapoomba katika Roho, maombi yetu yatawezeshwa na Roho, Maombi yetu yataleta matokeo na yataleta matokeo yenye nguvu. Hivyo, twaweza kuona kwamba ili kuomba katika Roho, lazima tubatizwe na Roho. Roho ya Unabii inafafanua kile kinachomaanisha juu ya kuomba katika Roho:

“Kwa Roho kila ombi la dhati huundwa, na ombi la namna hiyo hukubalika kwa MUNGU.” (Tumaini la Vizazi Vyote uk. 189)

“Akirejelea kauli ya Paulo katika Warumi 8:26 na 27, anaandika:

“Ni lazima tuombe si kwa Jina la Kristo bali pia kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Hili hueleza nini inamaanisha pale inaposemwa kwamba Roho hutupatanisha sisi,

akiomba kwa kuugua kusikoweza kutamkika. Warumi 8:26. Ombi la namna hiyo MUNGU hupendezwa kulijibu” (Christ’s Object Lessons, p. 147)

Ni Roho Mtakatifu atuitaye kuomba. Atatuonyesha hitaji lingine kuu ili kuliombea kwa sababu MUNGU anataka kuanza kulitendea kazi hitaji hilo. Twasoma juu ya uzoefu kama huo katika maisha ya Yesu akimwombea Petro:

“Akasema, Simoni, Simoni, tazama, Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike; nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako.” (Luka 22:31, 32)

Roho Mtakatifu alimsadikisha Kristo kuomwombea Petro—na hata kufunua uliokuwa mpango wa Shetani kuhusiana na Petro. Yesu alipojua hili, mara moja alianza kuomwombea Petro. Roho Mtakatifu atafanya kile kile kupitia sisi; Ataleta akilini mwetu mtu fulani ili kumwombea. Anaweza akafunua au asifunue kile anachotutaka sisi kuwaombea wengine. Jambo muhimu ni kwamba tuitikie kuchochewa na Roho ili tuombe.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Katika maelezo ya Paulo juu ya vita ya kiroho ambapo hatuna budi kujihusisha nayo dhidi ya Shetani, alisema nini kuhusiana na sala?
- Ni jinsi gani Roho ya Unabii inafafanua kile kinachomaanisha kuhusiana na kuomba katika Roho?
- Fafanua muda ambapo Roho Mtakatifu hukuchochea kuomba kwa ajili ya mtu fulani.
- Je, huwa unatamani kuwa Mkristo aombaye katika Roho?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU adumu kuwabatiza kila mmoja kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU akuongoze kuomba kwako kwa Roho Mtakatifu.
- Kwa ajili ya wale wote uliowaorodhesha kuwaombea.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

“Utushibishe asubuhi kwa fadhili zako, Nasi tutashangilia na kufurahi siku zetu zote.” (Zaburi 90:14).

*Tuonjeshe rehema Yako—tuongoze kukiri dhambi zetu. Tulete katika kufurahi kikamilifu katika Wewe.*

# SIKU YA 13

## KUUNGANA KWA AJILI YA MAOMBI KATIKA ROHO

Kwa muda mrefu Wakristo kuungana katika maombi kwa ajili ya kusudi mahususi kumeeleweka kwa waumini kama sehemu muhimu ya maisha ya Mkristo. Kwa kipindi fulani nilidhani kuungana kwa maombi kulimaanisha kukutana kwa Wakristo wawili au zaidi kwa ajili ya sala. Wakati wa sala kila mmoja anaweza kuomba cho chote kile kinachokuja akilini. Kila sala ingekuwa na vipengele vya kawaida na pia ingekuwa na maombi kadhaa ambayo yalitofautiana na yale ya wengine waliokuwa wakiomba. Hii si ufafanuzi wa kibiblia wa Wakristo wanaoungana pamoja kwa ajili ya maombi. Hapana, sala ya umoja ni Wakristo wawili au zaidi wanaoombea kitu kimoja. Wameungana katika hamu, kusudi, na ombi. Wanaomba pamoja mahali na wakati mmoja kwa lengo moja la maombi. Ikiwa hawawezi kukutana mahali pamoja ili kuomba, basi wataomba kwa wakati mmoja kwa lengo moja la maombi, au wanaweza kuomba pamoja kwenye simu. Hata hivyo, ikiwezekana, ni nguvu zaidi kwa kila mmoja ikiwa watakutana pamoja kwa ajili ya maombi.

Katika maisha yetu binafsi, sala ya umoja na waumini wenzetu ni nguvu yenye nguvu dhidi ya Shetani. Hii ndiyo sababu Yakobo anatushauri tuungane pamoja tunapoombea wagonjwa na kuombeana:

“Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la BWANA. Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na BWANA atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa. Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.” Yakobo 5:14-16

Kwa kweli, ni muhimu kwa wale walio tayari kukutana na Yesu atakaporudi kuwa wameingia katika maombi ya kweli na ya umoja kwa ajili ya kila mmoja. Hatukuumbwa kusimama peke yetu katika vita vyetu na Shetani. Tunahitajiana maombi ya kila mmoja kwa ajili ya ushindi kamili dhidi ya adui.

Maombi ya pamoja pia ni muhimu kwa ajili ya kuendeleza ufalme wa MUNGU duniani. Shetani atapinga kila hatua inayoendelea ya kazi ya MUNGU. Maombi ya pamoja yataongeza kwa kiasi kikubwa nguvu ya MUNGU ili kuendeleza ufalme Wake.

Agano la Kale lina marejeleo mengi ya waumini wanaoungana pamoja katika maombi. "Mwalimu" katika Mhubiri anatoa somo muhimu kuhusu umuhimu wa wengine kujiunga nasi katika vita vyetu dhidi ya adui yetu, Shetani:

“Hata ikiwa mtu aweza kumshinda yule aliye peke yake, wawili watampinga; wala kamba ya nyuzi tatu haikatiki upesi.” (Mhubiri 4:12)

Kitabu cha Walawi kinatuambia:

“Na watu watano wa kwenu watawafukuza watu mia, na watu mia wa kwenu watawafukuza watu elfu kumi; na adui zenu wataanguka mbele yenu kwa upanga.” (Walawi 26:8)

Tukijaribu kusimama peke yetu katika vita dhidi ya Shetani na majaribu yake, tutashindwa kwa urahisi zaidi. Kama "mwalimu" asemavyo, mmoja pekee anaweza kushindwa kwa urahisi zaidi, huku wawili wakiweza kujilinda—na watatu wakiwa na nguvu zaidi. Hii ndiyo sababu kushirikiana katika maombi na Wakristo wengine ni muhimu sana na wenye nguvu.

Yesu alitoa kauli muhimu zaidi kuhusu umuhimu—na hata ulazima—wa waumini wawili au zaidi kujiunga pamoja katika ushirika na maombi.

“Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni. Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.” (Mathayo 18:19, 20)

“Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.” (1 Yohana 5:14, 15).

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Jadili kuhusiana na kuungana kwa sala katika Roho.
- Toa andiko linaloonyesha kuwa sala ya pamoja ina ufanisi zaidi kuliko Mkristo akiomba peke yake.
- Je, unafikiri Shetani huwataka Wakristo kuungana pamoja kwa ajili ya sala?
- Unaweza kufanya nini ili kuhusika zaidi katika kuungana pamoja katika sala pamoja na waumini wenzako?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili kesha hili pamoja naye. Omba na m Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU adumu kuwabatiza kila mmoja kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU akuongoze kuungana kila mara pamoja na waumini wenzako katika sala.
- Kwa ajili ya wale wote uliowaorodhesha kuwaombea.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

“Unigeuze macho yangu nisitazame visivyofaa, Unihuishe katika njia yako.” (Zaburi 119:37).

*Nifanye nisitamani mambo ya dunia hii. Yahuishe maisha yangu ya kiroho*

## SIKU YA 14

## MAOMBI STAHIMILIVU KATIKA ROHO

Katika karne zote, sala ya kudumu imechukuliwa kuwa sehemu muhimu ya maendeleo ya ufalme wa MUNGU duniani. Hata hivyo, sisi tunaoishi katika utamaduni wa kileo huwa tunatamani majibu ya haraka kwa ajili ya matatizo yetu. Mara nyingi mtazamo huu wa kutatua matatizo haraka hujipatia njia yake katika maisha yetu ya sala. Mara nyingi tutaomba kitu mara kwa mara, lakini si kwa kudumu kuomba kwa ustahimilivu. Ukweli ni kwamba kuomba kwa bidii si suala la hiari; ni la lazima, kama vile sala ya pamoja ilivyo ya lazima, ikiwa tunataka kumshinda adui yetu kwa mtu mmojammoja na kwa pamoja kama kanisa. Wale walio tayari kukutana na Yesu watajua kutokana na uzoefu wao binafsi maana ya maombi yenye ustahimilivu. Maombi yatakuwa yamechukua jukumu kubwa katika kuwaandaa kwa ajili ya tukio hilo kuu la marejeo Yake.

Yesu binafsi alifahamu umuhimu wa maombi yenye kuvumilia. Mara nyingi alitumia usiku kucha katika maombi. Katika Luka 18, alisimulia kisa kilichoonyesha wazi umuhimu wa kila muumini kuingia katika maombi ya kudumu. Vifungu viwili muhimu vinasisitiza hoja Yake. Luka anawasilisha mfano wenye maneno:

"Akawaambia mfano, ya kwamba imewapasa kumwomba MUNGU sikuzote, wala wasikate tamaa." (Luka 18:1).

Kusudi la mfano huu lilikuwa kutufundisha umuhimu wa kudumu katika maombi. Luka alijua Yesu alifundisha kwamba ni sharti, au tunapaswa daima kuomba kila wakati na tusizimie, au kuacha kuomba, hadi tupate jibu. Yesu anafundisha katika mfano huu kwamba tunapaswa kuendelea kuomba, na tusiache au kukata tamaa. Kifungu cha pili kinachosisitiza umuhimu wa kudumu katika maombi ni hiki

"Na MUNGU, je! Hatawapatia haki wateule wake wanaomlilia mchana na usiku, naye ni mvumilivu kwao?" (mstari wa 7).

Hapa Yesu anafundisha wazi kwamba mara nyingi majibu ya MUNGU kwa maombi yetu huja tu kama matokeo ya kilio chetu kwake "mchana na usiku." Kuomba kwa haraka hakuleti matokeo ambayo maombi ya kudumu yenye kuvumilia yataleta.

Ellen White alihisi udhaifu wa kiroho miongoni mwa watu katika siku zake. Alimuuliza malaika wa MUNGU kwa nini ilikuwa hivyo. Angalia jibu:

"Nilimuuliza malaika kwa nini hakukuwa na imani na nguvu tena katika Israeli. akasema: 'Mnaachilia mkono wa BWANA mapema sana. Peleka maombi yenu kwenye kiti cha enzi, na mshikilie kwa imani thabiti. Ahadi ni hakika. Aminini kwamba mwapokea mnayoomba, nanyi mtapata.' Kisha nikaelekezwa kwa Eliya. Alikuwa kama sisi, na aliomba kwa bidii. Imani yake ilistahimili jaribu. Mara saba aliomba mbele za BWANA, na mwisho wingu lilionekana" (Early Writings, uk. 73).

Wengi wetu bado "tunaachilia mkono wa BWANA mapema sana." Lazima tujifunze jinsi ya kudumu kwa muda mrefu na BWANA katika maombi.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Inamaanisha nini kudumu na MUNGU katika maombi?
- Je, unafikiri kuomba kwa kudumu ni rahisi kwa Mkristo wa kawaida katika Ulimwengu wa Magharibi? Kwa nini, au kwa nini isiwe hivyo?
- Yesu alisema nini kuhusu umuhimu wa kudumu katika maombi?
- Malaika alimwambia nini Ellen White kuhusu sababu ya kuwepo kwa nguvu ndogo sana katika kanisa la MUNGU leo?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU akuongoze ujifunze jinsi ya kudumu katika maombi
- Kwa ajili ya watu walio kwenye orodha yako ya kuwaombea.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Maana kama vile kijana amwoavyo mwanamwali, ndivyo wana wako watakavyokuoa wewe; na kama vile bwana arusi amfurahiavyo bibi arusi, ndivyo MUNGU wako atakavyokufurahia wewe. Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalemu; hawatanyamaza mchana wala usiku; ninyi wenye kumkumbusha BWANA, msiwe na kimya; wala msimwache akae kimya, mpaka atakapoufanya imara Yerusalemu, na kuufanya kuwa sifa duniani." (Isaya 62:5-7).

*Tufanye tukuombe daima hadi utuhuishe, na utusaidie tulisifu jina lako katika jumuiya hii.*

## SIKU YA 15

## MAOMBI YA MAOMBEZI KATIKA ROHO KWA AJILI YA WENGINE

Kanuni ya kudumu katika maombi inatumika katika kila eneo la maisha ya Kikristo, ikiwa ni pamoja na juhudi zetu za kuwaongoza wengine kwa Kristo. Inapaswa kuwa wazi kutokana na majadiliano yetu ya awali kwamba maombi yetu ni muhimu kwa ajili ya wokovu wa wale walio katika mzunguko wetu wa familia na marafiki.

Paulo anawahimiza Wakristo kufanya “maombezi” kwa ajili ya watu wote:

“Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote; kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za MUNGU Mwokozi wetu” (1 Timotheo 2:1-3).

Tunapaswa kuanzisha mikutano na MUNGU kupitia maombi ya maombezi. Maombi yetu kwa ajili ya waliopotea huleta katika kukutana kwa ajili ya upatanisho kati yao na MUNGU na mikutano ya utengano kati yao na Shetani. Maombi ya upatanisho ni kipengele kikubwa katika……"huduma ya upatanisho…” kila Mkristo ameitwa kushiriki katika:

“Lakini vyote pia vyatokana na MUNGU, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; yaani, MUNGU alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho.” (2 Wakorintho 5:18, 19).

Katika sala yake kwa Baba katika Yohana 17, Kristo anatoa sala ya upatanisho kwamba “umoja ufanyike kati ya Baba na waumini:

“Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.” (Yohana 17:20, 21).

Kristo anaomba upatanisho kamili kati ya Baba na waumini wote. Hakuomba tu ombi hilo la maombezi kwa ajili yetu kwa miaka 2,000 iliyopita, Anaendelea kutuombea maombi ya upatanisho leo:

"Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao MUNGU kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee" (Waebrania 7:25).

Katika barua zote za Paulo tunasoma kuhusu maombezi yake ya kila mara kwa MUNGU kwa niaba ya wale anaowaandikia:

"Kwa maana MUNGU, nimwabuduye kwa roho yangu katika Injili ya Mwana wake, ni shahidi wangu jinsi niwatajavyo pasipo kukoma" (Warumi 1:9).

"Kwa sababu hiyo mimi nami, tangu nilipopata habari za imani yenu katika BWANA Yesu, na pendo lenu kwa watakatifu wote, siachi kutoa shukrani kwa ajili yenu; nikiwakumbuka katika sala zangu" (Waefeso 1:15, 16).

"" (Wakolosai 1:9).

Paulo aliwajua vizuri na aliwapenda sana. Hakika alielewa ulazima wa kuwaombea watakatifu wote kila mara. Alihimiza kila Mkristo kufanya vivyo hivyo kwa ajili ya kila mmoja:

"Kwa sababu hiyo sisi nasi, tangu siku ile tuliposikia, hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu, ili mjazwe maarifa ya mapenzi yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni" (Waefeso 6:18).

MUNGU alifunua umuhimu wa maombezi ya upatanisho pale Samweli alipozungumza maneno yafuatayo kwa Mfalme Sauli:

"Walakini mimi, hasha! Nisimtende BWANA dhambi kwa kuacha kuwaombea ninyi; lakini nitawaelimisha katika njia iliyo njema, na kunyoka" (1 Samweli 12:23).

Hapa tunajifunza kwamba ni dhambi kwetu kukataa kumwombea mtu mwingine. Roho ya Unabii inahimiza kuombeana kwa maneno haya:

"Ingawa MUNGU hakai katika mahekalu yaliyojengwa kwa mikono, lakini anaheshimu pamoja na uwepo wake, makusanyiko ya watu wake. Ameahidi kwamba pale wanapokusanyika pamoja kumtafuta, kukiri dhambi zao, na kumwombea kila mmoja, atakutana nao kwa Roho wake. Lakini wale wanaokusanyika kumwabudu wanapaswa kuondoa kila kitu kibaya. Wasipomwabudu katika roho na kweli na katika uzuri wa utakatifu, kukusanyika kwao pamoja hakutawafaidia kitu" (Review and Herald, Novemba 30, 1905).

Wakristo wanapojazwa Roho kila siku, MUNGU atawaongoza katika maisha ya maombi ya maombezi. Atawakumbusha ni nani wa kumwombea na, mara nyingi, nini cha kuombea katika maisha ya kila mtu. Kwa hivyo, tunaweza kuona wazi

ni kwa nini Shetani atafanya kila awezalo kutufanya tuamini kwamba sivyo ilivyo muhimu au muhimu kwamba hasahasa tuombeane. Anataka tuamini kwamba si lazima sana kwetu kuwaombea wale walio nje na Kristo. Anataka tuamini kwamba MUNGU atafanya kazi kwa ajili ya wokovu wa waliopotea hata kama hatuwaombei wale marafiki na wale walio ndani ya malango ya familia zetu. Tunatumaini, hutaamini uongo wake kuhusu umuhimu wa maombi kwa ajili ya wengine au wewe mwenyewe. Hii ndiyo sababu atashambulia maisha yetu ya sala, pengine zaidi ya sehemu nyingine yoyote ya maisha yetu ya kiroho.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Mkristo anapomfanyia mtu maombezi, ni kipi ambacho anakifanya?
- Ni kwa kipi hasa, Yesu alipofanya maombezi katika kuwaombea wafuasi Wake, kama ilivyoandikwa katika Yohana 17?
- Je, maombi ya uombezi ni fursa au ni lazima? Kwa nini?
- Shetani ameshambuliaje maisha yako ya sala?
- Unawezaje kuwa mwombezi bora zaidi wa maombi kwa ajili ya wengine?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU akuongoze uwe mwombezi mzuri wa maombi kwa ajili 44aw engine.
- Kwa ajili ya watu walio kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Nami nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi; nitawatakaseni na uchafu wenu wote, na vinyago vyenu vyote. Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda." (Ezekieli 36:25-27).

*Fungua macho yetu kwa sanamu za kidunia katika maisha yetu na utusafishe kutokana na Tupe mioyo mipya na hamu ya kukutumikia Wewe—tufanye tukutii katika njia zetu zote.*

## SIKU YA 16

## KUOMBA AHADI ZA MUNGU KATIKA ROHO

MUNGU ametupa ahadi nyingi katika Biblia ili kukidhi kila hitaji letu. Agano la Kale na Jipya yote yana mifano bora ya Watu wa MUNGU wakidai ahadi za Neno Lake wanapokabiliwa na magumu. Mojawapo ya uzoefu wangu wa kwanza wa mafundisho ya Biblia kuhusu maombi ilikuwa katika The ABCys of Bible Prayer, kitabu kilichoandikwa na Glen Coon. Nilijifunza maana ya kudai ahadi za MUNGU katika maombi kama kijana Mkristo, na imethibitika kuwa baraka kubwa katika maisha yangu na utumishi wangu. Kanuni ya maombi ni rahisi:

**Omba:**

"Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa" (Mathayo 7:7).

**Amini:**

"Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." (Marko 11:24).

**Dai ahadi hiyo kwa shukrani kabla jibu lolote halijaonekana:**

"Basi wakaliondoa lile jiwe. Yesu akainua macho yake juu, akasema, Baba, nakushukuru kwa kuwa umenisikia. Nami nalijua ya kuwa wewe wanisikia sikuzote; lakini kwa ajili ya mkutano huu wanaohudhuria nalisema haya, ili wapate kusadiki kwamba ndiwe uliyenituma. Naye akiisha kusema hayo, akalia kwa sauti kuu, Lazaro, njoo huku nje." (Yohana 11:41-43).

Katika mistari hii tunaona kwamba Yesu alimshukuru Baba kwa kusikia na kujibu maombi yake kabla ya ushahidi wa kujibiwa.

Ahadi za MUNGU ni hakika. Tunaweza kuwa na uhakika kwamba MUNGU atafanya kile anachosema:

"MUNGU si mtu, aseme uongo; Wala si mwanadamu, ajute; Iwapo amesema, hatalitenda? Iwapo amenena, hatalifikiliza?" (Hesabu 23:19).

**Na aweza kufanya kile anachoahidi:**

"Aa! BWANA MUNGU, tazama, wewe umeziumba mbingu na nchi, kwa uweza wako mkuu na kwa mkono wako ulionyoshwa; hapana neno lililo gumu usiloliweza" (Yeremia 32:17).

Kama vile mti wa mwaloni ulivyo kwenye mbegu ya muoka, ndivyo ilivyo utimilifu wa ahadi ya MUNGU katika ahadi yenyewe inapodaiwa kwa imani. Kuhusu ahadi za Neno la MUNGU, Roho ya Unabii inasema:

"Katika kila amri na katika kila ahadi ya neno la MUNGU kuna uweza, uzima hasa ule wa MUNGU, ambao kwa huo amri yaweza kutimizwa na ahadi kujulikana" (Vielelezo vya Mafundisho ya Kristo, uk. 38).

Nguvu ya MUNGU na uzima wake vimo katika ahadi za Biblia.

Hakuna kinachoweza kuzuia ahadi Zake kutimizwa tunapozidai kwa imani katika maombi ya kudumu.

Katika 2 Mambo ya Nyakati 20 tunapata mfano mzuri wa maombi ya kudai ahadi za MUNGU. Yehoshafati, Mfalme wa Yuda, alikuwa akikabiliwa na uvamizi uliokuwa wa muungano wa majeshi. Alikuwa amejiandaa kwa ajili ya mgogoro kama huo kwa kujenga jeshi na ulinzi wa Yuda. Alikuwa na zaidi ya watu milioni 1 waliofunzwa vizuri wanaume walio tayari kwa vita. Hata hivyo, tishio hilo lilipojulikana kwa mfalme, jibu lake la kwanza halikuwa kutegemea maandalizi yake ya vita, bali badala yake alimtazama BWANA.

Tunapokabiliwa na matatizo maishani, majibu yetu yanapaswa kuwa yaleyale—mtazame BWANA kwanza. Hii haimaanishi kwamba hatufanyi tunachoweza ili kukabiliana na hali yoyote inayoweza kutokea. Hatari ni kwamba tuna mwelekeo wa papo kwa hapo kutegemea uwezo wetu wa kibinadamu ili kujiokoa. Akili zetu mara nyingi huanza kubuni njia za kutatua tatizo badala ya kumgeukia MUNGU kwanza. Jibu la Yehoshafati ni mfano mzuri kwetu kufuata.

Sala ya Yehoshafati imeandikwa katika 2 Mambo ya Nyakati 20:6-13:

"Akasema, Ee BWANA, MUNGU wa baba zetu, si wewe uliye MUNGU mbinguni? Tena si wewe utawalaye falme zote za mataifa? Na mkononi mwako mna uweza na nguvu, asiweze mtu ye yote kusimama kinyume chako. Si wewe, Ee MUNGU wetu, uliyewafukuza wenyeji wa nchi hii mbele ya watu wako Israeli, ukawapa wazao wa Ibrahimu rafiki yako hata milele? Nao walikaa humo, wamekujengea patakatifu pa jina lako humo, wakisema, Yakitujia mabaya, upanga, hukumu, au tauni, au njaa, tutasimama mbele ya nyumba hii, na mbele zako, (maana jina lako limo katika nyumba hii), na kukulilia katika shida yetu, nawe utasikia na kuokoa. Na sasa, tazama, wana wa Amoni, na Moabu, na wa mlima Seiri, ambao hukuwaacha Israeli waingie katika nchi yao, walipotoka nchi ya Misri; lakini wakawageukia mbali, wasiwaharibu; tazama, jinsi wanavyotulipa, wakija kututupa toka milki yako, uliyoturithisha. Ee MUNGU wetu, je! Hutawahukumu? Maana sisi hatuna uwezo juu ya jamii kubwa hii, wanaotujia juu yetu; wala

hatujui tufanyeje; lakini macho yetu yatazama kwako. Wakasimama Yuda wote mbele za BWANA, pamoja na wadogo wao, na wake zao, na watoto wao."

Sala hii inaonyesha hatua tano za kuomba kwa ushindi kwa ajili ya ahadi za MUNGU:

- Kwanza, mfalme alianza kwa kusifu sifa za MUNGU, hasa zile zinazohusiana na tatizo alilokuwa akikabiliana nalo (mstari wa 6). Alipokabiliwa na adui, kama Yehoshafati alivyokuwa, ilikuwa jambo la kumhimiza kwamba MUNGU anatawala tawala zote za mataifa kwamba, "nguvu na uweza vi mkononi Mwake, na kwamba hakuna mtu awezaye kumzuia.
- Pili, mfalme alikumbuka ushindi uliopita, sawa na ushindi wa sasa ambao Yuda waliuhitaji (mstari wa 7). Akikumbuka msaada wa MUNGU hapo awali, kama inavyohusiana na hitaji letu leo, linatukumbusha uaminifu wa MUNGU na kujenga imani yetu.
- Tatu, alisema katika sala ahadi ambayo MUNGU alikuwa amewapa watu wake katika uzoefu uliopita—ahadi inayohusiana na tatizo alilokuwa akikabiliana nalo (mistari ya 8 na 9).
- Baada ya hatua hizi tatu katika maombi, Yehoshafati akataja tatizo (mistari ya 10-12).
- Hatimaye, alimsifu MUNGU kabla ya ushahidi wowote wa ushindi kuonekana. (mistari ya 18 na 19).

Angalia kanuni ya kuomba ahadi za MUNGU—na sio kuzingatia tatizo: sifa, ushindi uliopita, ahadi, tatizo, sifa.

**Tafakari na Majadiliano ya Binafsi**

- Simulia wakati ulipoomba ahadi ya MUNGU, na jinsi hiyo ilivyotofautiana tangu wakati ulipozingatia tatizo katika maombi pekee?
- Je, ni nini ABC za maombi?
- Ni vipengele gani vya sala ya Mfalme Yehoshafati?
- Unaweza kufanya nini ili kuanza kuomba ahadi za MUNGU badala ya kuomba tatizo?
- Orodhesha ahadi zako uzipendazo katika Neno la MUNGU?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na mjadiliane naye kuhusu ibada hii. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU akuongoze ujifunze jinsi ya kuomba ahadi zake badala ya kuzingatia matatizo unayokabiliana nayo.
- Kwa ajili ya watu walio kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Unifahamishe nami nitaishika sheria yako, Naam, nitaitii kwa moyo wangu wote" (Zaburi 119:34).

*Nipe hamu ya kukutii kwa moyo wangu wote.*

# SEHEMU YA III—UBATIZO WA ROHO NA UINJILISTI

## SIKU YA 17

## KAZI YA INJILI YAKAMILIKA CHINI YA UWEZA WA ROHO MTAKATIFU

Yesu alitabiri kwamba “Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.” (Mathayo 24:14). Kabla tu ya marejeo ya Yesu, kutakuwa na mlipuko mkubwa wa uinjilisti utakaotoa ushuhuda mkuu wa injili hapa duniani.

Nabii Yoeli alitabiri kumiminwa mara mbili kwa Roho Mtakatifu—kwa mara ya kwanza au mvua ya vuli na mvua ya masika:

“Furahini, basi, enyi wana wa Sayuni, mkamfurahie BWANA, MUNGU wenu; kwa kuwa yeye huwapa ninyi mvua ya masika, kwa kipimo cha haki, naye huwanyeshea mvua, mvua ya masika, na mvua ya vuli, kama kwanza.” (Yoeli 2:23).

Petro alionyesha katika mahubiri yake siku ya Pentekoste kwamba kumwagwa kule kwa mara ya kwanza, au mvua ya vuli, ya Roho Mtakatifu kulikuwa kumeanza siku hiyo:

“lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli, Itakuwa siku za mwisho, asema MUNGU, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto. Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake Roho yangu, nao watatabiri.” (Matendo 2:16-18).

Mvua hii ya awali ya Roho pia huitwa ubatizo wa Roho Mtakatifu:

“Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache. Basi walipokutanika, wakamwuliza, wakisema, Je! BWANA, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme? Akawaambia, Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.” (Matendo 1:4-8).

Kitabu cha Matendo kinaelezea mlipuko mkubwa wa uinjilisti uliovuna maelfu kwa Kristo.

Kila Mkristo ambaye amesoma kitabu cha Matendo ya Mitume ametamani pengine siku ambayo utendaji kazi mkuu kama huo wa Roho Mtakatifu utafanyika tena. Miaka kadhaa iliyopita nilianza kuelewa vyema jinsi utendaji mkuu wa Roho wa MUNGU utakavyotokea nilipoanza kujifunza na kutafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. MUNGU alianza kufafanua jinsi waumini "waliotiwa mafuta, waliojazwa na Roho" atakavyowatumia kuwavuta maelfu kwa Kristo. Niligundua kwamba mwinjilisti wa kitaaaluma na matangazo ya redio au televisheni hayangeimaliza kazi ya MUNGU ya siku za mwisho, ingawa hizi zitachukua jukumu. Badala yake, kazi ya MUNGU itakamilika pale watu Wake watakapotafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu na kumruhusu Kristo kuwafikia wengine kupitia wao. Kazi ya MUNGU haitakamilika kwa mpango au mbinu mpya; MUNGU atakamilisha kazi Yake kupitia waumini waliojazwa Roho Mtakatifu ambao hujisalimisha kikamilifu kwa Kristo na kumruhusu aishi ndani yao na kuwahudumia wengine kupitia wao. Ndiyo maana Yesu aliwaambia wanafunzi Wake wangojee ubatizo wa Roho Mtakatifu kabla ya kutaka kuipeleka injili ulimwenguni (Matendo 1:4-8). Hata ingawa walikuwa pamoja na Yesu na kuwahudumia wengine kwa muda wa miaka mitatu na nusu, hawakuwa tayari kuwaambia ulimwengu kuhusu Yesu. Walihitaji kusubiri nguvu ya Roho.

Wakristo waliojiweka wakfu wanapompata Kristo kwa njia hii, kwa mara nyingine ya pili mlipuko mkubwa wa uinjilisti utatokea, na kwa mara ya pili tena Roho Mtakatifu, au mvua ya masika, itanyesha juu ya dunia hii. Sehemu ya masomo haya ya ibada imetolewa kumsaidia msomaji kuelewa jinsi mlipuko huu mkuu wa pili wa uinjilisti utakavyotokea, na jinsi kila mwamini anavyoweza kuwa sehemu yake. Kwa kweli, wote walio tayari kukutana na Yesu atakaporudi watakuwa wameshiriki katika hilo.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Je, umewahi kuhisi nguvu za Roho Mtakatifu kama ulivyohisi?
- Ungependa kuwashuhudia wengine?
- Wanafunzi walipaswa kusubiri nini kabla ya kupeleka injili kwa dunia, na kwa nini?
- Unafikiri ni nini kitakuwa kigezo kikuu katika kazi ya MUNGU kuwa imekamilika?
- Je, unataka kuwa sehemu ya mlipuko mkuu wa mwisho wa uinjilisti?
- Unawezaje kuwa sehemu ya kazi hii ya mwisho ya uinjilisti ya MUNGU?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU akuongoze ujifunze jinsi unavyoweza kuwa mtendaji mzuri shahidi kwa ajili ya Yesu.
- Kwa ajili ya watu walio kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Ee BWANA, nimesikia habari zako, nami naogopa; Ee BWANA, fufua kazi yako katikati ya miaka; Katikati ya miaka tangaza habari yake; Katika ghadhabu kumbuka rehema." (Habakuki 3:2).

*Utuongoze kutoka katika dhambi zetu; utuhurumie na utusamehe. Utukuze. Jina lako kupitia matendo makuu ya wokovu.*

## SIKU YA 18

## UBATIZO WA ROHO NA USHUHUDA

Waadventista wa sabato, pamoja na Wakristo wengine wengi, wamekuwa wakitabiri marejeo ya pili ya Kristo kwa miaka mingi. Siku ya saba Waadventista wanaamini kwamba Kristo angeweza kuja kabla ya sasa ikiwa mambo fulani yangetokea. Mfano wa Wanawali 10 unafundisha kwamba kurudi kwa BWANA arusi kungekawishwa.

Ni nini kiini cha kuchelewa huku kurudi kwa Kristo? Ninaamini kuna sababu mbili. Kwanza, watu wa MUNGU hawako tayari. Pili, kazi ya kuhubiri injili kwa ulimwengu, kuwaonya kuhusu kuja kwa Kristo, na matukio yanayozunguka tukio hilo hayajatokea. Ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo Sura ya 14 haujaenda ulimwenguni, kama ilivyopaswa kuwa kabla ya kurudi kwa Kristo:

"Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni MUNGU, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji. Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake. Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya MUNGU iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake. Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za MUNGU, na imani ya Yesu. Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Andika, Heri wafu wafao katika BWANA tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao. Kisha nikaona, na tazama, wingu jeupe, na juu ya wingu hilo ameketi mmoja, mfano wa Mwanadamu, mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa chake, na katika mkono wake mundu mkali." (Ufunuo 14:6-14).

Matukio makubwa na ya kutisha yatakuja duniani kabla tu ya Kristo kuja mara ya pili. Zamani watu wa MUNGU hawakuwa tayari kwa ajili ya matukio, kama

ilivyokuwa katika siku za Nuhu ambapo gharika haikuja mpaka onyo la mafuriko lilipokuwa limewafikia wakazi wa dunia, na safina ilikuwa tayari kwa ajili ya mafuriko:

"Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu." (Mathayo 24:37).

Ujumbe wa onyo utatolewa na "safina," au kanisa, litakuwa tayari. Ndipo mwisho utakapokuja.

Kristo aliufikishaje ujumbe mzito zaidi wa Nuhu kwa ulimwengu wa siku za Nuhu? Petro anatuambia katika barua yake ya kwanza. Roho Mtakatifu aliyem-"huisha" Kristo au aliyemfufua kutoka kaburini, ni Roho ambaye kupitia huyo, Kristo kwa kumtumia Nuhu "alihubiri" kwa wanaume na wanawake (wanaoitwa roho) ambao walikuwa mateka, au wafungwa, wa Shetani:

"Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa MUNGU; mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa, ambayo kwa hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri; watu wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa MUNGU ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji." (1 Petro 3:18-20).

Hesabu 27:15 na 16 inaonyesha kwamba Biblia inatumia neno roho kurejea wanaume na wanawake walio hai:

"Mimi, BWANA, nimekuita katika haki, nami nitakushika mkono, na kukulinda, na kukutoa uwe agano la watu, na nuru ya mataifa; kuyafunua macho ya vipofu, kuwatoa gerezani waliofungwa, kuwatoa wale walioketi gizani katika nyumba ya kufungwa." (Isaya 42:6, 7).

Kwa hivyo, tunaona kutoka kwa Maandiko kwamba ilikuwa Kristo, kwa Roho Mtakatifu, akizungumza kupitia Nuhu aliyewatayarisha wakazi wa dunia kwa ajili ya mafuriko. Ndivyo itakavyokuwa katika siku za mwisho kabla tu ya kuja kwa Kristo mara ya pili (Mathayo 24:37). Kristo atanena kwa njia ya Roho Mtakatifu kupitia Wakristo waliojazwa na Roho kuandaa ulimwengu kwa ajili ya Marejeo ya Pili.

Nimekuwa Mkristo Mwadventista wa Sabato kwa miaka mingi, na mchungaji kwa miaka mingi. Katika dhehebu langu, na pia katika madhehebu mengine ya Kikristo, naamini muda na pesa nyingi zimetumika katika mipango, programu, na mbinu za kumleta Kristo ulimwenguni. Mimi sipingi mipango, programu, na mbinu, lakini ninaogopa kwamba, mara nyingi zaidi, tumekuwa tukitegemea

mambo haya ili kukamilisha kazi ya MUNGU. Mipango, programu, na mbinu hazitamaliza kazi ya MUNGU. Wanenaji wazuri, matamasha makubwa ya muziki, au setilaiti hazitamaliza kazi ya MUNGU. Roho Mtakatifu wa MUNGU atakamilisha kazi ya MUNGU—Roho wa MUNGU, akizungumza na kuhudumu kupitia wanaume na wanawake waliojazwa na Roho.

**Tafakari na Majadiliano ya Binafsi**

- Unafikiri kwa nini Yesu hajaja bado?
- Yesu alisema nini kuhusu siku za Nuhu na siku zetu?
- MUNGU alimalizaje kazi yake ya onyo katika siku za Nuhu?
- Unafikiri MUNGU atamtumia nani zaidi au nini katika kukamilisha kazi Yake duniani?
- Unaweza kufanya nini ili uwe mtu ambaye MUNGU atamtumia kukamilisha kazi Yake?

**Shughuli ya Maombi**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU ashuhudie kupitia kwenu kwa Roho Wake, kama alivyofanya kupitia Nuhu.
- Kwa ajili ya watu walio kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Uniendeshe katika mapito ya maagizo yako, Kwa maana nimependezwa nayo." (Zaburi 119:35).

*Nifanye nifurahie amri zako na si mambo ya ulimwengu huu.*

## SIKU YA 19

## UMUHIMU WA UBATIZO WA ROHO KATIKA KUSHUHUDIA

Ukweli wa umuhimu wa ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa ajili ya kushuhudia umefunuliwa waziwazi katika Agano Jipya. Tunauona katika uzoefu wa Yesu. Luka anaelezea ubatizo wa Kristo katika sura ya tatu ya kitabu chake cha injili. Anatuambia kwamba wakati wa ubatizo wa Kristo aliomba, na "Roho Mtakatifu alishuka" juu yake:

"Ikawa, watu wote walipokwisha kubatizwa, na Yesu naye amebatizwa, naye anaomba, mbingu zilifunuka; Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili, kama hua; sauti ikatoka mbinguni, Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe." (Luka 3:21, 22).

Kuanzia wakati huo na kuendelea Luka anasema kwamba Yesu "alijazwa" na Roho Mtakatifu na kuhudumu katika "nguvu" za Roho:

"Na Yesu, hali amejaa Roho Mtakatifu, alirudi kutoka Yordani, akaongozwa na Roho muda wa siku arobaini nyikani" (Luka 4:1). Yesu akarudi katika nguvu ya Roho Mtakatifu ikaenea Galilaya; habari zake zikaenea kote katika eneo lote linalozunguka" (mstari wa 14).

Kabla ya ujazo huu wa Roho, au ubatizo, hakuna huduma ya Kristo iliyoandikwa; Tunaambiwa kwamba hakuna wafuasi waliokuwa wamevutwa Kwake. Mara tu baada ya kubatizwa, au kujazwa Roho, tunaambiwa kwamba "habari zake zikaenea katika nchi zote za kandokando." Baada ya Kristo kujazwa na Roho Mtakatifu, tunasoma katika injili zote juu ya maelfu wakiitikia ujumbe na huduma. Mafundisho yote ya Kristo yalitiwa mafuta na Nguvu ya Roho, ambayo ilikuwa matokeo ya kujazwa Kwake na Roho Mtakatifu, likiwa ni jawabu la maombi yake wakati wa ubatizo wake wa maji:

"Roho wa BWANA yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa, Na kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa." (mistari ya 18, 19).

"Hata siku ile alipochukuliwa juu, alipokuwa amekwisha kuwaagiza kwa Roho Mtakatifu wale mitume aliowachagua" (Matendo 1:2).

"Habari za Yesu wa Nazareti, jinsi MUNGU alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na

kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana MUNGU alikuwa pamoja naye." (Matendo 10:38).

Yesu alijua vyema umuhimu na hitaji la huduma iliyojaa Roho. Hii ndiyo sababu aliwaambia wanafunzi wangoje ahadi ya ubatizo wa Roho Mtakatifu kabla hawajaenda kutangaza injili.

"Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache." (Matendo 1:4, 5).

Yesu aliendelea kuwaambia kwamba wangepokea nguvu ya kushuhudia ikiwa pale walipopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu:

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." (mstari wa 8).

Wanafunzi walifanya kile Yesu alichowaagiza wafanye. Walisubiri na kwa umoja waliomba ahadi ya ubatizo wa Roho Mtakatifu itimizwe kwao.

"Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kwangu" (mstari wa 14).

Katika kujibu maombi yao ya siku 10, Roho Mtakatifu alikuja siku ya Pentekoste na "wote wakajazwa Roho Mtakatifu:"

"Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka." (Matendo 2:1-4).

Kilichotokea baadaye kinafichua moja ya madhumuni makuu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. MUNGU aliwatumia waumini hawa waliojazwa na Roho kusimulia kuhusu "Matendo ya ajabu ya MUNGU:"

"Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, Tazama, hawa wote wasemao si Wagalilaya? Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo? Warparthi na Wamedi na Waelami, nao wakaao Mesopotamia, Uyahudi na Kapadokia, Ponto na Asia, Frigia na Pamfilia, Misri na pande za Libia karibu na Kirene, na wageni watokao Rumi, Wayahudi na waongofu, Wakrete na Waarabu;

tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya MUNGU." (mistari 7-11).

MUNGU alishinda vikwazo vya lugha ili kufikisha habari njema za Mwokozi aliyefufuka kwa Wayahudi waliokuwepo siku hiyo. Watu elfu tatu waliitikia hubiri la Petro lililowezeshwa na Roho:

"Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu." (mstari wa 41).

Kanisa la awali liliendelea kuhudumu chini ya nguvu ya upako wa Roho Mtakatifu. MUNGU alifanya kazi kwa njia ya ajabu kupitia waumini hawa waliojazwa na Roho kuwavuta wengine wengi kwa Kristo:

"Wakimsifu MUNGU, na kuwapendeza watu wote. BWANA akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa." (mstari wa 47).

Wakristo hawa wa awali walitambua umuhimu wa kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu ili kuishi maisha ya kiMUNGU na kushuhudia kwa ufanisi kwa ajili ya BWANA.

Ubatizo wa Roho ulikuwa muhimu sana kiasi kwamba pale wanaume na wanawake wengi Samaria walikuwa wamemkubali Yesu kama Mwokozi wao na wakabatizwa katika maji. Filipo, Petro na Yohana, walitumwa kukutana nao. Punde baada ya kuwasili kwao, waliwawekea mikono waumini hawa wapya na kuwaombea kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.

"Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa MUNGU, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake. Na yeye Simoni mwenyewe aliamini akabatizwa, akashikamana na Filipo; akashangaa alipoziona ishara na miujiza mikubwa inayotendeka. Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la MUNGU, wakawapelekea Petro na Yohana; ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu; kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake BWANA Yesu. Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu." (Matendo 8:12-17).

Tunaona kipaumbele kile kile katika wito wa MUNGU kwa Sauli akiwa njiani kuelekea Dameski. Kristo alijifunua kwa Sauli katika maono:

"Lakini Sauli, akizidi kutisha na kuwaza kuwaua wanafunzi wa BWANA, akamwendea Kuhani Mkuu, akataka ampe barua za kuenda Dameski zilizoandikwa kwa masinagogi, ili akiona watu wa Njia hii, waume kwa wake,

awafunge na kuwaleta Yerusalemu. Hata alipokuwa akisafiri, ikawa anakaribia Dameski; ghafula ikamwangaza kote kote nuru kutoka mbinguni. Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, Sauli, Sauli, mbona waniudhi? Akasema, U nani wewe, BWANA? Naye akasema, Mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe. Lakini simama, uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda. Na wale watu waliosafiri pamoja naye wakasimama kimya, wakiisikia sauti, wasione mtu." (Matendo 9:1-7).

Kisha Kristo alimwelekeza Sauli aende Dameski na kusubiri zaidi maagizo, baada ya hapo MUNGU alimtuma Anania kwa Sauli ili amwekee mikono na kuomba ubatizo wa Roho Mtakatifu na uponyaji wa macho yake:

"Anania akaenda zake, akaingia mle nyumbani; akamwekea mikono akisema, Ndugu Sauli, BWANA amenituma, Yesu, yeye aliyekutokea katika njia uliyoijia, upate kuona tena, ukajazwe Roho Mtakatifu. Mara vikaanguka machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona, akasimama, akabatizwa" (mistari ya 17, 18).

Kama matokeo ya kujazwa na Roho, "Sauli alizidi kuwa hodari" (mstari wa 22). Neno nguvu halimaanishi tu nguvu za kimwili. Muktadha unaonyesha kwamba Sauli aliongezeka katika uweza na nguvu za kiroho katika kutangaza injili. Nguvu hii ya kiroho na nguvu ya kushuhudia ilitokana na ubatizo wa Roho Mtakatifu alioupokea wakati Anania alipobatizwa alimwombea.

**Tafakari na Majadiliano ya Binafsi**

- Huduma ya Yesu kwa Baba yake ilipata nguvu lini, na jinsi gani
- Je, Biblia inaelezea huduma yake ya kubatizwa kwa Roho?
- Yesu aliwaambia wanafunzi wake wafanye nini kabla hawajaanza kuhudumu?
- Kanisa la kwanza lilikuwa na matokeo gani baada ya kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu?
- Kwa nini MUNGU aliwatuma Petro na Yohana kwa waumini wapya wa Wasamaria, na Anania kwa Sauli baada ya kuongoka kwake?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU ashuhudie kupitia wewe katika nguvu za Roho.

- Kwa ajili ya watu walio kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

“Nafsi yangu imeambatana na mavumbi, Unihuishe sawasawa na neno lako” (Zaburi 119:25).

*Tuko mbali sana na mahali tunapopaswa kuwa kiroho. Turejeshe kiroho kama ulivyoahidi.*

# SIKU YA 20

## UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU NA KUANDAA NJIA KWA AJILI YA UJIO WA KRISTO

Nabii Malaki alitabiri kwamba MUNGU angemtuma Eliya, akimaanisha ujumbe wa "Eliya," kabla ya kuja kwa Yesu Kristo:

“Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya BWANA, iliyo kuu na kuogofya.” (Malaki 4:5).

Unabii huu una matumizi mawili: moja linahusu ujio wa kwanza wa Kristo; lingine linahusu ujio Wake wa pili.

Mwandishi wa injili, Luka, anatueleza kuwa Yohana Mbatizaji alitimiza matumizi ya kwanza ya unabii huu wa Malaki:

“” (Luka 1:17).

Yohana Mbatizaji aliendelea katika huduma katika “roho na nguvu” za Eliya. Hii ilimaanisha nini?

Ilimaanisha kwamba alikuwa amejaa Roho Mtakatifu na alihubiri ujumbe uliotiwa mafuta na Roho Mtakatifu ili kuandaa watu wa siku zake kwa ajili ya Masihi, ambaye angeonekana muda mfupi hapo baadaye:

“Kwa sababu atakuwa mkuu mbele za BWANA; hatakunywa divai wala kileo; naye atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye.” (Luka 1:15).

Nguvu ya Roho Mtakatifu ilikuwa pamoja na mahubiri ya Yohana. Umati ulifika kumsikia, na wengi walibatizwa:

“Siku zile aliondokea Yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema, Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya BWANA, Yanyosheni mapito yake. Naye Yohana mwenyewe alikuwa na vazi lake la singa za ngamia, na mshipi wa ngozi kiunoni mwake; na chakula chake kilikuwa nzige na asali ya mwitu. Ndipo walipomwendea Yerusalemu, na Uyahudi wote, na nchi zote za kandokando ya Yordani; naye akawabatiza katika mto wa Yordani, huku wakiziungama dhambi zao.” (Mathayo 3:1-6).

Yesu alikuwa na ufahamu mzuri wa unabii wa Malaki, na aliutumia kwenye huduma na ujumbe wa Yohana Mbatizaji:

“Kwa maana manabii wote na torati walitabiri mpaka wakati wa Yohana. Na ikiwa mnataka kukubali, yeye ndiye Eliya atakayekuja. Mwenye masikio, na asikie.” (Mathayo 11:13-15).

Unabii wa Malaki una matumizi ya pili, unarejelea watu watakaotoa ujumbe mkuu wa onyo kabla ya kuja kwa Yesu, unaoitwa ujumbe wa malaika watatu:

“Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni MUNGU, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji. Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake. Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya MUNGU iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake. Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za MUNGU, na imani ya Yesu.” (Ufunuo 14:6-12).

Ujumbe huu wa siku za mwisho wa Eliya unakusudiwa kuwaandaa wanaume na wanawake kwa ujio wa pili wa Kristo. Yesu anakuja! Tuwe tayari kwa Neema Yake BWANA. Kama vile Yohana Mbatizaji alivyohitaji kujazwa na Roho Mtakatifu ili kutoa ujumbe wa Eliya wa siku zake, vivyo hivyo waumini wa MUNGU wa siku za mwisho, lazima wajazwe na Roho Mtakatifu ili kutoa ujumbe wa Eliya wa siku za mwisho kwa ulimwengu wa leo. Ujumbe huu wa onyo wa siku za mwisho utakaotolewa na watu waliojazwa Roho Mtakatifu utaendelea mbele katika "roho na nguvu" za Eliya, kama vile ujumbe wa Yohana ulivyofanya.

Kwa nini ujumbe huu wa mwisho bado haujatolewa kwa nguvu kama hiyo? Umehubiriwa kwa zaidi ya miaka 150. Mamilioni ya dola yametumika, na yanaendelea kutumika kutoa ujumbe huo. Nini kimeenda kombo? Mimi binafsi naamini ukosefu wetu wa kuelewa na kupata ubatizo wa Roho Mtakatifu ndio sababu.

Simaanishi kwamba MUNGU hajabariki juhudi zetu za kuwaonya ulimwengu kuhusu ujio wa pili wa Kristo na masuala yanayohusiana na siku hizi za mwisho. Nasema kwamba bado hatujafikia baraka na nguvu kuu inayotungoja wakati watu wa MUNGU watakapokuwa watu waliojazwa Roho Mtakatifu. Wakati hilo litakapofanyika, ujumbe wa siku za mwisho wa Eliya utaendelea mbele katika "roho na nguvu" za Eliya.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Ni matumizi gani mawili ya unabii wa Malaki unahusiana na Eliya?
- Ni kwa namna gani matumizi ya kwanza ya unabii wa Malaki yalitimia?
- Yohana Mbatizaji alikuwa na nini kilichomwezesha kutoa ujumbe wa Eliya katika siku zake?
- Ujumbe wa Eliya wa leo ni nini?
- Ni uzoefu gani wa kiroho unaohitajika ili matumizi ya pili ya unabii wa Malaki yatimie?
- Nini kitatokea wakati ujumbe wa mwisho wa MUNGU utakapokuwa ukitolewa kwa "roho na nguvu" za Eliya?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na mjadili ibada hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Mtakatifu.
- Ili MUNGU awaongoze watu Wake na kanisa Lake kuwa watu waliojazwa Roho Mtakatifu.
- Kwa ajili ya wale walio kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako:**

“Unielekeze moyo wangu na shuhuda zako, Wala usiielekee tamaa.” (Zaburi 119:36).

*Nifanye nipende mashauri Yako, na uniepushe na tamaa ya fedha na madaraka.*

## SIKU YA 21

## TATIZO LA KANISA LA LAODIKIA

MUNGU alitoa historia ya kinabii ya kanisa la Kikristo katika kitabu cha Ufunuo. Ufunuo sura ya 2 na 3 vinaeleza vipindi saba vya historia ya kanisa ambavyo vinahusiana na makanisa saba halisi huko Asia, katika nchi ya Uturuki. Pia vinahusiana na vipindi saba vya kihistoria vya kanisa, kuanzia kanisa la mitume la awali hadi leo. Kanisa la saba limeelezewa katika Ufunuo 3:14-21

Enzi ya kanisa la leo inaitwa Laodikia. Jiji la Laodikia lilijulikana kwa chemchemi zake za tiba ya maji moto na baridi (kama Kikuletwa na Bogoria huko Manyara). Manufaa ya tiba ya maji yanaeleweka vizuri leo, na hili lina umuhimu tunapofikiria kuwa MUNGU anaeleza kanisa la leo kuwa vuguvugu, si moto wala si baridi (mstari wa 16). Haidotherapia ni tiba ya maji. Hii inamhuzunisha mno MUNGU, kiasi kwamba ikiwa kanisa litaendelea kuwa katika hali hii ya uvuguvugu, MUNGU atalitapika kutoka kinywani Mwake.

Kutapika ni nini?

Kutapika ni kitendo cha kulazimishwa kwa nguvu kutoka ndani ya tumbo (chakula, maji, nyongo) kupitia mdomo, kawaida hutokea kwa sababu ya ugonjwa, sumu, au kichefuchefu, na ni njia ya mwili kujiondolea vitu visivyofaa; ni tofauti na 'kuchukua' (retching) ambapo unajaribu lakini huwezi kutapika.

Kwa nini hali hii ya uvuguvugu ni hatari sana machoni pa MUNGU? Jibu linaonekana katika shauku Yake kwa kanisa. MUNGU anataka kanisa liwe moto au baridi—anataka kanisa liwe na thamani ya kitiba duniani. Unaona, kanisa lililo vuguvugu halina sifa ya kitiba—halileti faida kwa wale wanaolikaribia. MUNGU anataka kanisa lilete uhai kila linapokwenda.

Hii ni sawa na kauli ya Yesu kwamba kanisa linapaswa kuwa “chumvi ya dunia:”

“Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu.” (Mathayo 5:13).

Chumvi na tiba ya maji moto na baridi vyote vina thamani kimatibabu. Yesu alisema katika Ufunuo kwamba wale wanaobaki katika hali ya uvuguvugu, isiyo na sifa ya kutoa uzima, watatapikwa kutoka kinywani mwake. Katika Mathayo anasema kwamba chumvi ambayo "imepoteza ladha yake" itatupwa nje (5:13). Yesu anasema jambo lile lile katika Ufunuo na Mathayo. Ikiwa kanisa halina sifa

ya kitiba, basi halina thamani yoyote kwa MUNGU na hatimaye litatupwa kutoka Kwake.

MUNGU anatamani kwamba kanisa liwe moto au baridi.

Yesu alifunua jinsi uhai unavyopaswa kutiririka kutoka kwa kanisa Lake aliposema, “” Yohana alifafanua maana ya Yesu kwa kusema, “” (Yohana 7:38, 39). Kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu, uhai ungetiririka kutoka kwenye kanisa.

Tunaweza kuona wazi kuwa onyo la MUNGU kwa Wakristo wa Laodikia wa siku za mwisho ni la muhimu sana. Tunapaswa kuamka na kutambua hali yetu na kumruhusu MUNGU kutubadilisha kutoka hali isiyokuwa ya uponyaji, afya, uzima au tiba kwa watu, hadi kuwa ya tiba ili tuwe tayari kumlaki Yesu atakapokuja na kusaidia watu kuweza kuponywa na Jua la Haki. Ukweli wa kusikitisha ni kwamba Wakristo wa Laodikia hawatambui hali yao ya kiroho iliyo hatarini:

“Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi.” (Ufunuo 3:17).

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Biblia inamaanisha nini inaposema kwamba kanisa la leo ni vuguvugu?
- Kwa nini MUNGU anataka kanisa liwe moto au baridi?
- Nini kitatokea kwa mtu ambaye hatabadilika kutoka hali yake ya uvuguvugu?
- Unafikiri ni ushahidi gani unaoonyesha kwamba washiriki wa kanisa fulani mahalia wanaweza kuwa vuguvugu?
- Unafikiri ni ushahidi gani unaoweza kuonyesha kwamba wewe ni Mkristo vuguvugu?

**Kujishughulisha Kuomba**

Kutana na mwanamaombi mwenzako na jadiliana naye kuhusu ibada hii. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alitoe kanisa Lake katika hali yake ya uvuguvugu, ya Laodikia.
- Kwa ajili ya watu walio kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

“Uniangalie na kunifadhili, Maana mimi ni mkiwa na mteswa. Katika shida za moyo wangu unifanyie nafasi, Na kunitoa katika dhiki zangu. Utazame teso langu na taabu yangu; Unisamehe dhambi zangu zote.” (Zaburi 25:16-18).

*Utuhurumie kwa maana tuko katika hali ya ukiwa na dhiki ya kiroho. Utusamehe dhambi zetu na ututoe katika hali yetu ya Laodikia.*

## SIKU YA 22

## SULUHISHO LA HALI YA LAODIKIA YA KANISA

Swali muhimu sana kwa kanisa la leo ni: Tunaweza vipi kubadilishwa kutoka hali ya “kutokuwa na faida yoyote ya kimatibabu” hadi kuwa na “Sifa ya kimatibabu iletayo uzima?” Ujumbe wa MUNGU kwa Laodikia unatoa jibu. Yesu anasema Yeye anasimama mlangoni na anataka kuingia katika maisha yetu:

“Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.” (Ufunuo 3:20).

Jinsi gani tunamruhusu aingie? Kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu:

“Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu. Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu.” (Yohana 14:16-18).

Katika mistari hii Yesu anawaambia wanafunzi Wake kwamba atakuja kwao wakati Roho Mtakatifu atakapokuwa anapatikana kuishi ndani yao. Hii ilitokea siku ya Pentekoste. Kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu, Yesu anaishi ndani ya mtu mwenye imani:

*Kujazwa Roho Mtakatifu kunapaswa kutarajiwa tu kama jibu la maombi.*

“Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa.” (1 Yohana 3:24).

Ubatizo wa Roho Mtakatifu utamfanyia nini Mkristo vuguvugu? Kujazwa kwa Roho wa MUNGU kutaleta uamsho/uhuishaji kwa mpokeaji, na uhuishaji ndicho kipande pekee cha suluhisho la tatizo la Laodikia. Ni katika uhuishaji pekee ndipo kanisa litakavyokuwa na sifa ya kitiba kwa dunia hii. Ni kwa uhuishaji pekee ndipo kanisa litakapokuwa katika hali ya kiroho ambayo MUNGU anaweza kulitumia kwa njia yenye nguvu kama njia ya kuokoa wanaume na wanawake kutoka kwenye nguvu za giza.

Roho ya unabii imeelezea umuhimu na uhitaji wa haraka wa uhuishaji alipoandika:

“Uhuishaji wa Kweli wa unyofu kati yetu ndiyo hitaji letu kubwa zaidi na la haraka. Kutafuta hili ndiyo kazi yetu ya kwanza” (Selected Messages, book 1, p. 121).

Alielewa pia uhusiano kati ya kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu na uhuishaji:

“Ubatizo wa Roho Mtakatifu kama ilivyokuwa siku ya Pentekoste utaongoza katika uhuishaji wa dini ya Kweli na kwa utendaji wa mambo mengi ya ajabu” (Selected Messages, book 2, p. 57).

Ubatizo wa Roho Mtakatifu huwapa Wakristo wa Laodikia nguvu inayohitajika ili kufufuliwa kiroho, na pia nguvu ya kushuhudia. Yesu alijua vizuri umuhimu wa kile kitakachotokea wakati Roho Mtakatifu atakapomwagwa kwa nguvu za mvua ya awali siku ya Pentekoste. Akizungumza kuhusu hili, alisema:

“Nimekuja kutupa moto duniani; na ukiwa umekwisha washwa, ni nini nitakalo zaidi?” (Luka 12:49).

Moto huo Yesu alizungumzia ni moto wa Roho Mtakatifu:

“Yohana alijibu akawaambia wote, Kweli mimi nawabatiza kwa maji; lakini yuaja mtu mwenye nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto” (Luka 3:16).

Mkristo wa Laodikia anapataje ubatizo wa Roho Mtakatifu na kuishi katika maisha ya uamsho? Kwa njia ile ile ambayo waumini wanapokea Roho Mtakatifu—kwa kuomba kwa bidii na kudai ahadi ya MUNGU. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulipokelewa na kanisa la awali siku ya Pentekoste kama matokeo ya kuomba kwa pamoja kwa siku 10, wakidai ahadi ya Kristo:

“Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache…… Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi…. Hawa wote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali, pamoja nao wanawake, na Mariamu mama yake Yesu, na ndugu zake” (Matendo ya Mitume 1:4, 5, 8, 14).

Hili linathibithishwa:

“Uamsho unapaswa kutarajiwa tu kwa jibu la maombi” (Selected Messages, book 1, p. 121).

Kila Mkristo leo anahitaji kuomba sala ya Daudi:

"Je! Hutaki kurudi na kutuhuisha, Watu wako wakufurahie?" (Zaburi 85:6).

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Ni suluhisho gani la kipekee kwa tatizo la Laodikia?
- Kanisa lina hitaji gani kubwa?
- Ni mambo gani mawili kanisa lazima lifanye ili kupata uamsho wa Kweli?
- Mitume walipokeaje nguvu za uamsho wa Roho Mtakatifu?
- Unadhani nini kitakuwa kikionekana katika maisha ya kanisa na Mkristo aliyejaa Roho Mtakatifu na ambaye amehuishwa?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadiliana naye kuhusu ibada hii. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Mtakatifu Wake.
- Ili MUNGU alete uamsho na matengenezo katika maisha yenu na kanisa Lake.
- Kwa ajili ya watu walio kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Je! Hutaki kurudi na kutuhuisha, Watu wako wakufurahie?" (Zaburi 85:6).

*Tuhuishe na utuangalie tuwe watu wanaofurahi kuwa upande Wako, tusaidie tufanane na Wewe, tuwe na tabia Yako.*

## SIKU YA 23

## MAOMBI NA UINJILISTI

Neno la MUNGU linafundisha kwamba maombi ni muhimu kwa mtu binafsi na kwa kanisa ili kufurahia uhuishaji:

“Je! Hutaki kurudi na kutuhuisha, Watu wako wakufurahie?” (Zaburi 85:6).

Maombi ni muhimu kwa “ngome” za Shetani kuangushwa, na kwa wokovu wa waliopotea:

“Wote wakanywa kinywaji kile kile cha roho; kwa maana waliunywea mwamba wa roho uliowafuata; na mwamba ule ulikuwa ni Kristo. Lakini wengi sana katika wao, MUNGU hakupendezwa nao; maana waliangamizwa jangwani” 2 Wakorintho 10:4, 5).

Maombi ni muhimu kwa Mkristo kubaki katika nguvu ya BWANA:

“Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote” (Waefeso 6:18).

Najiuliza ni ajabu jinsi maombi, ambayo yanaonekana kuwa na nguvu ndogo na yasiyo na maana kwa mtu wa kawaida, ila ni muhimu sana na yenye nguvu kwa mtu wa kiroho. Kwa nini maombi ni muhimu na ya lazima katika kazi ya MUNGU?

Wale tunaowajua wako nje ya Kristo na wanaishi chini ya nguvu za Shetani wako katika hali hatari sana. Hatima yao ya milele iko hatarini kama hawatabadilika. Lakini wenyewe hawana nguvu za kubadilika. Paulo anawaelezea kama wale ambao mawazo yao yamepofushwa na Shetani:

“Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea; ambao ndani yao MUNGU wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake MUNGU. Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni BWANA; na sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya Yesu. Kwa kuwa MUNGU, aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa MUNGU katika uso wa Yesu Kristo” (2 Wakorintho 4:3-6).

Waliopotea wamepofushwa na injili kwa sababu kwao imefichwa. Neno lililotafsiriwa kama kuficha ni neno la Kigiriki ***kalupsis***, linalorejelea “pazia.”

Ufunguo wa kuokoa waliopotea ni kuondoa pazia hili linalowafanya kuwa vipofu. Kwa kuongeza kiambatisho hapo kwenye neno la Kigiriki kwa pazia neno

linakuwa “ufunuo,” au “kuvuviwa.” Hivyo, waliopotea wanahitaji kuvuviwa, au ufunuo wa Ukweli wa MUNGU. Waliopotea hawahitaji taarifa zaidi—wanahitaji kuangazia uelewa wao ili waweze “kuona” Ukweli wa injili.

Swali muhimu basi, ni jinsi gani kuvuviwa kwa hali hii kutatokea katika maisha ya waliopotea?

Maombi ya upatanisho yatawaondolea wasiokuwa na imani pazia linalosababisha upofu wa kiroho. Shetani ana mawazo na ngome za uongo, zilizojengeka vizuri katika akili za waliopotea. Habari njema ni kwamba MUNGU amempa Mkristo mamlaka ya kubomoa ngome za Shetani na kuleta “” (2 Wakorintho 10:4, 5). Mistari hii miwili ni muhimu sana linapokuja suala la kuelewa mahali pa maombezi kwa waliopotea. Roho ya unabii inaleta kwa uwazi hitaji la maombi kwa wale walioko nje ya Kristo iliponena:

“Kwa maombi mengi lazima ufanye kazi kwa ajili ya roho, kwa kuwa ndiyo njia pekee ambayo unaweza kuifikia mioyo. Hii siyo kazi yako, bali kazi ya Kristo aliye kando yako, inayovutia mioyo” (Evangelism, p. 341).

Angalia kwenye Tovuti ya MaarifaMtandaoni.Com au RohoYaUnabii.Org au RohoYaUnabii.Africa kwa vitabu hivi kama vile Uinjilisti nk.

Nukuu kamili ya Evangelism:

Tukumbuke daima kuwa ni kazi ngumu kuwaondoa watu kwenye makosa waliyopokea tangu utotoni. Tuelewe kuwa dunia si mbinguni, na tutakutana na hali za kukatisha tamaa ambazo lazima tushinde, lakini tuvumiliane kwa upole sikitiko, na huruma nyororo na wema na wale walio gizani. Kuwaleta katika nuru hakutafanikishwa kwa hoja tu, bali ni kazi ya neema ya Kristo moyoni mwenu, ikidhihirika katika tabia zenu kwa uthabiti, lakini kwa upole, usahili na unyenyekevu wa Kristo. Kwa maombi mengi fanyeni kazi kwa ajili ya roho, maana ni njia hii pekee ya kugusa mioyo. Sio kazi yenu, bali ni kazi ya Kristo aliye kando yenu, Ndiye anayegusa mioyo.......{EVsw 341:3}

Kitabu cha Praying Church Sourcebook kinatoa orodha ifuatayo ya mapenzi ya MUNGU kwa wasiookoka. Kama waumini katika Kristo tuna haki ya kuwasilisha maombi haya mbele ya kiti cha enzi kwa ajili ya waliopotea. Jumuisha yafuatayo katika maombi yako:

- Ili MUNGU awavute Kwake Yeye Mwenyewe:

“Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka; nami nitamfufua siku ya mwisho.” (Yohana 6:44).

- Ili watafute kumjua MUNGU:

“Ili wamtafute MUNGU, ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone, ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu.” (Matendo ya Mitume 17:27).

- Ili waumini Neno la MUNGU:

“Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru MUNGU bila kukoma, kwa kuwa, mlipopata lile neno la ujumbe la MUNGU mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la MUNGU; na ndivyo lilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini.” (1 Wathesalonike 2:13).

- Ili Shetani akome kuwapofusha juu ya Ukweli na mvuto wake katika maisha yao uangushwe (2 Wakorintho 4:4; 10:4, 5).
- Ili Roho Mtakatifu afanye kazi ndani yao:

“Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu. Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi; kwa habari ya haki, kwa sababu mimi naenda zangu kwa Baba, wala hamnioni tena; kwa habari ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa. Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.” (Yohana 16:8-13).

- Ili waache dhambi:

“Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake BWANA” (Matendo ya Mitume 3:19).

- Ili waamini katika Kristo kama Mwokozi:

“Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa MUNGU, ndio wale waliaminio jina lake” (Yohana 1:12).

- Ili wamtii Kristo kama BWANA:

“Si kila mtu aniambiaye, BWANA, BWANA, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.” (Mathayo 7:21).

- Ili wawe na mizizi na kukua katika Kristo:

"Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, BWANA, enendeni vivyo hivyo katika yeye; wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukrani." (Wakolosai 2:6, 7).

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Ni kwa vipi maombi ni muhimu katika kazi ya MUNGU ya kuokoa waliopotea?
- Roho ya Unabii inasema nini kuhusu maombi kwa ajili ya waliopotea?
- Maombi yanafanyaje kwa wale tunaowashuhudia?
- Una mpango gani wa kutumia kanuni za maombi kwa wale walioko kwenye orodha yako ya maombi?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na kanisa Lake.
- Ili MUNGU akuongoze kuwa mwombaji wa dhati kwa waliopotea.
- Kwa ajili ya watu walio kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Na uzuri wa BWANA, MUNGU wetu, uwe juu yetu, Na kazi ya mikono yetu utufanyie thabiti, Naam, kazi ya mikono yetu uithibitishe." (Zaburi 90:17).

*Tabia Yako na ionekane katika maisha yetu. Bariki jitihada zetu za kuendeleza ufalme Wako katika kusanyiko hili na katika jamii yetu.*

## SIKU YA 24

## MBINU YA KRISTO YA UINJILISTI

Roho ya unabii ilitupa maelezo ya wazi sana kuhusu mbinu ya Kristo ya ushuhudiaji:

"Mwokozi alichangamana na watu kama yule anayetamani mema yao. Alionyesha huruma Yake kwao, akawahudumia mahitaji yao, na akaitambua imani yao. Kisha akawaambia, 'Nifuateni Mimi'" (Huduma ya Uponyaji, uk. 143). *Angalia hiki kitabu katika MaarifaMtandaoni.Com na RohoYaUnabii.Org, au RohoYaUnabii.Africa*

Kwa kuwa hii ilikuwa mbinu ya Kristo ya ushuhudiaji, tunapopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu na Kristo anapoanza kuishi kikamilifu zaidi ndani yetu, Atajitahidi kudhihirisha mbinu hii ya ushuhudiaji kupitia sisi. Ataanza kutuongoza "kuchangamana" na wale walioko kwenye mzunguko wa familia na marafiki zetu, akiweka ndani ya mioyo yetu tamanio "la mema yao." Jema kuu zaidi ni kwao kumjua Yesu Kristo kama Mwokozi wao.

Njia ya Kristo ilikuwa ni kuchukua hatua ya kwanza ya kuwasiliana na wale walio karibu Naye. Yeye Anataka mimi na wewe tufanye vivyo hivyo. Ukiona hili ni gumu, unahitaji kuendelea kuomba BWANA akusaidie kwa hili, Naye Atakusaidia! Kumbuka, ni Yesu ndani yako anayekuchochea kufanya hili. Unapoendelea kujisalimisha chini ya uongozi Wake katika kila eneo la maisha yako, kushuhudia kwako kutazidi kufanana na mbinu Yake.

Tunapoendelea kuomba ubatizo wa Roho Mtakatifu, upendo wa MUNGU utadhihirika zaidi na zaidi ndani ya mioyo yetu:

"Na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la MUNGU limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi." (Warumi 5:5).

Upendo huu utaonekana katika huduma yetu kwa wengine. Wataanza kupata imani kwamba tunawajali kwa dhati na watakuwa tayari kushirikiana nasi mambo yanayowasumbua. Kila mtu ana majeraha, ndoto zilizovunjika, huzuni, na matatizo ambayo wanapambana nayo au hata changamoto za kifamilia. Hii ndiyo sababu hasa Kristo amekuelekeza kwao. Yeye Anajua mahitaji yao, na anajua kwamba una jibu kwao. Kristo anataka kufunua jibu hilo kupitia wewe, na kwenda kwao. Yeye Anataka kujifunua Mwenyewe kwao kupitia wewe. Roho ya unabii inanena kuhusu hili:

"Ukarimu wa Kikristo haupewi kipaumbele sana na watu wa MUNGU…. Wale ambao wameonja upendo wa Kristo haswa, wanapaswa kukuza mvuto wao wa kijamii, kwani kwa njia hii wanaweza kuleta roho kwa Mwokozi" (Testimonies for the Church, vol. 6, uk. 172).

"Kwa hivyo ni kupitia mawasiliano binafsi na ushirika, ndiyo ambapo watu wanapatikana kwa nguvu ya wokovu ya injili" (Mlima wa Baraka, uk. 36).

Haya yote yanahusianaje na Mkristo aliyejawa na Roho Mtakatifu? Kwanza, omba Kristo aendelee kukujaza na Roho Wake na kukupa hamu ndani ya moyo, kwa ajili ya roho ambazo Yeye anazo au ziko karibu na mvuto wako. Tengeneza orodha ya wale walio kwenye mzunguko wako wa familia na marafiki ambao unahisi hawamjui Kristo, au ambao wanaweza kuwa Wakristo lakini hawajui ujumbe muhimu wa kuja kwa Kristo mara ya pili. Anza kuwaombea watu hawa kila siku, ukitumia kanuni za maombi zilizoorodheshwa katika somo au ibada ya awali. Kisha, omba kwamba MUNGU akupatie fursa ya kuanza kuwakaribia ili kuwasaidia kwa namna fulani. Tunapaswa kuwa tayari kuwekeza muda na juhudi inayohitajika ili kuwasogelea watu. Shauku yetu kwao lazima iwe ya dhati, kuwajali na kutaka kuwasaidia. Unapokuwa karibu na wale unaowaombea, tafuta fursa ambazo MUNGU anakupa kushirikiana nao.

Kumbuka kila wakati kwamba MUNGU tayari anajaribu kuvuta mawazo na maslahi yao Kwake.

Katika hali mbalimbali Anahitaji tu sisi tuwe tayari ili Azungumze Neno la kutia moyo kwao. MUNGU atakupa Maneno ya kusema. Yeye Anajua wanachohitaji kusikia, na nguvu za Roho Mtakatifu zitashuhudia maneno unayosema.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Orodhesha vipengele vya mbinu ya Kristo ya ushuhudiaji.
- Kwa nini unadhani Kristo alichagua mbinu hii ya kushuhudia?
- Wakristo wanapaswa kufanya nini ikiwa hawana hamu ya kumshuhudia Kristo?
- Mkristo anapaswa kumwomba MUNGU afanye nini hasa kuhusiana na ushuhudiaji?
- Unapanga vipi kutumia mbinu ya Kristo ya ushuhudiaji?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kumbatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na kanisa Lake.
- Ili MUNGU akuongoze kushuhudia kama Kristo alivyoshuhudia kwa wengine.
- Juu ya wale walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi**

"Ndivyo litakavyokuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu; halitanirudia bure, bali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma" (Isaya 55:11).

*Bariki Neno Lako ambalo limehubiriwa na kufundishwa kwa kusanyiko hili. Na lifanye kusudi ambalo ulilituma litimie.*

# SEHEMU YA IV—UBATIZO WA ROHO NA KUKAA KATIKA KRISTO

## SIKU YA 25

## NJIA YA KUGUNDUA

Mafundisho ya kukaa ndani ya Kristo katika Biblia ni mojawapo ya Kweli muhimu zaidi ambayo Mkristo anaweza kuelewa. Kila kitu kinategemea uzoefu wa hali halisi ya kukaa ndani ya Kristo na Kristo kukaa ndani ya muumini. Hata hivyo, kila Mkristo anayegundua Ukweli huu wa utukufu wa Kristo ndani yetu amefuata njia inayofanana na wasafiri wenzao. Walikuwa wamemkubali Kristo kama Mwokozi wao lakini walikuwa na mzigo na kuchanganyikiwa na safari yao ya Kikristo iliyokuwa na upungufu wa utii na kutozaa matunda katika utumishi. Walitamani kutembea kwa uaminifu na BWANA wao kwa uthabiti, lakini hawakuipata kamwe. Walipambana na dhambi zinazowakabili, lakini dhambi hizo zilionekana kuwashinda. Waliomba na kusoma Biblia zao, lakini hilo halikuleta ushindi walioutamani. Baada ya miaka ya mapambano, walifika mahali wakakata tamaa na kuchoka. Hisia zao za kushindwa zilikuwa kubwa mno. Maisha ya ushindi wa kudumu dhidi ya dhambi yalionekana kuwa hayawezekani kufikiwa. Kisha siku moja waligundua Ukweli wa fumbo la muungano na Kristo—Kristo akiishi ndani yao. Walipogundua, walishangazwa na jinsi Ukweli huu wa ajabu ulivyokuwa rahisi, lakini uelewa wao ulikuwa umewapita kwa miaka. Baada ya kugundua hili, maisha yao hayakuwa vile tena. Furaha yao kwa BWANA ilikuwa ya kina na ya kudumu. Maisha yao sasa yalikuwa na ushindi wa kudumu, hata dhidi ya dhambi zinazowakabili. Hawakujihisi tena na mzigo au wasiwasi katika utumishi wao kwa BWANA, na utumishi wao ukawa wenye matunda zaidi.

Ukweli wa kukaa ndani ya Kristo na Yeye kukaa ndani yetu, na jinsi tunavyopaswa kuishi maisha ya Kikristo, yenye ushindi ni rahisi sana—na bado ni vigumu kueleweka—hata Wakristo wengi hawajawahi kuugundua Ukweli huu kikamilifu. Leo MUNGU anatuita kwenye uzoefu huu wa ajabu ndani ya Kristo. Kwa nini? Yesu anakuja hivi karibuni! Wale wote watakaokuwa tayari kumlaki watakuwa kama Yeye:

"Wapenzi, sasa tu wana wa MUNGU, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo." (1 Yohana 3:2).

Uzoefu wao wa kila siku utakuwa ni wa ushindi kamili ndani ya Kristo ikiwa watakuwa "kama" Yesu anaporudi:

"Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake. Yeye hakutenda dhambi, wala hila haikuonekana kinywani mwake. Yeye alipotukanwa, hakurudisha matukano; alipoteswa, hakuogofya; bali alijikabidhi kwake yeye ahukumuye kwa haki." (1 Petro 2:21-23).

Kwa hivyo, Ukweli huu mzuri wa Kibiblia si wa umuhimu mdogo kwa Wakristo wanaoishi katika siku zetu. Yesu anakuja hivi karibuni, na MUNGU anatuita kwenye uzoefu wa juu zaidi pamoja Naye kuliko tulivyowahi kuwa nao. Sehemu hii ya ibada imekuwa kwa lengo la kuwaongoza wote wanaosoma kuelewa na kupata uzoefu wa kukaa ndani ya MUNGU anaotupatia; Kristo ndani yetu, tumaini la utukufu kwa watu Wake:

"Ambao MUNGU alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu" (Wakolosai 1:27).

Ukweli huu unapoeleweka na kugunduliwa, muumini atatangaza kutoka kwenye kina cha moyo wake, "Kristo alifanya yote." Ukombozi ambao Kristo anatoa unazika ardhini majivuno yote ya kibinadamu. Mwanadamu hawezi kudai utukufu wowote kwa ushindi dhidi ya majaribu na dhambi. Utukufu wote utakwenda kwa MUNGU na utatangazwa kwenye maisha yale ya milele:

"Mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za MUNGU. Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa MUNGU, na haki, na utakatifu, na ukombozi; kusudi, kama ilivyoandikwa, Yeye aonaye fahari na aone fahari juu ya BWANA" (1 Wakorintho 1:29-31).

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Eleza njia ambavyo Wakristo wengi waliogundua Ukweli wa "Kristo ndani yangu, tumaini la utukufu," wamefuata.
- Je, kuelewa na kupata uzoefu wa Ukweli huu kutabadili vipi maisha ya Mkristo?
- Kwa nini Ukweli huu ni muhimu kwa Mkristo kuelewa na kupata uzoefu?
- Je, unatamani kwa kiasi gani kuelewa na kupata uzoefu wa Ukweli wa kukaa ndani ya Kristo na Kristo kukaa ndani yako?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kumbatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na kanisa Lake.
- Ili MUNGU afungue uelewa wenu wa Ukweli wa Kibiblia wa kukaa ndani ya Kristo.
- Ombeeni wale walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Maana, tazama, giza litaifunika dunia, Na giza kuu litazifunika kabila za watu; Bali BWANA atakuzukia wewe, Na utukufu wake utaonekana juu yako. Na mataifa wataijilia nuru yako, Na wafalme kuujia mwanga wa kuzuka kwako" (Isaya 60:2, 3).

*Tutoe kwenye giza letu la kiroho. BWANA, amka kati yetu na ufunue utukufu wa tabia Yako kupitia sisi. Vuta wengi katika jamii yetu kwenye nuru ya Ukweli uliotupa.*

## SIKU YA 26

## MAPAMBANO YA MKRISTO

Niliita ibada ya leo, "Mapambano ya Mkristo," kwa sababu asiyeamini hana mapambano ambayo Mkristo anayapitia. Mtu ambaye hajamwamini Kristo hana Roho wa MUNGU na anaongozwa tu na akili zake za kimwili. Kulingana na Paulo, akili ya kimwili ni "uadui dhidi ya MUNGU: kwa maana haitii sheria ya MUNGU, wala haiwezi kuitii." (Warumi 8:7). Mtu asiye Mkristo haitii sheria kwa sababu MUNGU ameweka ndani ya moyo wake kufanya hivyo. Anatii kwa sababu binafsi, ubinafsi, au shinikizo la kijamii, nk. Au labda alilelewa katika nyumba yenye maadili na ana dhamiri inayomwongoza kuishi maisha ya heshima.

Kwa upande mwingine, Mkristo anamtii MUNGU kwa sababu Roho wa MUNGU ameweka ndani ya moyo wake hamu ya kutii: "Lakini MUNGU na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake" (Warumi 6:17).

Mtu aliyezaliwa upya anatamani sana kutimiza mapenzi ya MUNGU katika maisha yake. Paulo anaita hii kufurahia "Sheria ya MUNGU kwa utu wa ndani" (Warumi 7:22). Chini ya ahadi ya Agano Jipya, Roho Mtakatifu huanza kuandika sheria ya MUNGU katika moyo na akili yake: "Maana, awalaumupo, asema Angalia, siku zinakuja, asema BWANA, Nami nitawatimizia nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda agano jipya; Halitakuwa kama agano lile nililoagana na baba zao, Katika siku ile nilipowashika mikono yao niwatoe katika nchi ya Misri. Kwa sababu hawakudumu katika agano langu, Mimi nami sikuwajali asema BWANA. Maana hili ndilo agano nitakaloagana na nyumba ya Israeli Baada ya siku zile, asema BWANA; Nitawapa sheria zangu katika nia zao, Na katika mioyo yao nitaziandika; Nami nitakuwa MUNGU kwao, Nao watakuwa watu wangu." (Waebrania 8:8-10).

"Mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tuliyoikatibu, iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa MUNGU aliye hai; si katika vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama." (2 Wakorintho 3:3).

Hata hivyo, mwamini mpya hugundua haraka kwamba kuna tamaa au hamu nyingine yenye nguvu ndani yake—hamu ya dhambi. Sasa kwa kuwa ana Roho wa MUNGU, anafahamu tamaa zake za dhambi, wakati kabla ya hapo, tamaa hizo hazikumteka sana. Hivyo Mkristo hugundua kwamba sasa kuna asili mbili ndani yake: moja inayotamani kufuata dhambi, na nyingine inayotamani kumtii MUNGU. Paulo anaelezea kwa uwazi mgongano huu mkali, unaopitiwa na kila Mkristo, katika Warumi 7:14-25:

“Kwa maana twajua ya kuwa torati asili yake ni ya rohoni; bali mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi. Maana sijui nifanyalo, kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda. Lakini kama nikilitenda lile nisilolipenda, naikiri ile sheria ya kuwa ni njema. Basi sasa si mimi nafsi yangu ninayetenda hilo, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu. Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu, halikai neno jema; kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo jema sipati. Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo. Basi kama lile nisilolipenda ndilo nilitendalo, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu. Basi nimeona sheria hii, ya kuwa kwangu mimi nitakaye kutenda lililo jema, lipo lililo baya. Kwa maana naifurahia sheria ya MUNGU kwa utu wa ndani, lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kunifanya mateka ya ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu. Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? Namshukuru MUNGU, kwa Yesu Kristo BWANA wetu. Basi, kama ni hivyo, mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya MUNGU, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi.”

Kila Mkristo anaweza kuwa na sifa ya mapambano ambayo Paulo anaelezea. Wakristo mara nyingi hupitia mapambano haya siku baada ya siku, mwezi baada ya mwezi, na mwaka baada ya mwaka, na hawapati ushindi wanaotaka juu ya dhambi. Kila Mkristo anafahamu vyema kwamba kuna “sheria ya dhambi” inayokaa ndani yao ambayo inapingana na shauku itolewayo na MUNGU kutii sheria Yake. Kama Paulo anavyosema, alifurahia sheria ya MUNGU. Alitamani sana kumtii MUNGU katika mambo yote; hata hivyo, aliona kuwa haiwezekani kwake kufanya hivyo. Asili yake ya dhambi kila wakati ilitafuta kumfanya kuwa mtumwa wa sheria ya dhambi.

Kutambua ugumu wa kumtii MUNGU kwa sababu ya nguvu ya dhambi katika maisha yake, Paulo analia, “Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?” Kisha anatangaza kwamba ukombozi kutoka kwa sheria ya dhambi unaweza kutokea “kwa njia ya Yesu Kristo BWANA wetu” (Warumi 7:24, 25).

Katika Warumi 8:1-4, Paulo anatoa suluhisho la tatizo hili katika maisha ya muumini: “Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, MUNGU, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya

dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili; ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho."

Suluhisho la tatizo la Mkristo ni kumruhusu Kristo Yesu, kupitia sheria ya Roho ya uzima, kutuweka huru dhidi ya sheria ya dhambi na mauti. Kwa maneno mengine, tunapaswa kumruhusu Yesu kuishi maisha Yake ndani yetu kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hii ndiyo Paulo anayoita "kuenenda katika Roho." Anafafanua zaidi juu ya hili katika waraka wake kwa Wagalatia: "Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka. (Wagalatia 5:16, 17).

Paulo anatuambia kwamba haki ya sheria itatimizwa "ndani yetu" tunapokuwa na Yesu akiishi ndani yetu kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu: "ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho." (Warumi 8:4).

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Ni tofauti gani kati ya mtazamo wa kweli wa Mkristo na yule asiye Mkristo kuelekea dhambi?
- Paulo anaelezaje mapambano ya Mkristo na dhambi?
- Paulo anasema nini kuhusu suluhisho la mapambano ya Mkristo na dhambi?
- Umekuwa na uzoefu gani na mapambano yako binafsi na dhambi?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza ninyi wote kwa Roho Wake Mtakatifu
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na kanisa Lake.
- Ili MUNGU akuongoze kuishi Kweli ndani ya Kristo kwa ushindi dhidi ya dhambi.
- Kwa ajili ya watu walio kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"MUNGU wa BWANA wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye; macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo; na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu

tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake" (Waefeso 1:17-19).

*Tupe hekima na ufahamu tunaouhitaji ili kukupenda na kukuthamini Wewe kikamilifu. Fungua macho yetu ili tuone dhambi zetu na ukuu wa rehema Yako na msamaha Wako. Tuelekeze kuelewa tumaini la ajabu tulilo nalo ndani ya Yesu. Fungua macho yetu ili tuone na kuamini katika nguvu Yako kuu inayopatikana kwetu ili kushinda lolote ambalo Shetani analeta maishani mwetu. Kwa nguvu Zako, turejeshe Kwako na tuamshe.*

## SIKU YA 27

## UWEZO WA DHAMBI KUVUNJWA

Kuna mambo mengi kuhusu habari njema ya injili ya Yesu Kristo. Moja ni kwamba pale msalabani, nguvu ya asili ya dhambi ilivunjwa kwa wale wote wanaomkubali Kristo na kuamini: "Mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena" (Warumi 6:6). "Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa MUNGU katika Kristo Yesu." (aya ya 11).

Yesu alipokufa msalabani, nguvu ya asili ya dhambi katika maisha ya kila muumini ilivunjwa. Hili ni tukio la kihistoria. Hata hivyo, linakuwa halisi katika maisha ya Mkristo ikiwa tu anaamini hilo.

Hii inamaanisha kuwa wewe usiyependa, usiyesamehe, mwenye hasira, mwenye tamaa, mwenye wasiwasi—na mengine mengi—ulikufa msalabani. Hiyo ni habari njema! Inamaanisha kuwa hauhitaji kudhibitiwa na mitazamo yako isiyopendeza, kutosamehe, hasira, mawazo na tamaa mbaya, n.k. Nguvu ya tamaa hizi za dhambi, na melekeo na mienendo, imevunjwa.

Tatizo ambalo Wakristo wengi hukutana nalo wanaposoma Aya hizi za Biblia ni kwamba wanahitimisha kuwa wanapaswa sasa kuwa na uwezo wa kumtii MUNGU kwa msaada Wake. Kwa mfano, fikiria Mkristo ambaye ana tatizo la hasira. Anafikiria kuwa ikiwa nguvu ya hasira yake ya dhambi ilivunjwa msalabani, sasa anaweza kuacha kuwa na hasira pale kitu kinapotokea chenye kumsababishia hasira. Anahisi faraja kubwa, akiwa na uhakika kuwa sasa hatimaye atapata ushindi.

Muda mfupi baadaye kitu kinatokea na kumsababisha kuudhika tena. Pengine mtu anamwingilia kwenye foleni, au mtu anasema kitu kibaya kwake. Mara moja hasira inampanda. Anajitahidi kuikandamiza hasira, lakini anagundua kuwa inazidi kuendelea. Hapendi hisia hizi, lakini anaonekana kuwa hana uwezo wa kuziacha. Anaanza kujiuliza kwa nini hasira bado inatokea kwenye hisia zake. Anahitimisha kuwa labda hakuomba au kupokea kutoka kwa MUNGU nguvu za kutosha kumsaidia katika jitihada zake za kuishinda hasira. Kwa hiyo, anaomba MUNGU aondoe hasira, ampe nguvu anazohitaji, ampe ushindi. Hata hivyo, anaendelea kukutana na mzunguko uleule wa kushindwa na dhambi zake zinazomkwaza. Mkanganyiko zaidi na hisia za kushindwa zinaingia. Tena, anatilia shaka kujitoa kwake kuacha hasira na hana amani katika kutembea kwake na BWANA.

Ni kweli kabisa kwamba nguvu ya asili yetu ya dhambi ilivunjwa msalabani. Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa ikiwa sasa tunaamini hili tunaweza kuanza kumtii MUNGU kwa kuweka juhudi za kufanya hivyo. Kumbuka, hatuna uwezo ndani yetu wenyewe wa kumtii MUNGU, ingawa mvuto mkubwa wa asili yetu ya dhambi ulivunjwa msalabani. Kujua na kuamini ukweli huo hakutoshi. Hapana. Kuna njia moja tu tutakayopata ushindi tunaoutamani. Ushindi dhidi ya majaribu na dhambi utafanyika katika maisha yetu ikiwa tu tutaamini Ukweli wa kusulibiwa kwa asili yetu ya dhambi na pia kumruhusu Kristo atupatie ushindi Wake. Ni lazima tuelewe kuwa tutakuwa na ushindi dhidi ya dhambi na majaribu ikiwa tu tutamruhusu Yeye aishi maisha Yake ya ushindi ndani yetu: "Kwa maana, wakiwa hawaijui haki ya MUNGU, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya MUNGU. Kwa maana Kristo ni mwisho wa sheria, ili kila aaminiye ahesabiwe haki" (Warumi 10:3, 4).

"Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida." (Wafilipi 1:21).

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Nini kilitokea kwa nguvu ya asili ya dhambi ya Mkristo msalabani?
- Ikiwa mtu anajua na kuamini Ukweli huu, je, inamaanisha kwamba sasa anaweza kuanza kumtii MUNGU kwa usahihi? Kwa nini ndiyo, au kwa nini hapana?
- Ni kitu gani kingine Mkristo anapaswa kuamini ili kushinda dhambi kwa usahihi?
- Je, umewahi kujaribiwa kuamini kuwa wewe si Mkristo kweli kwa sababu ya tatizo la dhambi maishani mwako?
- Je, umewahi kumwomba MUNGU aondoe dhambi fulani maishani mwako, lakini alionekana kama hakusikia au hakujibu, na bado unaendelea kupambana na hiyo dhambi?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasilian Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na kanisa Lake. o Ili MUNGU akufunulie jinsi unavyopaswa kumruhusu Yesu aishi maisha Yake ya ushindi ndani yako na kupitia wewe.
- Kwa ajili ya watu walio kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

“(MUNGU) Awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani. Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa MUNGU.” (Waefeso 3:16-19).

*Tujaze kwa Roho Wako. Tutiwe nguvu kwa uwezo wa Roho Wako ili tuweze kusimama dhidi ya mashambulio yote ya adui. Tujaze kwa upendo Wako na utufungulie macho yetu kuelewa upendo wa Kristo ili tuthibitishe upendo wa Kristo kwa wengine kwa maneno yetu na matendo yetu.*

## SIKU YA 28

## KRISTO ANATOA USHINDI

Mpaka Mkristo atakapokuja kuelewa na kupata uzoefu wa kile kinachomaanisha kumruhusu Kristo ampe ushindi Wake, hatapata maisha ya utii thabiti anayoyatamani. Katika ibada ya leo, nitawasilisha jinsi ya kumruhusu Kristo aishi maisha Yake ya ushindi ndani yako. Unapokuja kuelewa na kupata uzoefu wa Ukweli huu, maisha yako ya Kikristo hayatakuwa tena kama ya zamani. Badala ya maisha ya utii wa kusuasua na ahadi zilizovunjika kwa MUNGU, utapata, kwa muda, maisha ya ushindi kupitia Kristo juu ya kila jaribu na dhambi ambayo Shetani anakuletea.

Je, maisha ya utii thabiti kama haya yanawezekana kweli? Je, tunaweza kweli kuwa na ushindi juu ya kila jaribu na dhambi katika maisha yetu? Hilo ndiyo aina ya maisha ambayo MUNGU anatuita kuishi: "mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena" (Warumi 6:6). "Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa MUNGU katika Kristo Yesu. Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake; wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa MUNGU kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa MUNGU kuwa silaha za haki. Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema." (Warumi 6:11-14).

Roho ya unabii inakubaliana na haya:

"Yeye asiye na imani ya kutosha kwa Kristo kuamini kwamba Aweza kumkinga asiwe na dhambi, hana imani itakayompatia kuingia katika ufalme wa MUNGU" (Manuscript 161, 1897, p. 9).

Kwa hiyo, jibu la jinsi tunavyoweza kuishi maisha ya Kikristo ya ushindi thabiti, ni lipi? Jibu ni kumruhusu Yesu aishi maisha Yake ya ushindi ndani yetu, Ukweli ambao umefundishwa kote katika Biblia: "Nimemweka BWANA mbele yangu daima, Kwa kuwa yuko kuumeni kwangu, sitaondoshwa." (Zaburi 16:8). "Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini. Mtumainini BWANA siku zote Maana BWANA YEHOVA ni mwamba wa milele." (Isaya 26:3, 4). "Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi,

akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.” (Yohana 15:4, 5).

Akili ya Kristo ilikuwa imejaa mawazo safi, matakatifu, na yenye wema. Ikiwa tumemwomba Kristo aishi ndani yetu kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu, na tukiamini, Atafanya hivyo, na tukiamini Atadhihirisha upendo Wake—mawazo

Yake safi, matakatifu, na yenye wema ndani ya akili zetu—Atafanya hivyo. Hili ni suala la imani; kuamini kwamba Atajidhihirisha kweli Yeye Mwenyewe katika maisha yetu. Paulo alitambua Ukweli huu aliposema: “Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa MUNGU, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.” (Wagalatia 2:20). “zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la MUNGU;” (Waefeso 6:16, 17).

Ili kupata uzoefu wa kukaa kweli ndani ya Kristo, ni lazima utambue kwamba Yesu anakaa ndani yako kwa maana halisi. Alisema kwamba Anakaa, na unaweza kumwamini. Hili hutokea unapoendelea kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu kila siku:

“Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu. Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu.” (Yohana 14:16-18). “Naye azishikaye amri zake hukaa ndani yake yeye naye ndani yake. Na katika hili tunajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa.” (1 Yohana 3:24).

Kwa Yesu kuishi ndani yako, unayo akili Yake: “Maana, Ni nani aliyeifahamu nia ya BWANA, amwelimishe? Lakini sisi tunayo nia ya Kristo.” (1 Wakorintho 2:16).

Tunao upendo Wake, furaha, amani, subira, upole, wema, imani, unyenyekevu, kiasi—matunda yote ya Roho: “Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.” (Wagalatia 5:22, 23).

Kupitia Yesu kuishi ndani yetu kwa njia ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, tunayo yale ayapendayo na asiyoyapenda, mawazo Yake safi, na msamaha Wake— na mengine mengi. Kila sifa ya Kristo ipo ndani yako kupitia Kristo kukaa ndani yako.

Mkristo atautumiaje Ukweli huu? Kwa ufupi, hatua ni hizi. Unapogundua jaribu la dhambi:

- Chagua kugeuza akili yako mara moja kutoka kwenye jaribu:
  “Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo.” (Wafilipi 4:8).
- Amini kwamba nguvu ya asili yako ya dhambi ya kuvutwa kwenye jaribu ili kukutawala imevunjwa.
- Amini Yesu Yuko ndani yako, na mwombe Adhihirishe sifa Yake ndani yako kwa kuhusiana na jaribu hilo. Ubainishe jambo kabisa.
- Amini kwamba Atadhihirisha mwenyewe kwa namna hiyo, pumzika katika imani hiyo, na usipigane na jaribu hilo. Tunapopigana na jaribu, kwa kweli tunalizingatia kwa umakini sana na kujaribu kulipinga kwa nguvu zetu badala ya kumwangalia Yesu kwa ushindi:

“Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha MUNGU.” (Waebrania 12:1, 2).

- Mshukuru kwa ukombozi Aliokupa.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Kulingana na Biblia na RYU, je, maisha ya utii thabiti yanawezekana?
- Biblia inafundisha nini kuhusu Yesu kuishi ndani ya Mkristo? Toa maandiko ya Biblia.
- Faida za kuwa na Kristo aishiye ndani yako ni zipi?
- Hatua za kumruhusu Yesu akupatie ushindi juu ya jaribu ni zipi?
- Unapanga kutumia vipi mafundisho haya katika maisha yako binafsi?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili Kwa MUNGU aendelee kubatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu. Ili MUNGU alete ufufuo katika maisha yako na kanisa Lake.
- Ili MUNGU akuongoze kumruhusu Yesu kuishi maisha ya ushindi ndani yako unapojaribiwa.
- Kwa ajili ya watu walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako:**

“Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu” (Waefeso 3:20).

*Fungua akili zetu ili tusikie nguvu Zako za kutuokoa kutoka kwenye dhambi, kutuamsha mmoja mmoja na kama kanisa, ili tueneze injili katika jamii yetu. Tupe imani kwamba nguvu kubwa zaidi katika ulimwengu huu inaishi ndani yetu kupitia Roho Wako Mtakatifu.*

## SIKU YA 29

## HAKI KWA IMANI

Haki kwa imani ni kumtazama Yesu aonyeshe maisha Yake ya haki na ushindi katika maisha yetu. MUNGU anataka tumwangalie Kristo kwaajili ya ushindi, si kwetu wenyewe:

“Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha MUNGU.” (Waebrania 12:1, 2).

Hii ni haki ya Kweli kwa njia ya imani na ndiyo mapenzi ya MUNGU kwa kila Mkristo. Oswald Chambers, mwandishi maarufu wa Kikristo, alieleza kweli huu wa ajabu katika Kesha yake ya tarehe 23, Julai kutoka katika Jarida lake la kila siku, *My Utmost for His Highest*:

“Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa MUNGU, na haki, na utakatifu, na ukombozi” (1 Wakorintho 1:30).

“Upande wa Maisha: Siri ya utakaso ni kwamba sifa kamili za Yesu Kristo zinatolewa kama zawadi kwangu, si polepole, bali mara moja ninapoingia kwa imani katika ufahamu kwamba Yeye Alikuwa kwetu... utakaso.…Utakaso unamaanisha hakuna kingine ila utakatifu wa Yesu kuwa wangu na kuonyeshwa katika maisha yangu.

“Siri ya ajabu ya kuishi maisha matakatifu haiko katika kumwiga Yesu, bali katika kuruhusu sifa kamili za Yesu kudhihirika katika mwili wangu wa uanadamu. Utakaso ni ‘Kristo ndani yako...’ (Wakolosai 1:27). Ni maisha Yake ya ajabu yanayoletwa kwangu katika utakaso—yanayoletwa kwa imani kama zawadi ya neema ya MUNGU. Je, niko tayari kwa MUNGU kufanya utakaso kuwa halisi kwangu kama ilivyo katika Neno Lake?

“Utakaso unamaanisha utoaji wa sifa takatifu za Yesu Kristo kwangu. Ni zawadi ya uvumilivu Wake, upendo, utakatifu, imani, usafi, na Uungu Wakae vinavyoonyeshwa ndani na kupitia kila roho iliyotakaswa. Utakaso si kupata nguvu kutoka kwa Yesu na kuwa mtakatifu—bali ni kupata utakatifu wenyewe

uliyoonyeshwa ndani Yake, na sasa ni Yeye Anavyoonyesha ndani yangu. Utakaso ni utoaji, si uigaji. Uigaji ni kitu kingine kabisa. Ukamilifu wa kila kitu upo ndani ya Yesu Kristo, na siri ya utakaso ni kwamba sifa zote kamili za Yesu ziko mikononi mwangu. Kwa hiyo, polepole lakini hakika ninaanza kuishi maisha ya mpangilio wa ajabu, ustahimilivu, na utakatifu—'.….nikiwa chini ya nguvu za MUNGU...' (1 Petro 1:5)."

Je, unaona uzuri wa Ukweli huu? Sehemu yetu ni kutamzama Yesu kwa imani inayotegemea, ikiamini ahadi ya MUNGU kuonyesha Kristo na haki Yake ndani yetu. Sehemu yetu pekee ni kuchagua kuruhusu hili litokee na kuamini kuwa litafanyika. Wakati tamaa za kutojua haki na majaribu yanapokuja, hatupigani dhidi ya hizo. Tunapaswa kuelekeza macho kwa Kristo anayekaa ndani yetu na kumuomba aonyeshe haki Yake Mwenyewe (Waebrania 12:1, 2). Kisha tunasubiri kwa imani tukiamini Atafanya hivyo.

Wakati Kristo anapoonekana kikamilifu ndani ya watu Wake basi dunia itakuwa na mwangaza wa utukufu Wake au tabia: "Na baada ya hayo naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu Wake." (Ufunuo 18:1).

Basi watu Wake watakuwa kama Yesu: "Wapenzi, sasa sisi tu watoto wa MUNGU, na hatujaonekana tutakavyokuwa; lakini tunajua kwamba, atakapodhihirishwa ndani yetu, tutakuwa kama Yeye; kwa maana tutamwona kama alivyo" (1 Yohana 3:2).

Wakati Ataporudi tutakuwa na uwezo wa kusimama mbele za Kristo katika utukufu Wake wote na tusiangamizwe. Hii ndiyo ahadi ya MUNGU kwa watoto Wake, na itatimizwa tunavyojifunza kumtazama Yesu kwa imani kwa udhihirisho huu wa ajabu wa Yeye kuwa ndani yetu: "Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu;" (Yuda 24).

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Kulingana na tafakari ya leo, mapenzi ya MUNGU kwa kila Mkristo ni yapi?
  - Mapenzi ya MUNGU kwa kila Mkristo ni kuishi kwa haki kwa imani kwa kutazamia Yesu kuonyesha maisha Yake ya haki ndani yetu. Ni kwamba Kila mtu aje kwenye wokovu.
- Haki ya kweli kwa imani ni nini?
- Haki ya kweli kwa imani ni kutazamia Yesu kuonyesha maisha Yake ya haki na ushindi katika maisha yetu kupitia imani yetu kwa MUNGU.
- Eleza kwa maneno yako mwenyewe kile alichosema Oswald Chambers.

- Unapanga kutumia haki kwa imani vipi katika maisha yako binafsi?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kubatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete ufufuo katika maisha yako na kanisa Lake.
- Ili MUNGU akuongoze na kumruhusu Yesu kujidhihirisha kikamilifu katika maisha yako ili upate uzoefu wa haki kwa imani kwa Kristo peke yake.
- Kwa ajili ya watu walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Kwa maana nitamimina maji juu yake aliye na kiu, na vijito vya maji juu ya mahali pakavu; nitamwaga roho yangu juu ya wazao wako, na baraka yangu juu yao utakaowazaa; nao watatokea katika manyasi, kama mierebi karibu na mifereji ya maji." (Isaya 44:3, 4).

*Sisi ni kama nchi kavu kiroho—mimina Roho Yako juu yetu na tufanye tuishi tena na kukua katika ukamilifu wa Kristo.*

# SIKU YA 30

## AMRI ZA MUNGU NA KUKAA KATIKA KRISTO

Utii kwa amri za MUNGU na kukaa katika Kristo ni mambo mawili yasiyoweza kutenganishwa. Huwezi kuwa na moja bila jingine. Yesu alisema: "9 Kama vile Baba alivyonipenda Mimi, Nami nilivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo Langu. 10 Mkizishika amri Zangu, mtakaa katika pendo Langu; kama vile Mimi nilivyozishika amri za Baba Yangu na kukaa katika pendo Lake.

"Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake." (Yohana 15:10).

Yesu, Roho Mtakatifu, na sheria za MUNGU ni vitu visivyoweza kutenganishwa. Tunapokaa katika Kristo na Yeye anapokaa ndani yetu, Amri Kumi zitakuwa sehemu muhimu ya maisha yetu kwa sababu Roho Mtakatifu atakuwa akiandika haya Maagizo muhimu ya MUNGU kwenye mioyo yetu:

"Mnadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tuliyoikatibu, iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa MUNGU aliye hai; si katika vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama." (2 Wakorintho 3:3).

Kwa kweli, ilikuwa Yesu ambaye, kabla ya kuzaliwa katika mwili yaani Emmanueli, alimpa Musa Amri Kumi. MUNGU ambaye alitoa amri hizo alijifunua kwa Musa kama "MIMI NIKO Ambaye Niko: "MUNGU akamwambia Musa, MIMI NIKO AMBAYE NIKO; akasema, Ndivyo utakavyowaambia wana wa Israeli; MIMI NIKO amenituma kwenu." (Kutoka 3:14).

Yesu alidai kuwa Yeye Ndiye 'MIMI NIKO' wa Agano la Kale: "Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambia, Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." (Yohana 8:58).

Katika nyaraka za Paulo tunapata maelekezo mengi kuhusu mitazamo na tabia ambazo BWANA anataka tuonyeshe katika maisha yetu. Paulo anatoa maelekezo wazi kuhusu tabia:

"mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya MUNGU katika haki na utakatifu wa kweli. Basi uvueni uongo, mkaseme kweli kila mtu na jirani yake; kwa maana tu viungo, kila mmoja kiungo cha wenzake. Mwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka; wala msimpe Ibilisi nafasi. Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa

mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji. Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia. Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa MUNGU; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi. Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na MUNGU katika Kristo alivyowasamehe ninyi." (Waefeso 4:22-32).

Kwa nini Biblia inatumia nafasi kubwa kutufundisha tabia ambazo MUNGU anataka tufuate? Kwa sababu ni tunahitaji kujua mitazamo na tabia ambazo anataka tuwe nazo ili tuweze kuwa na ufahamu wa hali tunapojaribiwa kuwa na tabia mbaya. Ikiwa hatujajua mapenzi ya MUNGU katika maeneo haya, hatutachagua kumruhusu Kristo kuonyesha kipande hicho cha tabia Yake ndani yetu. Kwa mfano, kama muumini hajui kuwa ni makosa kushikilia ghadhabu na kusema kitu cha kukosoa wakati mtu anapomkosea, hatageuza mawazo yake mbali na ghadhabu na roho ya ukosoaji anayoanza kuhisi. Hatamchagua Kristo kuonyesha "kutokuwa na ghadhabu" na "roho isiyo na ukosoaji" katika hali hiyo kwa sababu hajui kwamba ghadhabu na roho ya ukosoaji ni makosa. Na hivyo, hataakisi tabia ya Kristo katika hali hiyo bainishi. Atakuwa hajaanza kukuza na kuendeleza tabia ya Kristo ndani yake katika eneo hilo la maisha yake.

Pale Kristo anapokaa ndani yetu, atajitahidi kuishi maisha yake ndani yetu na kupitia sisi. Hii ina maana kwamba atajitahidi kuishi Amri Kumi katika maisha yetu kama vile alivyofanya alipokuwa duniani: "Kuyafanya mapenzi yako, Ee MUNGU wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu." (Zaburi 40:8).

Amri Kumi zinahusiana kwa karibu na upendo. Yesu alifanya hii kuwa wazi alipofundisha:

"Na tazama, mtu mmoja akamwendea akamwambia, Mwalimu, nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele? Akamwambia Kwani kuniuliza habari ya wema? Aliye mwema ni mmoja. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri. Akamwambia, Zipi? Yesu akasema, Ni hizi, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo, Waheshimu baba yako na mama yako, na, Mpende jirani yako kama nafsi yako?" (Mathayo 19:16-19).

"Mmoja wao, mwana-sheria, akamwuliza, akimjaribu; Mwalimu, katika torati ni amri ipi iliyo kuu? Akamwambia, Mpende BWANA MUNGU wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako

kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii." (Mathayo 22:35-40).

Mtume Paulo alifundisha kwamba upendo na Amri Kumi za MUNGU zinahusu uzoefu mmoja katika maisha ya mtu:

"Msiwiwe na mtu cho chote, isipokuwa kupendana; kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria. Maana kule kusema, Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani; na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria." (Warumi 13:8-10).

Amri nne za kwanza zinaonyesha jinsi tunavyopaswa kumpenda MUNGU, na sita zilizobaki zinatuambia jinsi tunavyopaswa kupendana. Hivyo, Kristo akiwa ndani yetu, Amri Kumi, upendo, na kumjua Yesu kwa karibu vyote vinahusiana kwa karibu. Huwezi kuwa na moja bila nyingine. Yohana aliandika kuhusu uhusiano huu wa karibu katika barua yake ya kwanza:

"Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake. Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa MUNGU umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake. Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda." (1 Yohana 2:3-6).

Yohana anaunganisha waziwazi kumjua Yesu kwa karibu, Amri Kumi, upendo, na kukaa ndani Yake. Anasema kwamba ikiwa tunakaa katika Kristo, tutakuwa "tukitembea," au kuishi, kama Yeye alivyoishi. Kwa nini? Kwa sababu Yesu atakuwa akiishi maisha yake ndani yetu, na maisha yetu yatakuwa maisha ya utii kwa Amri Kumi za MUNGU.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Je, Yesu alihusianaje kukaa ndani Yake na Amri Kumi?
- Je, Yesu alihusianaje upendo na Amri Kumi?
- Je, Nani alitoa Amri Kumi katika Mlima Sinai?
- Je, MUNGU anaandika Amri Kumi wapi leo, na kwa njia ipi?
- Je, Unapanga vipi kutumia somo hili la tafakari katika maisha yako wiki hii?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uvuvio katika maisha yenu na kanisa Lake.
- Ili MUNGU aandike Amri Kumi kwenye mioyo yenu, na kuwasaidia kuruhusu Yesu kuishi utii wake kwa Amri Kumi katika maisha yenu.
- Kwa ajili ya watu walio kwenye orodha ya maombi yenu.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

“Wakati umewadia BWANA atende kazi; Kwa kuwa wameitangua sheria yako.” (Zaburi 119:126).

*Ondoa kuvunja sheria kwetu—tujalie moyo wa utii.*

## SIKU YA 31

## KUISHI NDANI YA KRISTO NA UTUMISHI

Utumishi kwa BWANA wakati mwingine waweza kuwa mzigo mzito, ikiwa umejaa wasiwasi na msongo wa mawazo, kabla ya Mkristo kuelewa na kuishi hali halisi ya kuishi ndani ya Kristo na Kristo kuishi ndani yake. Hata hivyo, mara tu siri ya umoja na Kristo inapokuwa dhahiri, kila kitu kinabadilika. Utumishi kwa BWANA unakuwa furaha, na wasiwasi na mizigo huondolewa.

RYU inaandika kuhusu amani kuu aliyo nayo Yesu alipokuwa akihudumia duniani. Akiandika kuhusu majibu Yake wakati wa dhoruba iliyotishia wanafunzi wake na Yeye, aliandika:

“Yesu alipoamshwa ili kukabiliana na dhoruba, alikuwa katika amani kamilifu. Hakukuwa na chembe ya hofu katika neno au mwonekano, kwani hakukuwa na hofu moyoni Mwake. Lakini hakupumzika katika mamlaka ya uweza wa mbinguni. Hakuwa kama “BWANA wa nchi na bahari na anga” pale alipopumzika kwa utulivu. Uweza huo alikuwa ameuvua, na asema “Mimi siwezi kufanya neno Mwenyewe” Yohana 5:30. Aliamini nguvu za Baba. Ilikuwa ni kwa imani—imani katika upendo na uangalizi wa MUNGU—ndivyo Yesu alivyotulia, na nguvu ya Neno hilo lililotuliza dhoruba lilikuwa nguvu ya MUNGU…

“Vile Yesu alivyopumzika kwa imani katika uangalizi wa Baba, vivyo hivyo nasi tunapaswa kupumzika katika utunzaji wa Mwokozi wetu. Kama wanafunzi wangemwamini, wangehifadhiwa katika amani. Hofu yao wakati wa hatari ilifunua kutokuamini kwao. Katika juhudi zao za kujiokoa, walimsahau Yesu; na ilikuwa tu wakati walipokata tamaa kujitegemea, na walipomgeukia ndipo walipoweza kupata msaada, “mapenzi yangu Mimi, bali mapenzi Yake aliyenipeleka.” Yohana 5:30. Masihi Alimtegemea Baba kwa nguvu. Ilikuwa kwa imani— imani katika upendo wa MUNGU na utumishi—ndiyo Yesu alipokuwa amepumzikia, na nguvu ya Neno hilo lililokomesha dhoruba ilikuwa nguvu ya MUNGU” (The Desire of Ages, uk. 336).

Kristo Anaendelea kutuvuta leo kumwamini BWANA wetu kwa njia ile ile:

……Kama Yesu alivyokuwa akipumzika kwa imani katika uangalizi wa Baba, ndivyo tunavyopaswa kupumzika katika huduma ya Mwokozi wetu. Ikiwa wanafunzi wangeamini Yeye, wangeweza kutunzwa kwa amani. Hofu yao wakati wa hatari ilionyesha kutokuamini kwao. Katika juhudi zao za kujiokoa, walimsahau Yesu; na ni wakati walipokuwa wamekata tamaa kwa kujitegemea wenyewe, ndipo walipogeuka Kwake ndiyo kwamba aliweza kuwasaidia.

….Ni mara ngapi uzoefu wa wanafunzi umekuwa wetu! Wakati dhoruba za majaribu zinapokusanyika, na radi kali zinapong'aa angani, na mawimbi yanapotupepeta, na tunaendelea kupigana na dhoruba peke yetu, tukisahau kuwa kuna Mmoja anayeweza kutusaidia. Tunategemea nguvu zetu sisi wenyewe hadi tumaini letu litakapopotea, na tunakuwa tayari kuangamia. Kisha hapo ndiyo tunamkumbuka Yesu, na hakika ikiwa tutamwita atuokoe, hatutalia bure…. Iwe tupo ufukoni au baharini, ikiwa tunaye Mwokozi mioyoni mwetu, hakuna haja ya hofu. Imani hai katika Mwokozi itatuliza dhoruba za maisha, na itatuokoa kutoka hatarini kwa njia anayoijua BWANA kuwa ndiyo bora.

Tunapokuwa tunakua ndani ya Kristo na Yeye akiishi ndani yetu, uwepo Wake utakuwa Ukweli. Kupumzika Kwetu ndani Yake kutakuwa halisi, si nadharia tu, bali thabiti. Hofu zote, wasiwasi, na msongo wa mawazo katika utumishi au maisha zitakwisha. Mizigo ya huduma itapunguzwa, ikichukua nafasi ya kupumzika kwetu katika uwepo wa Yesu. Lazima tukate tamaa kujitegemea wenyewe na kumgeukia Kristo.

Tunapokuwa tunakulia ndani ya Kristo, tutakuwa na uhusiano na Yeye kama alivyokuwa na Baba Yake, ambao ulimsaidia kupumzika katika uhakika kwamba Baba Yake angezungumza na kuhudumukupitia Yeye.

"Je, huamini kwamba Mimi Nipo ndani ya Baba, na Baba Yupo ndani Yangu? Maneno ninayoyasema kwenu siyasemi kwa nafsi Yangu Mwenyewe: bali Baba aishiye ndani Yangu, Ndiye anayefanya matendo" (Yohana 14:10).

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Ikiwa unahisi hofu au msongo wa mawazo katika utumishi wako kwa BWANA, hilo linamaanisha nini kuhusu wewe?
- Je, ilikuwa sahihi kwa wanafunzi kuwa na hofu walipokuwa katika mashua kwenye dhoruba?
- Kwa nini, au kwa nini hapana?
- Je, unajibu vipi mara unapokumbana na mitihani, majaribu, na shida katika maisha yako?
- Je, MUNGU anataka ujibu vipi katika hali ngumu na za majaribu?
- Je, unapanga vipi kutumia somo la tafakari hii katika maisha yako wiki hii?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Omba pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho na matengenezo katika maisha yako na katika kanisa Lake.
- Ili MUNGU akukumbushe kumtazama kwa Yesu na kumtegemea wakati fursa ijayo ya kumtumikia Kristo au jaribu litaingia katika maisha yako.
- Kwa ajili ya watu walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

“Onjeni mwone ya kuwa BWANA yu mwema; Heri mtu yule anayemtumaini.” (Zaburi 34:8).

*Tupe imani Kwako, BWANA, na si katika vitu vya kidunia, kisha utubariki kwa wingi.*

# SIKU YA 32

# MAPUMZIKO YA SABATO

Habari njema inafundishwa katika kisa cha Uumbaji. Katika Mwanzo tunasoma: "Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote. Na siku ya saba MUNGU alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya." (Mwa. 2:1, 2).

Hapa tunagundua kwamba MUNGU alifanya kazi, kisha akapumzika. Hatuelezwi zaidi, ila jambo hili lina umuhimu mpaka ikapelekea MUNGU kuliwekea mkazo hapa. Hali ya Adamu ilikuwa kinyume kabisa. Kwanza, aliingia katika mapumziko ya MUNGU kwa kuwa Sabato ya siku ya saba ilikuwa siku yake ya kwanza kamili ya maisha. Baada ya kuingia katika mapumziko ya MUNGU siku ya saba, kisha alifanya kazi.

Mpangilio huo huo unahusu ukombozi wa mwanadamu. Katika Kristo, MUNGU alikamilisha kazi ya ukombozi kupitia maisha Yake yasiyo na dhambi, kifo, na ufufuo. Mwanadamu huanza kufurahia kazi ya ukombozi wa MUNGU katika maisha yake kwa kupumzika katika kile ambacho MUNGU tayari amekwishakifanya kwa ajili yake. Anapumzika katika Ukweli kwamba Yesu alikufa kwa dhambi Zake na amempa uzima wa milele kama zawadi ya bure. Anapumzika katika Ukweli kwamba anakuwa na haki ya Kristo inayomfunika. Pia anapumzika katika Ukweli kwamba kwenye msalaba, nguvu ya asili yake ya dhambi ilivunjika, na sasa yuko huru kumtumikia MUNGU. Kila siku, anapumzika katika Ukweli kwamba Kristo anaishi ndani yake na ataishi maisha Yake kupitia Yeye ikiwa atachagua kumruhusu.

Muumini anapokuwa amepumzika katika Ukweli huu, anaweza "kufanya kazi," au kutumika kwa uaminifu na kumtii MUNGU katika maisha na utumishi. Mapumziko haya ni muhimu kwake ili kumtumikia MUNGU kwa uaminifu. Kwa mapumziko ninamaanisha kwamba anakubali kwa imani kile MUNGU amefanya kwa ajili ya ukombozi wake, na anaamini kabisa katika Kristo.

Katika Waebrania 4 tunapata maelezo ya kufanana ya dhana ya mapumziko katika kisa cha kushindwa kwa Israeli kuingia katika mapumziko ya MUNGU wakati walipokuwa jangwani:

"Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa MUNGU. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile MUNGU alivyostarehe katika kazi zake. Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili

kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.” (Waebrania 4:9-11).

Neno la MUNGU lina maelezo wazi kuhusu dhana ya mapumziko. Tunapokuwa tunaingia katika mapumziko ya MUNGU tunakoma jitihada zetu wenyewe. Tunaambiwa kwamba ni muhimu kwetu kutafuta kuingia katika mapumziko haya. Vinginevyo, tutashindwa katika kumtii MUNGU kwa sababu ya kutokuwa na imani, yaani kutoamini.

Njia pekee ya kushinda majaribu na dhambi ni kupumzika katika Ukweli kwamba Yesu anaishi ndani yetu na kumruhusu aishi maisha Yake kupitia sisi. Lazima tupumzike katika Ukweli huo kwa imani na tusihamasishe kazi ya MUNGU ya ukombozi katika maisha yetu kwa kujaribu kufanya kazi kama malipo au kuweka jitihada zetu wenyewe kutii. Sehemu yetu ni kuamini na kuchagua kumruhusu Kristo aishi maisha Yake ndani yetu. Tunapaswa kupumzika katika kazi Yake iliyokamilika. Kupumzika ndani ya Kristo ndiyo maana halisi ya mapumziko ya Sabato ambayo MUNGU anaita tuwe na uzoefu nayo:

“Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, MUNGU wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa. ” (Kutoka 20:8-11).

Sehemu yetu ni kuchagua na kuamini. Hii inahitaji kujisalimisha kwa Kristo kwa asilimia mia moja wakati wote.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Habari njema inafundishwa vipi katika kisa cha uumbaji?
- Ni Ukweli gani kuhusu Yesu ambao Wakristo wanapaswa kupumzika ndani yake?
- Kupumzika ndani ya Yesu kuna uhusiano upi na maisha ya Kikristo yanapaswa kuzingatiaje hili?
- Maana halisi ya mapumziko ya Sabato ni nini?
- Unapanga vipi kutumia somo la tafakari hii katika maisha yako wiki hii?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Omba pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete ufufuo katika maisha yako na katika kanisa Lake.
- Ili MUNGU akuelekeze kuingia katika maana halisi ya mapumziko ya Sabato.
- Kwa ajili ya watu walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Mtafuteni BWANA, maadamu anapatikana, Mwiteni, maadamu yu karibu; Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie BWANA, Naye atamrehemu; Na arejee kwa MUNGU wetu, Naye atamsamehe kabisa." (Isaya 55:6, 7,).

*Tusaidie kukutafuta BWANA na kuacha njia zetu za uovu na mawazo mabaya. Tufanye tukugeukie Wewe kwa moyo wetu wote. Utuhurumie na utusamehe.*

# SEHEMU YA V—UBATIZO WA ROHO NA USHIRIKA

# SIKU YA 33

# KITU FULANI KINAKOSEKANA

Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni uzoefu muhimu kwa Mkristo ikiwa atataka kuwa kama Yesu kwa maisha na utumishi. Kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu, Yesu anaishi kwa ukamilifu zaidi ndani ya mumini. Matokeo ya uhusiano huu wa karibu na Yesu, mumini ataanza kushuhudia ushindi wake mkubwa juu ya dhambi na atakuwa katika uhusiano wa maana zaidi na Mwokozi wake.

Uhusiano kati ya ubatizo wa Roho Mtakatifu na ushirika wa kweli wa Kikristo pia ni muhimu kwa Mkristo kuelewa na kufahamu. Hata kama tunapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, hatutakua kiroho kama MUNGU anavyokusudia bila ushirika wenye maana, unaotegemeana kwa pande zote na waumini wengine wenye Roho Mtakatifu. Kuwa na Roho Mtakatifu, na kubaki kwa namna fulani ukiwa peke yako na kujitegemea kutoka kwa Wakristo wengine wenye Roho Mtakatifu, siyo tu kutakwamisha ukuaji wetu wa kiroho lakini pia kunaweza kusababisha kupoteza ukamilifu wa uwepo wa Roho Mtakatifu katika maisha yetu.

Madhehebu yanayoangazia Maandiko, ikiwemo Waadventista wa Siku ya Saba, mara nyingi huwa na Maarifa mengi kuhusu Maandiko au maelekezo ya kiroho. Tunajua Kweli nyingi muhimu wa Biblia. Juhudi zetu za kueneza injili zinaangazia ukweli  ambao hututofautisha na madhehebu mengine. Hivyo, wengi wanaochagua kuwa washiriki wa kanisa hufanya hivyo kwa sababu ya Ukweli huo na wala siyo mapokeo ya kanisa au kile ambacho familia inafundisha.

Moja ya Ukweli ambao mara nyingi umenihuzunisha ni udhaifu wa jumla wa Waumini wa Siku ya Saba katika eneo la ushirika wa Kikristo. Sisi ni kundi lililo na uhuru wa kipekee kwa waumini. Lazima uwe na roho fulani ya kujitegemea ili kuwa Mwadventista wa Siku ya Saba kwa mara ya kwanza, kwa sababu kuchagua kuadhimisha Sabato ya siku ya saba kunatutofautisha sana naWakristo wengine.

Mara nyingi nimekuwa nikisoma maelezo ya waumini baada ya Pentekoste: "Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali." (Matendo 2:42).

Nilijua tulikuwa "sawa kabisa," kama kanisa, linapokuja suala la mafundisho. Hata hivyo, linapokuja suala la ushirika hatufanyi vizuri sana. Nimeona kwamba Waadventista wengi ni watu wanaofanya kazi kwa bidii na wanazitegemeza familia zao na wanayo bidii ya kuhudhuria ibada za asubuhi za Sabato. Ibada nyingi za kanisa huwa rasmi kwa kiasi fulani, na kuna muda mdogo au hakuna

mwingiliano kati ya waumini. Hivyo, ushirika wa wastani unajumuisha salamu za joto kabla na baada ya ibada. Kisha wengi wanaenda nyumbani na kurudi Jumamosi inayofuata. Kanisa letu lina mkutano wa maombi katikati ya wiki, ambao mara nyingi huwa na usomaji wa Biblia kutoka kwa mchungaji na msimu wa maombi. Hata hivyo, wengi wa washiriki wa kanisa wanahisi kwamba wana shughuli nyingi sana au wana uchovu mwingi kushiriki katika huduma hii ya katikati ya wiki.

Nimeona mara nyingi kwamba kama Wakristo wa Waadventista wa Siku ya Saba, ushirika unapaswa kuwa na jukumu muhimu zaidi kuliko jinsi ilivyo sasa. Tafakari hizi saba zitakuonyesha kwa nini Wakristo wenye Roho Mtakatifu wanapaswa kuingia katika ushirika wa karibu na wenzao waliojaa Roho Mtakatifu ikiwa wanataka kukua katika ukamilifu wa Kristo na kuwa tayari kwa kurudi Kwake.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Ni sifa zipi za kanisa la mapema la Kikristo ilikuwa nazo, kama ilivyoorodheshwa katika Matendo 2:42?
- Tafakari kuhusu kiasi gani cha ushirika wa kweli wa Kikristo unacho sasa, au ulivyokuwa zamani.
- Kwa nini unafikiri ushirika wa Kikristo ni muhimu katika maisha ya leo?
- Kwa nini unafikiri ushirika wa Kikristo ni muhimu katika kujitayarisha na kurudi kwa Kristo?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kumbatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na katika kanisa Lake.
- Ili MUNGU kufungua uelewa wako kuhusu kwa nini ushirika wa Kikristo ni muhimu.
- Kwa ajili ya watu walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

“Kwa kitambo kidogo nimekuacha; lakini kwa rehema nyingi nitakukusanya. Kwa ghadhabu ifurikayo nalikuficha uso wangu dakika moja; lakini kwa fadhili za milele nitakurehemu, asema BWANA, Mkombozi wako. Kwa maana jambo hili limekuwa kama maji ya Nuhu kwangu; maana kama nilivyoapa ya kwamba maji ya Nuhu hayatapita juu ya dunia tena, kadhalika nimeapa ya kwamba sitakuonea

hasira, wala kukukemea. Maana milima itaondoka, na vilima vitaondolewa; bali wema wangu hautaondoka kwako, wala agano langu la amani halitaondolewa; asema BWANA akurehemuye." (Isaya 54:7-10).

*Uzitupilie mbali katika dhambi zetu—Utuhurumie na kutuokoa na dhambi zetu. Turejeshe katika nguvu za kiroho.*

## SIKU YA 34

## KANISA LA AWALI NA USHIRIKA

Ninaamini binafsi kwamba BWANA anawasukuma watu Wake kuangalia kwa karibu jinsi ilivyokuwa katika kanisa la Agano Jipya. Waadventista wa Siku ya Saba, kama masalia ya MUNGU kwa waumini duniani. Tumekuwa tukijitahidi kushikilia mafundisho ya Neno la MUNGU, kama ilivyokuwa kanisa la Agano Jipya. Ninaamini kwamba sasa BWANA anatuita si tu kuendelea kwa uthabiti "katika fundisho la mitume," bali pia kuendelea kwa uthabiti katika "ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali" (Matendo 2:42). MUNGU anawaita watoto Wake kuwa watu Wake wa masalio kama kanisa la Agano Jipya, si tu katika mafundisho bali pia katika ushirika. Ushirika ni sehemu muhimu kwa watu wa masalia wa MUNGU. Tukizingatia hili, hebu tuangalie kwa karibu jinsi kanisa la mapema la MUNGU lilivyokuwa.

Kitabu cha Matendo kinatuambia kwamba Wakristo wa awali walikutana katika hekalu/sinagogi na kutoka nyumba hadi nyumba: "Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe." (Matendo 2:46).

Wakristo walipokuwa hawakubaliki katika nyumba za ibada za Kiyahudi, nyumba zao zilikuwa kitovu cha ibada yao na ushirika. Nyumba za waumini zilikuwa sehemu walipokutana kwa sifa, ushirika, na mafundisho. Mistari mingi ya biblia inazungumzia nyumba katika Agano Jipya ambapo Wakristo walikutana: "Hata walipoingia, wakapanda orofani, walipokuwa wakikaa; Petro, na Yohana, na Yakobo, na Andrea, Filipo na Tomaso, Bartholomayo na Mathayo, Yakobo wa Alfayo, na Simoni Zelote, na Yuda wa Yakobo." (Matendo 1:13).

"Mwanamke mmoja, jina lake Lidia, mwenye kuuza rangi ya zambarau, mwenyeji wa Thiatira, mcha MUNGU, akatusikiliza, ambaye moyo wake ulifunguliwa na BWANA, ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo. Hata alipokwisha kubatizwa, yeye na nyumba yake, akatusihi, akisema, Kama mmeniona kuwa mwaminifu kwa BWANA, ingieni nyumbani mwangu mkakae. Akatushurutisha." (Matendo 16:14, 15).

"Na Wayahudi wakaona wivu, wakajitwalia watu kadha wa kadha katika watu ovyo wasio na sifa njema, nao wakakutanisha mkutano, wakafanya ghasia mjini, wakawaendea watu wa nyumba ya Yasoni, wakataka kuwapeleka mbele ya watu wa mji; na walipowakosa, wakamkokota Yasoni na baadhi ya ndugu mbele ya wakubwa wa mji, wakipiga kelele, wakisema, Watu hawa walioupindua

ulimwengu wamefika huku nako, na Yasoni amewakaribisha; na hawa wote wanatenda mambo yaliyo kinyume cha amri za Kaisari, wakisema na kwamba yupo mfalme mwingine, aitwaye Yesu. Wakafadhaisha ule mkutano na wakubwa wa mji walipoyasikia hayo. Nao walipokwisha kumtoza dhamana Yasoni na wenziwe wakawaacha waende zao." (Matendo 17:5-9).

"Ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia neno lo lote liwezalo kuwafaa bali naliwafundisha waziwazi, na nyumba kwa nyumba" (Matendo 20:20).

"Nisalimieni Epaineto, mpenzi wangu, aliye malimbuko ya Asia kwa Kristo." (Warumi 16:5).

"Tena naliwabatiza watu wa nyumbani mwa Stefana; zaidi ya hao, sijui kama nalimbatiza mtu ye yote mwingine" (1 Wakorintho 1:16). "Makanisa ya Asia wawasalimu. Akila na Priska wawasalimu sana katika BWANA, pamoja na kanisa lililoko ndani ya nyumba yao" (1 Wakorintho 16:19).

"Wasalimuni ndugu walioko Laodikia, na Nimfa, na kanisa lililo katika nyumba yake." (Wakolosai 4:15).

Mitume walielewa kwa hakika umuhimu wa ushirika mdogo wa nyumbani. Kwa miaka mitatu na nusu walikuwa wakimwabudu na kushiriki na Yesu kwa namna hii. Tunaweza kuelewa jinsi ilivyokuwa kawaida kwa mitume kuendelea na aina hii ya ushirika wa vikundi kidogo kwa mamia na maelfu ya watu walipomkubali Kristo. Mtindo wa ushirika wa nyumbani ungefanya iwe rahisi sana kufuatilia na kupanga idadi kubwa inayojiunga na kanisa kila siku:

"Wakimsifu MUNGU, na kuwapendeza watu wote. BWANA akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa." (Matendo 2:47).

Kikundi hiki kidogo cha ushirika kilihudumia ukuaji wa kanisa vizuri. Inakadiriwa kwamba katika karne ya tatu, Wakristo milioni sita walikuwa wanaishi katika Dola ya Kirumi. Vikundi hivi vidogo vya ushirika vilisaidia ukuaji. Washiriki wapya walijumuishwa kwa haraka na kushirikia na wengine kwa kina. Pia itaonekana kwamba vikundi hivi vilikuwa si tu kwa ajili ya kulea bali vilikuwa na tabia ya kueneza injili. Vikundi vya nyumbani vilikuwa na uwezo wa kusaidia kanisa kukua hata katika nyakati za mateso makali. Pia, kadiri idadi ya kanisa la nyumbani ilivyokuwa kubwa, washiriki walikuwa wanalazimika kugawanyika na kuunda vikundi vipya katika nyumba zingine.

Ushirika wa karibu unaotokana na kikundi kidogo huunda mshikamano wa karibu sana miongoni mwa washiriki wa kikundi. Kuimarishana kwa pande zote kunafanyika kwa urahisi zaidi. Ni katika mazingira haya kwamba waumini

wenzetu wanapata nguvu kutoka kwa kila mmoja. Mwanadamu ameumbwa kuwa na nguvu zaidi anapokuwa pamoja na wengine kuliko anavyokuwa peke yake. Wakristo wa leo wanahitaji nguvu zinazotokana na ushirika wa karibu kama ule ambao kanisa la awali la mitume lilikuwa nayo. Kama vile MUNGU alivyosema mwanzoni, "Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye." (Mwanzo 2:18). Si vizuri kwa Mkristo kujitahidi kukabiliana na nguvu za Shetani na dunia peke yake.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Wakristo wa awali walikutana wapi kwa ajili ya ushirika, na kwa nini?
- Vikundi vya ushirika wa nyumbani vikundi?
- Kwa nini unafikiri ushirika wa Kikristo ni muhimu katika maisha ya leo?
- Je, unafikiri kutakuwepo wakati ambapo ushirika wa nyumbani utakuwa muhimu? Kwa nini ni hivyo, au kwa nini si hivyo?
- Je, ungependa kuwa sehemu ya kikundi cha ushirika wa nyumbani kilichojazwa Roho? Ikiwa ndiyo, unawezaje kuwa sehemu ya hicho?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kumbatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na katika kanisa Lake.
- Ili MUNGU akuongoze wewekuwa sehemu ya kikundi cha ushirika.
- Kwa ajili ya watu walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Maana kama vile kijana amwoavyo mwanamwali, ndivyo wana wako watakavyokuoa wewe; na kama vile bwana arusi amfurahiavyo bibi arusi, ndivyo MUNGU wako atakavyokufurahia wewe. Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalemu; hawatanyamaza mchana wala usiku; ninyi wenye kumkumbusha BWANA, msiwe na kimya; wala msimwache akae kimya, mpaka atakapoufanya imara Yerusalemu, na kuufanya kuwa sifa duniani." (Isaya 62:5-7).

*BWANA, tufanye kuwa na maombi kwako daima hadi tupate uamsho kwetu na kulisifu Jina Lako katika jamii hii.*

# SIKU YA 35

# UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU NA VIKUNDI VYA USHIRIKA

Ubatizo wa Roho Mtakatifu na vikundi vya ushirika huendana pamoja. Vyote ni muhimu kwa Mkristo ili kukua katika ukamilifu wa Kristo. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni muhimu kwa washiriki wa msingi wa kundi la ushirika ili kundi liweze kufanya kazi kama MUNGU anavyokusudia. Tunaona hili waziwazi katika uzoefu wa Kristo na mitume. Mitume kumi na wawili walikuwa na uhusiano wa karibu sana wa binafsi na Kristo na kati yao wenyewe kwa miaka mitatu na nusu. Hata hivyo, tunawapata wakigombana kati yao walipokuwa wanaelekea kwenye karamu ya Pasaka kabla ya Kristo kuchukuliwa na umati na hatimaye kusulubiwa: "Yakatokea mashindano kati yao, kwamba ni nani anayehesabiwa kuwa mkubwa." (Luka 22:24).

Hawakuwa bado wamefikia kiwango cha ushirika wa upendo na kujitolea kwa MUNGU au kwa kila mmoja wao katika miaka hiyo. Kuwa sehemu ya kundi la ushirika, ambapo Kristo alikuwa kiongozi, haikuleta mabadiliko yanayohitajika ili kukua katika ukamilifu wa Kristo. Baadaye, tunaona walibadilika kwa kiasi kikubwa. Nini kilichobadilisha hali hiyo? Ni kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste ndiko kufanya tofauti. Kuanzia siku hiyo, wao, na wengine wote waliokuwepo, waliingia katika ushirika wa Kikristo wa kweli ambao MUNGU anataka kila muumini apate uzoefu:

"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali. Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, wakimsifu MUNGU, na kuwapendeza watu wote. BWANA akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa." (Matendo 2:42, 46, 47).

Namna ya ushirika wa kanisa la awali haiwezi kutokea wakati wa ibada ya asubuhi ya Sabato kwa sababu ya mienendo ya mahusiano inayohitajika kati ya waumini waliojaa Roho. Njia pekee ambayo uzoefu huu wa aina hiyo unaweza kutokea ni katika vikundi vidogo vya ushirika wa Kikristo. Huduma ya ibada ya Sabato ya siku zote ni muhimu. Jambo kuu ni kwamba hiyo peke yake haitoshi.

Umuhimu wa waumini waliojaa Roho kufanya ushirika pamoja katika vikundi vidogo unaonyeshwa kwa mifano miwili. Paulo anatupa mfano mmoja wa umuhimu wa uhusiano wa kudumu kati ya waumini katika barua yake ya kwanza

kwa Wakorintho, katika sura ya 12. Anatumia mfano wa mwili wa binadamu kuelezea kanisa na washirika wake. Anaonyesha jinsi ilivyo muhimu kwa kila sehemu ya mwili kuhudumia mwili. Waumini waliojaa Roho wanahitajiana wao kwa wao, kila mmoja wao kwa mwingine. Wanapaswa kuhudumiana kama vile moyo wako, mkono wa kulia, macho, nk., yanavyohudumia sehemu nyingine za mwili wako. Kutokana na mfano huu, inaonekana wazi kwamba ni muhimu kwa kila sehemu ya mwili kubaki katika uhusiano wa karibu na wa kudumu na sehemu nyingine za mwili. Ni vikundi vya ushirika wa nyumbani ndivyo vinavyomwezesha muumini aliyejaa Roho kudumisha uhusiano wa karibu na wa kudumu na mwili wa Kristo, ambao unawawezesha washiriki wa mwili kuhudumiana:

"Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho Yeye Yule; mwingine imani katika Roho Yeye Yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho Yule Mmoja; na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda Roho Huyo Mmoja, Yeye Yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo Yeye. Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo." (1 Korintho 12:7-12).

"Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa MUNGU, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo. (Waefeso 4:11-16).

Mfano mwingine wa umuhimu wa vikundi vya ushirika wa nyumbani unaweza kuonekana karibu na mahali pa kuota moto. Fikiria kwa muda wakati ulipokuwa ukikaa karibu na moto wa kuota na kuangalia kuni zinavyokuwa zikiungua. Ili moto uendelee kuwaka, ilikuwa muhimu kuongeza kuni mara kwa mara. Kama makaa yenye moto yanatenganishwa na mengine yanayoungua, yatapunguza moto wake na kuisha. Hii inaonyesha wazi umuhimu wa ushirika wa karibu wa Kikristo. Ili muumini aliyejaa Roho adumishe "moto" usije kuzima maishani

mwake, anahitaji si tu kuendelea kuomba kwa MUNGU kwa ajili ya kujazwa na Roho (Waefeso 5:18), bali pia lazima aendelee kubaki katika ushirika na waumini wengine waliojaa Roho.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Kuna uhusiano kati ya ubatizo wa Roho Mtakatifu na vikundi vya ushirika vya Kikristo?
- Je, ushirika wa mitume na Yesu kwa miaka tatu na nusu ulikuwa wa kutosha kuwaandaa Washirika kwa ukaribu aliotaka Yesu kuwa nao? Kwa nini ndivyo, au kwa nini si hivyo?
- Ni mfano upi alitumia mtume Paulo kueleza jinsi Wakristo wanavyopaswa kuwa na ushirika wa karibu na kila mmoja wao?
- Ni mfano gani kutoka kwa maumbile unaotufundisha somo hili pia?
- Je, unahisi kwamba ushirika wa karibu wa Kikristo ni muhimu kwa maisha yako ya kiroho? Kwa nini unafikiri hivi?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kubatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na katika kanisa Lake.
- Ili MUNGU abariki juhudi zako za kuwa sehemu ya kikundi cha ushirika.
- Kwa ajili ya watu walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Nafsi yangu imeyeyuka kwa uzito, Unitie nguvu sawasawa na neno lako." (Zaburi 119:28).

*Hali yangu ya dhambi imenifanya niwe dhaifu. Nigeuze mbali na dhambi zangu. Nitegemeze kiroho kama ulivyoahidi.*

## SIKU YA 36

## KANISA

Neno la Kigiriki linalotumika katika Agano Jipya kwa ajili ya kanisa ni ***ekklesia***, ambalo linamaanisha “walioitwa.” Wakati wanaume na wanawake wanapojibu mwito wa Roho Mtakatifu wa kumkubali Kristo kama Mwokozi wao, wanakuwa sehemu ya ekklesia, wale walioitwa.

Tunapojifunza Agano Jipya, tunagundua kuwa kuna vipande viwili muhimu sana kuhusu kanisa. Wale walioitwa wanaitwa kuamini mafundisho ya Biblia. Paulo anaelezea kanisa kwa maneno haya: “15 Lakini nikikawia, upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya MUNGU, iliyo kanisa la MUNGU aliye hai, nguzo na msingi wa Kweli.” (1 Timotheo 3:15).

Paulo anaita kanisa “nguzo na msingi wa Kweli.” Wale walioitwa wanapaswa kuamini, kuishi, na kufundisha Ukweli wa Neno la MUNGU.

Kuna kipande kingine muhimu cha kanisa kinachoonyeshwa katika Waraka wa kwanza wa Yohana:

“Hilo tulililoliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi: na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo.” (1 Yohana 1:3).

Kipengele hiki ni muhimu kwa kanisa na Agano Jipya linakiita “ushirika.” Kwa maana rahisi, ushirika hakika si dhana mpya. Kwa kweli, katika maana moja tunashirikiana tunapokuwa na ibada kanisani siku ya Sabato au tunapohudhuria shughuli za kijamii za kanisa pamoja. Hata hivyo, dhana ya ushirika katika Agano Jipya ni pana zaidi kuliko vile Wakristo wengi wanavyotambua.

Neno la Kigiriki lililotafsiriwa kama ushirika ni *koinonia*. Aina hii ya nomino inamaanisha kushiriki, kushirikiana, au kuwa na ushirika wa moja kwa moja, (siyo kuwa pamoja kimtandao bali ni kuwa pamoja na wenzako walipo na kushirikiana nao). Aina ya kitenzi hiki inamaanisha kuwasiliana, kusambaza, na kutoa. Hivyo, *koinonia* pamoja maana yake ni zaidi ya kukaa pamoja katika Patakatifu kwa ajili ya ibada ya Sabato au kucheza michezo pamoja katika shughuli za kijamii. Maana ya ushirika katika Agano Jipya inaenda zaidi ya hapo. Kimsingi, inamaanisha kuhudumiana. Si tu kujua majina ya kila mmoja, kujua mahali tunapoishi, na kuwakaribisha kwa joto kanisani asubuhi ya Sabato. Bali namaanisha kushiriki matumaini, ndoto, changamoto, na maumivu ya kila mmoja. Inamaanisha kumruhusu MUNGU atutumie sisi katika kuhudumia kila

mmoja. Kulingana na Agano Jipya, ushirika wa kanisa ni mkusanyiko wa watu, walioitwa kutoka duniani na MUNGU kuwa jamii ya wenye imani ya Biblia na wanaowasiliana, kusambaza, kutoa, na kuhudumiana kwa namna ya moja kwa moja.

Ushirika unamaanisha kushiriki matumaini, ndoto, changamoto, na maumivu ya kila mmoja. Inamaanisha kumruhusu MUNGU atutumie sisi kumhudumia kila mmoja.

Ikiwa Wakristo hawapo katika aina hiyo ya uhusiano na kila mmoja wao, wanakosea sana mpango wa MUNGU kwa kanisa Lake. Tunaweza kuwa tunashika Sabato na kwenda kanisani, lakini ikiwa hatupo katika ushirika wa Kweli wa koinonia, hatuna uzoefu wa kweli kwa maana ya kanisa kulingana na kiwango kamili cha Mwenyezi MUNGU.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Je, Neno "kanisa" linamaanisha nini katika Agano Jipya?
- Je, sehemu mbili gani za kanisa la Kikristo zilizopop katika Agano Jipya?
- Je, Inamaanisha nini kuwa katika ushirika wa koinonia na kila mmoja?
- Je, uko katika ushirika wa koinonia na Wakristo wengine?
- Ikiwa ndiyo, uzoefu wako na ushirika huu umekuwa vipi?
- Ikiwa hapana, Je, ungependa kuwa katika aina hii ya ushirika?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kubatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na katika kanisa Lake.
- Ili MUNGU abariki juhudi zako za kuwa sehemu ya kikundi cha ushirika wa koinonia, au kubariki kundi lako la ushirika ikiwa uko katika moja.
- Kwa ajili ya watu walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Mcheni BWANA, enyi watakatifu wake, Yaani, wamchao hawahitaji kitu." (Zaburi 34:9).

*Tufanye tuwe na hofu na heshima Kwako kwa mioyo yetu yote. Tukomboe kutokana na mambo yanayotuzuia kupata tunachohitaji kiroho.*

# SIKU YA 37

# FAMILIA YA MUNGU

Dhambi ilivunja familia ya MUNGU. Mpango wa ukombozi ulianzishwa kurejesha familia hii. Paulo anawaeleza wale ambao wameitikia mwito wa MUNGU maishani mwao kwa njia ifuatayo: “Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake MUNGU.” (Waefeso 2:19).

Neno la Kigiriki linalotafsiriwa kama “nyumba” ni ***oikeios.*** Tunapokuwa waumini katika Yesu Kristo, tunakuwa sehemu ya nyumba ya MUNGU. Tunakuwa sehemu ya familia Yake.

Kwa asili, tunapofikiria kuhusu kanisa, mara nyingi tunawaza huwa tunawaza ile taasisi na mkusanyiko. Hatufikirii sana kuhusu kanisa kama familia ndogo. Hata hivyo, kanisa la awali kulingana na mtazamo wa Kibiblia na kihistoria lilikuwa limejumuisha vikundi vidogo vya nyumbani. Vikundi hivi vya ushirika vilifanya kazi kama familia.

Wakati Paulo anaelezea hisia zake mwenyewe kwa familia ya MUNGU huko Thessaloniki, anaeleza uhusiano unaopaswa kuonekana katika familia ya MUNGU: “Bali tulikuwa wapole katikati yenu, kama vile mlezi awatunzavyo watoto wake mwenyewe. Vivyo hivyo nasi tukiwatumaini kwa upendo mwingi, tuliona furaha kuwapa, si Injili ya MUNGU tu, bali na roho zetu pia, kwa sababu mmekuwa wapendwa wetu.” (1 Wathesalonike 2:7, 8,)

Uhusiano wa aina hii ya upendo hauwezi kutokea katika mazingira mkusanyiko mkubwa. Ikiwa shughuli zetu za kanisa zinajumuisha mara nyingi kuwasili kanisani asubuhi ya Sabato, kuwasalimia marafiki wetu, na kisha kurudi nyumbani, hatuwezi kufikia kiwango hiki cha uhusiano wa familia.

Kwa mfano, ni nini ungedhani kingetoea kama ungejaribu kukutana na familia yako mara moja kwa wiki, na kutengana nayo kila wiki na kisha kukutana mara moja kwa wiki kwa saa moja au mbili, mkisalimiana kwa kifupi, kisha kuketi kwenye mabenchi na kusikiliza mtu anatoa hotuba ya mada fulani? Baada ya hapo, mnarudi kwa njia zenu tofauti hadi baada ya siku saba mnapokutana tena na kusalimiana, na kuketi kwenye mabenchi yaliyo katika mistari, na kusikiliza mada nyingine? Unafikiri umoja wa familia hiyo ungekuwaje? Nadhani ungejiuliza kama kweli hiyo ni familia. Wengi tumeona kuwa mtindo wetu wa umoja wa familia ulikuwa na nafasi kubwa ya kuboreshaw. Kwa jinsi ya

kushangaza na kwa huzuni, Wakristo wengi wanajaribu kuwa familia ya kanisa kwa kutumia mtindo huu wa familia.

Katika familia yenye afya, washiriki wanajua kila mmoja kwa undani. Wanajua hofu, matumaini, ndoto, msongo wa mawazo, na changamoto za kila mmoja. Katika familia yenye upendo na kujali, washiriki wanakuwepo kwa ajili ya kutiana moyo kwa maneno na vitendo.

Familia ya MUNGU inapaswa kufanya kazi kwa njia hiyo hiyo. Hata hivyo, familia ya MUNGU ina faida moja muhimu zaidi kuliko familia ya kawaida ya kidunia. Familia ya MUNGU inapata matunda na karama za Roho katika mazingira yao. MUNGU Mwenyewe Ndiye anayehudumia washiriki wa familia hiyo. Anafanya hivyo kupitia kila mshiriki wa familia anapokuwa amepokea na kubatizwa kwa Roho Mtakatifu. Uhusiano wa karibu na MUNGU ambao kubatizwa kwa kila siku kunaleta unamruhusu Kristo kuishi ndani na kuhudumiana kupitia kila muumini, lakini mtindo huu wa familia unaweza kutokea tu katika mazingira ya kikundi kidogo cha ushirika.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- MUNGU alikusudia aina gani ya mahusiano kwa watoto Wake?
- Dhambi ilifanya nini katika mpango wa MUNGU?
- Mpango wa ukombozi unafanya nini kwa familia ya MUNGU iliyojaa mapengo?
- MUNGU anataka washiriki wa kanisa Lake kuwa na aina gani ya uhusiano na kila mmoja?
- Ni mazingira gani yanayofaa zaidi kwa hili kutokea?
- Je, ungependa kufurahia mfano wa MUNGU kwa familia Yake ya kanisa?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kumbatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na katika kanisa Lake.
- Ili MUNGU akuongoze kuingia katika aina ya uzoefu wa familia ya kanisa anayotaka wewe kuwa nayo.
- Kwa ajili ya watu walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

“Mateso ya mwenye haki ni mengi, Lakini BWANA humponya nayo yote.” (Zaburi 34:19).

*Tuelekeze kuwa watu Wako wenye haki waliotubu dhambi. Tukomboe kutoka kila dhiki ambayo Shetani anajaribu kutuletea.*

## SIKU YA 38

## MATUNDA YA ROHO NA USHIRIKA

Vipengele viwili muhimu vya vikundi vya ushirika vya Kikristo vilivyo na mafanikio ni matunda na karama za Roho zinazojitokeza katika maisha ya washiriki. Kuna njia moja tu ya kuhakikisha kwamba haya yapo: washiriki wanapaswa kuwa na Roho Mtakatifu.

Katika tafakari ya leo tutazingatia jukumu la Tunda la Roho katika ushirika. Ikiwa tunda la Roho halipo na halijakomaa katika maisha ya washiriki, hawataweza kupata faida kamili kutoka kwa kikundi cha ushirika. Vilevile, hawatakuwa na tabia inayohitajika kuhudumia washiriki wenzao. Matunda ya Roho yanatajwa katika barua ya Paulo kwa Wagalatia: “Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, wema, imani, unyenyekevu, kiasi: juu ya mambo kama haya hakuna sheria” (Wagalatia 5:22, 23).

Tunda la kwanza ni upendo. Neno la Kigiriki hapa ni upendo wa agape, aina ya juu zaidi ya upendo. Huu ni upendo wa MUNGU kwetu, ukiwa na lengo la kufanya kile kilicho bora kwa anayependwa. Yesu alielezea aina hii ya upendo katika Mathayo 5:44:

“Lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi.”

Paulo alielezea upendo wa agape katika 1 Wakorintho 13:4-7:

“Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote.”

Tunda hili la upendo litamfanya mshiriki wa kikundi cha ushirika kuonyesha uelewa na hisia kwa wengine katika kikundi. Mfano wake utaweza kupunguza sauti kali au mitazamo katika wengine. Vilevile, hatakuwa na mtazamo wa kumhukumu mwingine wakati mshiriki anaposhiriki na kikundi, changamoto zake binafsi. Badala yake, tunda la upendo litamfanya ahisi huruma na mapenzi. Atamfikia mwenzake kwa maneno ya uponyaji, kumhamasisha, na ukombozi kwa yule anayehitaji msaada.

Kila tunda linalofuata katika orodha ya Paulo lina jukumu muhimu katika kudumisha aina ya hali inayohitajika kwa kikundi cha ushirika cha Kikristo kutekeleza madhumuni ya MUNGU.

Sifa hizi, zinazounda tunda la Roho, ni ngumu kufikiwa bila kujazwa na Roho Mtakatifu. Wakristo waliopakwa mafuta na Roho Mtakatifu wanahitajika ili kikundi cha ushirika kutimiza kusudi lake la kutoa angahewa ambayo washiriki wote wanaweza kukua katika ukamilifu wa Kristo:

"Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa MUNGU, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo." (Waefeso 4:11-16).

Tunda la Roho, huonekana tu katika maisha ya muumini kupitia kubatizwa na Roho Mtakatifu, na lazima liwepo katika maisha ya washiriki wa msingi wa kikundi cha ushirika. Tunda hili huleta tabia ya Kristo kwenye kikundi. Ni kupitia kwa watu MUNGU hutuonyesha upendo Wake. Hivyo itakuwa kupitia kwa Wakristo waliojazwa Roho Mtakatifu kwamba MUNGU ataonyesha upendo Wake kwa wote wanaokuja kwenye ushirika, iwe ni Wakristo au si Wakristo.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Kila mshiriki wa ushirika anapaswa kuwa na nini ili Tunda la Roho liwepo?
- Orodhesha mambo tisa yaliyopo kwenye tunda la Roho na kueleza jinsi kila moja inavyokuwa baraka kwa wale katika kikundi cha ushirika.
- Una mpango gani wa kuwa sehemu ya kikundi hiki cha ushirika?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kubatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na katika kanisa Lake.
- Ili MUNGU adhihirieshe tunda la Roho katika maisha yako na kukuongoza kwenye kikundi cha ushirika kilichojazwa Roho Mtakatifu.

- Kwa ajili ya watu walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Maana mtatoka kwa furaha, Mtaongozwa kwa amani; Mbele yenu milima na vilima vitatoa nyimbo; Na miti yote ya kondeni itapiga makofi. Badala ya michongoma utamea msunobari, Na badala ya mibigili, mhadesi; Jambo hili litakuwa la kumpatia BWANA jina, Litakuwa ishara ya milele isiyokatiliwa mbali." (Isaya 55:11-13).

*Tuangalie upya ukamilifu wa furaha na amani ndani Yako. Ondoa kichaka cha miiba na miiba ya kiroho iliyoko maishani mwetu na katika kanisa letu. Hebu iwepo furaha kubwa na kusherehekea kwa ajili Yako. Lihimidiwe Jina Lako katika kusanyiko hili.*

## SIKU YA 39

## KARAMA ZA ROHO NA USHIRIKA

Kiungo kingine muhimu kwa kikundi cha ushirika kuwa na mafanikio ni utendaji wa karama za Roho katika kikundi hicho. Kwa kuwa karama za kiroho huonekana kupitia waumini waliojaa Roho Mtakatifu, ni muhimu kwa washiriki kuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu.

Sura kadhaa katika Agano Jipya zinajadili karama za kiroho. Maandiko maarufu kuhusu karama za kiroho yanapatikana katika barua za Paulo: "4 Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja;

"Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja; Vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake. Basi kwa kuwa tuna karama zilizo mbalimbali, kwa kadiri ya neema mliyopewa; ikiwa unabii, tutoe unabii kwa kadiri ya imani; ikiwa huduma, tuwemo katika huduma yetu; mwenye kufundisha, katika kufundisha kwake; mwenye kuonya, katika kuonya kwake; mwenye kukirimu, kwa moyo mweupe; mwenye kusimamia kwa bidii mwenye kurehemu, kwa furaha." (Warumi 12:4-8).

"Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye yule; mwingine imani katika Roho yeye yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja; na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye. Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo." (1 Wakorintho 12:7-12).

"Lakini kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo. Hivyo husema, Alipopaa juu aliteka mateka, Akawapa wanadamu vipawa. Basi neno hilo, Alipaa, maana yake nini kama siyo kusema kwamba yeye naye alishuka mpaka pande zilizo chini za nchi? Naye aliyeshuka ndiye yeye aliyepaa juu sana kupita mbingu zote, ili avijaze vitu vyote. Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu" (Waefeso 4:7-11).

Karama hizi zinahudumia jukumu muhimu sana katika ukuaji wa kiroho wa muumini binafsi na kanisa. Paulo anatumia mfano wa mwili wa mwanadamu na orodha ya viungo mbalimbali vya mwili, akionyesha umuhimu wa kila sehemu katika utendaji wa mwili wote. Hitimisho ni wazi. Ni muhimu kwa kila sehemu ya mwili kufanya kazi kwa ufanisi ili mwili wote kwa ukamilifu, uwe na afya na kuwa na mafanikio katika kutimiza kilichokusudiwa kufanywa: “Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi. Mguu ukisema, Kwa kuwa mimi si mkono, mimi si wa mwili; je! Si wa mwili kwa sababu hiyo? Na sikio likisema, Kwa kuwa mimi si jicho, mimi si la mwili; je! Si la mwili kwa sababu hiyo? Kama mwili wote ukiwa jicho, ku wapi kusikia? Kama wote ni sikio ku wapi kunusa? Bali MUNGU amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka. Lakini kama vyote vingekuwa kiungo kimoja, mwili ungekuwa wapi? Lakini sasa viungo ni vingi, ila mwili ni mmoja. Na jicho haliwezi kuuambia mkono, Sina haja na wewe; wala tena kichwa hakiwezi kuiambia miguu, Sina haja na ninyi. Bali zaidi sana vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa vinyonge zaidi vyahitajiwa zaidi.” (1 Wakorintho 12:14-22).

Paulo anasema kwamba “viungo vitunzane kila kiungo na mwenziwe” (mstari wa 25). Wakati vinapofanya kazi katika mwili wa kanisa, karama zinathibitisha baraka kubwa kwa kila kiungo cha mwili wa Kristo.

Inapaswa kuwa wazi kutokana na maelezo ya Paulo kwamba karama za Roho ni muhimu ikiwa Mkristo binafsi na kanisa wanapaswa kukua. Kauli ya Paulo kwamba viungo vinapaswa “vitunzane kila kiungo na mwenziwe” ni rejeleo wazi la ushirika wa Kweli wa Kikristo. Ili kupata uelewa wa kina kwa viungo vya kanisa letu, lazima tuwajue kwa dhati au kwa kweli. Tunapaswa kuwa huru kushiriki mahitaji yetu ya kina, changamoto, matumaini, na ndoto zetu ikiwa tunataka kuhudumiana. Paulo alirejelea umuhimu wa kuhudumiana wakati aliposema:

“Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo.” (Wagalatia 6:2).

Aina hii ya ushirika haiwezi kutokea kwa kuendesha kanisa kwa njia ya desturi au jadi. Ikiwa uhusiano wetu pekee na washiriki wa kanisa letu ni kukutana nao asubuhi ya siku ya Sabato na kuwapa salamu za joto-joto “Sabato Njema, na mambo mema” na kuishia hapo tu, itakuwa haiwezekani kwa ushirika wa Kibiblia kutokea.

Karama za Roho zitafanya kazi kwa njia ya vitendo katika kubariki wale walio katika ushirika. Kwa mfano, karama ya ufundishaji katika Agano Jipya ni ile inayofundisha Neno la MUNGU. Inafahamika jinsi ilivyo muhimu kama karama katika kikundi cha ushirika. Lengo la kikundi si kuwa kikundi cha masomo ya Biblia pekee, na kisha kuambiana nendeni kwa amani, hata kama mtu amefiwa

au ana shida ya mahali pa kuishi. Kuna nafsi ya masomo ya kina ya Biblia; hata hivyo, kipande kikuu cha kikundi cha ushirika wa Kikristo ni ibada na ushirika wa uponyaji. Karama ya kufundisha inayolingana na kusudi hili itakuwa mbaraka mkubwa kwa wote watakaohudhuria. Masomo yatakuwa kwa ujumla mafupi kutoka kwenye Maandiko badala ya kipindi kirefu cha kufundisha. Msimamo utawekwa kwenye matumizi ya kivitendo ya Maandiko kwa masuala binafsi yanayojitokeza katika mazingira ya kikundi.

Mfano mwingine ni karama ya kutia moyo. Wakati karama hii inapoonekana, MUNGU ataitumia kusema maneno ya kutia moyo, faraja, na matumaini, hasa kwa washiriki wa kikundi ambao wanateseka na kukabiliana na tatizo kubwa maishani mwao. Ufunuo wa karama hii huleta ushauri wa Kibiblia wenye kutia moyo miongoni mwawashiriki wa kikundi.

Karama hizi za kiroho zinazojitokeza katika kikundi cha ushirika wa Kikristo zitawezesha Roho Mtakatifu kuhudumia washiriki wote.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Kila mshiriki wa ushirika anapaswa kuwa na nini ili karama za Roho ziwepo?
- Orodhesha baadhi ya karama za Roho na eleza jinsi kila moja itakavyotumika na MUNGU kuhudumia wale walio katika kikundi cha ushirika.
- Je, umeshuhudia MUNGU akidhihirisha karama za kiroho kupitia wewe kuhudumia wengine? Ikiwa ndiyo, ni karama zipi?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hili, pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na katika kanisa Lake.
- Ili MUNGU adhihirishe karama za Roho katika maisha yako ambazo amekuchagulia, na kukuongoza kuzitumia karama hizi ili kuhudumia wengine.
- Kwa ajili ya watu walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

"Pigeni tarumbeta katika Sayuni, Takaseni saumu, kusanyeni kusanyiko kuu; Kusanyeni watu, litakaseni kusanyiko, Kusanyeni wazee, kusanyeni watoto, Na hao wanyonyao maziwa; bwana arusi na atoke chumbani mwake, Na bibi arusi katika hema yake. Hao makuhani, wahudumu wa BWANA, na walie Kati ya patakatifu na madhabahu, Na waseme, Uwaachilie watu wako, Ee BWANA, Wala usiutoe urithi wako upate aibu, Hata mataifa watawale juu yao; Kwani waseme kati ya watu, Yuko wapi MUNGU wao? Hapo ndipo BWANA alipoona wivu kwa ajili ya nchi yake, akawahurumia watu wake. BWANA akajibu, akawaambia watu wake; Tazameni, nitawaletea nafaka, na divai, na mafuta, nanyi mtashiba kwa vitu hivyo; wala sitawafanya tena kuwa aibu kati ya mataifa" (Yoeli 2:15-19).

*Tupe shauku kubwa ya kukusanyika kwa makusudi na kukutafuta kwa dhati kwa maombi. Tusaidie kutukuza Jina Lako kupitia sisi ili wengine waone kuwa Upo pamoja nasi. Tuonee huruma na kutufanyia mambo mapya ili tuweze kuzaa matunda na kustawi kama watu Wako.*

## SIKU YA 40

## VIKUNDI VYA USHIRIKA NA UKUAJI WA KANISA

Ushirika wa waumini utaweza kuchukua jukumu muhimu katika katika uleaji wa kiroho, kihisia, na hata kimwili ambao MUNGU anataka kila mmoja wetu apate.

Ukuaji unapaswa—na lazima iwe—lengo la kila kikundi cha ushirika wa Kikristo. Ikiwa kikundi hakikui, hakifanyi kazi kama MUNGU anavyokusudia. Kumbuka, ubatizo wa Roho Mtakatifu umetolewa kwa ajili ya ukuaji wetu binafsi wa kiroho na kwa ajili ya kueneza injili:

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." (Matendo 1:8).

Hivyo basi, watu wasiokuwa waumini, au wale ambao si washiriki wa kanisa, wanapaswa kuwa mashahidi.

Ni muhimu kwa ukuaji wetu wa kiroho binafsi kuwa na sehemu katika kuwaleta wengine kwa Kristo. Tunapaswa kufuata amri ya MUNGU ya kuwa "Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi." (Mwanzo 1:28). MUNGU angeweza kutumia malaika katika kazi ya kuleta roho au watu wasikie injili; hata hivyo, hakufanya hivyo. Kwa nini? Anajua umuhimu wa kila mmoja wetu kushiriki moja kwa moja katika kufikia wengine kwa Kristo. Kutoka RYU tunaona kwamba:

"Ikiwa utakwenda kufanya kazi kama Kristo anavyokusudia wanafunzi Wake wafanye, na kuleta roho kwa Yeye, tutaona hitaji la uzoefu wa kina na maarifa makubwa katika mambo ya MUNGU, na tutaona kiu na njaa ya haki. Tutamwomba MUNGU, na imani yetu itaimarika na nafsi yetu itakunywa kwa kina kutoka katika kisima cha wokovu. Kukutana na upinzani na majaribu kutatufanya tukimbilie kwenye Biblia na maombi. Tutakua na kuongezeka katika neema na maarifa ya Kristo, na tutaendelea kupata uzoefu wa utajiri" (Njia Salama, uk. 80).

Msaada unaotolewa na kikundi cha ushirika utaweza kuwa na jukumu kubwa katika jitihada zetu za kuwafikia wengine. Wanakikundi watashirikiana katika maombi kwa wale tunaojaribu kuwafikia. Ushauri wa wale walio na uzoefu zaidi katika kuleta roho utakuwa msaada mkubwa kwetu. Baba wa kiroho na mama

katika kikundi wataweza kutumiwa na MUNGU kusaidia wale wasio na uzoefu mkubwa katika kuongoza wengine kwa Kristo.

Kikundi cha ushirika kitatoa mazingira mazuri kwa mtu anayemtafuta MUNGU, kwani atakutana na watu wenye upendo na kujali watakaomkubali kama alivyo. Mtafutaji wa injli atapata mazingira ambayo Roho wa MUNGU anaweza kufanya kazi kwa nguvu kubwa kwa ajili ya uongofu wake kwa Kristo. Tunaposoma katika kitabu cha Matendo, tunapata kwamba Wakristo wa awali walipokuwa wakishirikiana kila siku, kanisa liliongezeka:

"Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, wakimsifu MUNGU, na kuwapendeza watu wote. BWANA akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa." (Matendo 2:46, 47).

MUNGU atahudumia waumini na wale wasiokuwa waumini waliopo katika kikundi cha ushirika. Atayafanya haya kupitia tunda la Roho na karama za Roho. Muktadha wa kikundi kidogo cha ushirika hubadilisha kabisa mtindo wa kijadi au desturi katika kuenenza injili pale watu wanapohudhuria mkutano kwa kujibu tangazo lililotumwa kwa vipeperushi au barua. Kiini cha kikundi cha ushirika ni uhusiano wa karibu, wa kina, na wa mmoja mmoja. Wakati asiyeamini anapoanza kukumbatia Ukristo na zile Kweli mpya za Biblia katika mazingira ya ushirika huu, anafanya hivyo katika muktadha wa uhusiano binafsi wa karibu na mshiriki mmoja wa kikundi. Hapo ndipo atapata mazingira ya ukombozi yanayochochea ukuaji wake binafsi wa kiroho.

**Tafakari na Majadiliano Binafsi**

- Je, vikundi vya ushirika wa kweli wa Kikristo vina madhumuni gani?
- Orodhesha mapendekezo juu ya jinsi kikundi cha ushirika kinavyoweza kuwa na ufanisi katika kuwafikia wengine nje ya kikundi kwa ajili ya Kristo?
- Una mpango gani wa kuwa sehemu ya kikundi cha ushirika kinachokua na kutumiwa na MUNGU kumtangaza Kristo pamoja na wengine?

**Kujishughulisha Kuomba**

Wasiliana na mwanamaombi mwenzako na jadili tafakari hii pamoja naye. Ombeni pamoja:

- Ili MUNGU aendelee kuwabatiza kila mmoja wenu kwa Roho Wake Mtakatifu.
- Ili MUNGU alete uamsho katika maisha yako na katika kanisa Lake.

- Ili MUNGU wakuongoze kuwa sehemu ya kikundi cha ushirika kinachokua na kutumiwa na Yeye kuwaleta wengine kwa Kristo.
- Kwa ajili ya watu walioko kwenye orodha yako ya maombi.

**Jumuisha Andiko Lifuatalo Katika Maombi Yako**

“Furahini, basi, enyi wana wa Sayuni, mkamfurahie BWANA, MUNGU wenu; kwa kuwa yeye huwapa ninyi mvua ya masika, kwa kipimo cha haki, naye huwanyeshea mvua, mvua ya masika, na mvua ya vuli, kama kwanza. Na sakafu za kupepetea zitajaa ngano, na mashinikizo yatafurika kwa divai na mafuta. Nami nitawarudishia hiyo miaka iliyoliwa na nzige, na parare, na madumadu, na tunutu, jeshi langu kubwa nililotuma kati yenu. Nanyi mtakula chakula tele na kushiba, na kulihimidi jina la BWANA, MUNGU wenu, aliyewatendea mambo ya ajabu; na watu wangu hawatatahayari kamwe. Nanyi mtajua ya kuwa mimi ni katikati ya Israeli, na ya kuwa mimi ndimi BWANA, MUNGU wenu, wala hakuna mwingine; na watu wangu hawatatahayari kamwe. Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono.” (Yoeli 2:23-28).

*Tupe shauku thabiti kwa Roho Wako Mtakatifu na utuelekeze kuomba kwa ajili ya ubatizo wa mvua ya kwanza ya Roho Mtakatifu katika maisha yetu na kwa ajili ya kumiminwa kwa mvua ya masika ya Roho Wako Mtakatifu. Dhihirisha karama za Roho Wako kupitia sisi na ututumie kutukuza Jina Lako. Funua nguvu Zako katikati yetu na katika jamii yetu ili wengi waje kukujua Wewe kama MUNGU wao na Mwokozi.*

## Kiambatanisho A: Orodha ya Maombi ya Kila Siku

Orodhesha watu watano au zaidi ambao wameacha kanisa, au wamerudi nyuma kiroho au ambao hawakuwahi kuwa washiriki wa kanisa, ambao unapanga kuwaombea na kuwasiliana nao katika siku 40 zijazo ili BWANA awalete kwenye kundi Lake kwa maandalizi ya kurudi kwa Kristo hivi karibuni. (Watu hawa wanapaswa kuwa wale wanaoishi katika eneo lako ili kuwaalika kanisani wakati wa siku 40 zijazo).

1. -----------------------------------------------------------
2. -----------------------------------------------------------
3. -----------------------------------------------------------
4. ----------------------------------------------------------
5. ----------------------------------------------------------

Omba kwa ajili ya watu hawa kila siku ukidai Maandiko yafuatayo kwa niaba yao. Yamechukuliwa toka katika *Praying Church Source Book*, kurasa 128-129.

- Ili MUNGU awavute Kwake Yeye Mwenyewe (Yohana 6:44)
- Ili wajitahidi kumjua MUNGU (Matendo 17:27)
- Ili waamini Neno la MUNGU (1 Wathesalonike 2:13)
- Ili Shetani afungwe ili asiwafungie macho kwa Ukweli na ushawishi wake katika maisha yao "uangushwe chini" (2 Kor. 4:4; 10:4, 5)
- Ili Roho Mtakatifu afanye kazi ndani yao (Yohana 16:8-13)
- Ili wageuke kutoka kwenye dhambi (Matendo 3:19)
- Ili waamini katika Kristo kama Mwokozi (Yohana 1:12)
- Ili wamtii Kristo kama BWANA (Mathayo 7:21)
- Ili waote mizizi na kukua ndani ya Kristo (Wakolosai 2:6, 7)

Kwa maombi na tafakari, tumia orodha ya Activities to Show You Care (angalia Kiambatanisho B) ili kubaini kile ambacho BWANA anataka ufanye ili kuwafikia wale walioko kwenye orodha yako ya maombi katika siku 40 zijazo.

## Kiambatanisho B: Vitendo vya Kuonyesha Upendo Wako

Haya ni mapendekezo ya mambo unayoweza kufanya kwa wale walioko kwenye orodha yako ya maombi ili kuonyesha kwamba unawajali. Ongeza kwenye orodha hii kama BWANA anavyoongoza.

1. Wasiliana ili kujulisha kile unachothamini kuhusu wao
2. Tuma kadi ukishiriki kile MUNGU alichoweka moyoni mwako kuwaambia
3. Tuma kipande cha Maandiko yenye kutia moyo
4. Wasiliana na kuomba pamoja nao
5. Toa mwaliko wa kuja nyumbani kwako kwa ajili ya chakula
6. Toa mwaliko wa kutoka nao kwenye mgahawa kwa chakula cha mchana
7. Tuma kadi ya kuzaliwa
8. Tuma kadi yenye kutia moyo
9. Chukua kitu ulichopika
10. Waalike kuungana nawe katika manunuzi, safari ya kwenda makumbusho n.k.
11. Tuma kadi ya hongera, au kadi ya pole pale inapohitajika
12. Mpe mtoto wao kadi ya kuzaliwa na zawadi inapofaa
13. Waalike kuhudhuria kanisani
14. Katika wakati mwafaka, uliza kama wangependa kupokea masomo ya Biblia

15. ____________________________________________

16. ____________________________________________

17. ____________________________________________

18. ____________________________________________

19. ____________________________________________

20. ____________________________________________

## Kiambatanisho C: Mapendekezo ya Salamu kwa Mawasiliano ya Maombi

Habari, _________________________(jina la mtu wa kupigia simu).

Huyu ni______________________________(jina lako).

Kanisa langu lina msisitizo maalum juu ya maombi, na linahitaji tuchague watu watano kuomba kwa ajili yao katika siku 40 zijazo.

Nimekuchagua wewe kuwa mmoja wa watano nitakaowaombea.

Je, ungependa niombe nini hasa kwa niaba yako, kama vile familia, kazi, shida ya kiafya, nk.

(Andika hapa chini kile anachotaka umwombee).

Nathamini fursa ya kuomba hili kwa ajili yako katika siku 40 zijazo.

Asante, _________________________(jina la mtu wa kuwasiliana naye). Nitawasiliana nawe.

## Kiambatanisho D: Baada ya Siku 40 za Maombi na Masomo ya Kiroho…

Sasa kwa vile umekamilisha siku 40 za maombi na masomo ya kiroho, huenda usihitaji uzoefu huu ulioshiriki na BWANA, na ushirika unaofurahia unaweza kupotea. Hivyo, nini kifanyike baadaye?

Moja ya uwezekano ni kwamba uanze kujifunza kwa kina masomo yaliyowasilishwa katika hii tafakari. Waweza kuendelea mfululizo wa hivi vitabu -Majina ya vitabu kwa mpangilio wa sehemu za tafakari ni:

- Ubatizo wa Roho Mtakatifu
- Ubatizo wa Roho na Maombi
- Ubatizo wa Roho Mtakatifu na Uinjilisti
- Ubatizo wa Roho Mtakatifu na Kudumu ndani ya Kristo
- Ubatizo wa Roho Mtakatifu na Ushirika wa Mvinyo Mpya

Ikiwa hii ni shauku yako, ningependekeza uanze na kitabu cha kwanza kilichoorodheshwa, Ubatizo wa Roho Mtakatifu, na uanze kujifunza pamoja na mwenzi wako wa maombi au kikundi cha ushirika ulichoshiriki katika siku 40 za maombi na masomo ya kiroho pamoja nawe. Huenda ukataka kuwalika wengine kujiunga nawe na kikundi chako. Kisha kila mmoja binafsi na kama kundi endeleeni kupiga hatua kupitia vitabu vya kuboresha maisha ya Kiroho pamoja Mfano Njia Salama, Tumaini la Vizazi Vyote, Huduma ya Mkristo, Maombi, Uinjilisti, NK. Hii itamwezesha BWANA kuimarisha uzoefu wako na Yeye, ambao umeanza katika maisha yako katika siku 40 zilizopita.

Au pale unapopenda, hamia kwenye masomo mengine yanayohusiana na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Vitabu vifuatavyo vinaweza kutumika kwa masomo binafsi na ya kikundi ili kujifunza kuhusu nyanja nyingine za uzoefu wa ubatizo wa Roho. Vinaweza kujifunza kwa mpangilio wowote kama vile BWANA atakavyoongoza.

- Ubatizo wa Roho na Kusubiri MUNGU
- Ubatizo wa Roho na Kurudi kwa Utukufu kwa Kristo
- Ubatizo wa Roho na Ukombozi
- Ubatizo wa Roho na Ujumbe wa Haki kwa Imani wa mwaka wa 1888
- Ubatizo wa Roho na Matukio ya Mwisho ya Dunia

Pili, endelea kuomba kwa ajili ya wale walioko kwenye orodha yako ya maombi na kuwa karibu nao. Pia, ongeza wengine kwenye orodha yako kama vile BWANA

atakavyoongoza, na kama kundi fikirieni shughuli za kupanga ili kuwaalika wale walioko kwenye orodha ya maombi kuhudhuria.

Kristo anataka tafakari binafsi ya kila siku, maombi, na kuwafikia wengine kuwa sehemu muhimu ya maisha ya kila Mkristo. Ikiwa kipande hiki cha maisha yako kitaishia katika siku hizi 40 tu za maombi na masomo ya kiroho, hutakua kuufikia ukamilifu wa Kristo ambao anataka upate. Pia, hii ndiyo njia pekee ya kuwa tayari kwa kurudi kwa Kristo hivi karibuni. Kwa kuwa ndiyo njia pekee ya uhusiano wetu wa karibu na Kristo kuendelea na kukua. MUNGU akubariki sana katika muda wako endelevu wa maombi na kujifunza, na juhudi zako za kushiriki na wengine.

Zingatia: Vitabu vyote vilivyoorodheshwa vinapatikana kupitia vituo vya vitabu vya Wasabato au kwenye www.spiritbaptism.org.

Ukitaka vitabu vingine vya Kiswahili -Tembelea

MaarifaMtandaoni.Com

RohoYaUnabii.Org

RohoYaUnabii.Africa

MaarifaMtandaoni.Africa

SpiritofProphecy.Swahili-in near future

Huduma ya uhamishoniUghaibuniMtandaoniMajumbani